SUPA JACKPOT
TZS. 1,159,574,731
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Jela** miaka 10 kwa kuua mtalaka

UKURASA 7



**BELLINGHAM: NAFURAHIA KUCHEZA NA VINICIUS JR**

UKURASA 22


# Nipashe

Alhamisi Oktoba 5, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581454

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




UKURASA WA 2

**Mahakama** yapangua wasimamizi mirathi ya mali za Bilionea Mrema

UKURASA WA 3

**Mjane** aangua kilio kizimbani akitoa ushahidi

UKURASA WA 17

**SMZ** yawekeza bil. 21/- kudhibiti mfumuko wa bei





# Bei za mafuta zaibua mjadala

• **Wasafirishaji** wajipanga kupandisha nauli, LATRA yatoa angalizo... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 8

**UPATIKANAJI MAJI SHULENI WAATHIRI KIWANGO CHA ELIMU**

SHULE ya Msingi ya Mtakatifu Vincent, Tarafa ya Itigi, wilayani Manyoni, mkoani Singida inakabiliwa na tatizo la huduma ya majisafi na salama...

**Kardinali Rugambwa awataka Watanzania kudumisha amani**

UKURASA 4

**Mtaji wa bil 48/-, wanufaika maelfu**

**Maombi kwa wiki mbili kuanzia keshokutwa**

**Vigezo na masharti:**

-Ualimu Sayansi, Hisabati
-Usafiri na Usafirishaji
-Afya, Ufundi na Nishati
-Madini, Sayansi, Ardhi
-Kilimo na Mifugo



# Kumekucha mikopo ya wanafunzi wa diploma

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA SC YATEPETA MBARALI UK.24

**KATUNI** UK.6

# Bei mpya za mafuta zaibua mjadala

**Na Waandishi Wetu**

WADAU wa usafiri nchini wamelalamikia kupanda kwa bei za dizeli na petroli huku wakibainisha kuwa kunaathiri biashara zao, hivyo kuiomba serikali kuangalia namna ya kudhibiti hali hiyo.

Wamesema kupanda kwa bei ya mafuta kutaongeza bei ya bidhaa mbalimbali na kusababisha kupanda kwa gharama za maisha.

Huku hali ikiwa hivyo, wasafirisha wamesema wanajipanga kuiandikia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) barua ya kuomba kupandishwa kwa nauli. Wamesema wamevumilia kwa muda mrefu huku bei hizo zikizidi kupanda jambo ambalo sasa halivumiliki.

Waliyasema hayo jana saa chache tangu Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), kutangaza kupanda kwa bei ya jumla ya mafuta ya petroli kwa Sh. 68 na dizeli Sh.189 katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara yenye bandari zinazopokea mafuta.

Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi Mkoa wa Dar es Salaam (DARCOBOA), Sabri Mabrouk, alisema wana mpango kuiandikia LATRA kuomba kupandishwa nauli ili kufidia hasara waliyoipata kwa muda mrefu.

Alisema wamevumilia hasara tangu mafuta hayo yanauzwa Sh. 2,000 hadi sasa yamefika Sh. 3,000.

Meneja wa Mabasi ya Tashrif, Hamisi Shemweta, alisema kuendelea kupanda kwa mafuta kunawapa hasara ikizingatiwa kuwa bei ya nauli haijapanda hasa kipindi hiki ambacho wateja ni wachache kwa kuwa si msimu wa safari.

Alisema basi lenye uwezo wa kubeba abiria 57, kwa sasa linabeba abiria 38 kwa safari moja sawa na abiria 76 kwenda na kurudi huku likitumia lita 260 za mafuta ya dizeli na kutembea jumla ya kilometa 720.

“Faida inayopatikana ni ndogo sana, tulivumilia tukiamini kuwa hali hii ni ya muda mfupi na itapita. Ila kwa hali ilivyo sasa hakuna jinsi zaidi ya serikali kupitia LATRA itufikirie kwa kupandisha nauli,” alisema.

Jijini Arusha, baadhi ya wakazi wa jiji hilo, walisema kupanda kwa bei ya mafuta kumesababisha kuongezeka kwa gharama za maisha huku madereva wa mabasi madogo ya abiria, aina ya Toyota Coaster, zinazofanya safari kati ya miji ya Moshi na Arusha, wakisema hawawezi kuendelea na nauli za sasa, zaidi ya kupandisha nauli.

Akizungumza na Nipashe, Amos Wema, dereva wa Coaster kati ya Arusha na Moshi, alisema: “Usafirishaji hauwezi kufanyika bila mafuta. Bei zimepanda na sisi lazima tutazame hasara kutokana na ongezeko la bei ya mafuta.

“Usishangae kuanzia kesho (leo) ukapanda Coaster au kifodi (Toyota Hiace) ukakutana na ongezeko la nauli. Kila mmoja anataka asiumie ndiyo maana tunasema serikali na hao EWURA, watutazame na sie waridhie tutakapopandisha nauli.”

Mkoani Kilimanjaro, wakazi wa Hai na Siha, wameiomba EWURA kudhibiti upandaji holela wa nauli za mabasi madogo aina ya Toyota Hiace na Toyota Noah, zinazotoa huduma za usafiri katika miji ya Moshi, Bomang’ombe na Siha kwa kuwa wananchi wa chini wanaumia na hawana kipato.

Mkazi wa Karansi, Wilaya ya Siha, Joroboam Mollel, alisema hata kama soko la dunia bei zinazidi kupanda, wanajua pia serikali imefanya juhudi za kufuta tozo na imechukua hatua za kukabiliana na upandaji wa bei za mafuta, hivyo kuomba serikali kutafuta namna nyingine ya kupunguza makali hayo ya maisha kutokana na ongezeko la bei ya mafuta.

Katibu wa Chama cha Wasafirishaji kwa Njia ya Barabara Mkoa wa Dodoma (TAROTWU), Mussa Nsese, alisema mabadiliko ya bei za mafuta yataathiri uchumi wa wananchi kutokana na kupanda kwa gharama za maisha.

Akizungumza na Nipashe kuhusu kupanda kwa bei za mafuta kulikotangazwa na EWURA, Nsese alisema gharama za maisha zitapanda kutokana na mabadiliko ya bei za nishati hiyo.

“Hizi bei zinakwenda kugusa kila mtu awe msafirishaji au mwananchi wa kawaida kwani itasababisha wasafirishaji wa bidhaa kutokana na kupanda kwa mafuta, kufidia gharama hizo kwa wananchi wa kawaida.

“Mtu hawezi kukubali kukodi Fuso kutoka Mbeya kuleta viazi hapa Dodoma halafu chipsi kavu ikaendelea kuuza Sh. 2,000, lazima itapanda tu kwa hiyo wananchi tusishangae kesho (leo) tukiamka na bei tofauti na leo (jana) katika bidhaa mbalimbali muhimu,” alisema.

**BEI MPYA**

Bei mpya zilizotangazwa na EWURA, petroli kwa bei ya rejareja katika Bandari ya Dar es Salaam imeongezeka kufikia Sh. 3,281 kutoka Sh. 3,213 huku dizeli ikifikia Sh. 3,448 kutoka Sh. 3,259.

Mkoa wa Tanga petroli imepanda hadi kufikia Sh. 3,327 kutoka Sh. 3,259 na dizeli Sh.3,494 kutoka Sh. 3,305. Bei mpya kwa Arusha petroli ni Sh. 3,365 kutoka Sh. 3,297 huku dizeli ikiuzwa Sh. 3,532 kutoka Sh. 3,343.

Mikoa mingine ni Kilimanjaro petroli sasa ni Sh. 3,355 kutoka Sh. 3,286 na dizeli Sh. 3,522 kutoka Sh. 3,333. Manyara petroli ni Sh. 3,403 kutoka Sh. 3,335 na dizeli Sh. 3,570 kutoka Sh. 3,382.

EWURA ilitaja sababu za kuongezeka kwa bei hizo kuwa ni kupanda kwa gharama za mafuta katika soko la dunia hadi kufikia asilimia 4.21 na gharama za uagizaji wa mafuta kufikia asilimia 17 kwa petroli, asilimia 62 kwa dizeli na asilimia nne kwa mafuta ya taa.

Sababu nyingine, ilisema ni uamuzi wa wazalishaji wakubwa wa mafuta duniani kupunguza uzalishaji na vikwazo vya kiuchumi ambavyo nchi ya Urusi imewekewa na mataifa ya magharibi.

**Imeandikwa na Jenipher Gilla (DAR), Godfrey Mushi (ARUSHA), Anjela Mhando (MOSHI) na Paul Mabeja (DODOMA).**



Wakazi wa Kijiji cha Lengijave, Kata ya Olkokola, wilayani Arumeru mkoani Arusha, wakichota maji katika kisima kijijini hapo jana. Eneo hilo limekuwa na shida ya maji kutokana na ukame unaosababishwa na mabadiliko ya tabianchi. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Mahakama yapangua wasimamizi mirathi ya mali za Bilionea Mrema

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

MAHAKAMA Kuu, Kanda ya Arusha, imetengua na kuwaondoa kwenye usimamizi wa mirathi ya aliyekuwa mfanyabiashara tajiri jijini Arusha, Bilionea Faustine Mrema, aliyefariki dunia mwaka 2017.

Bilionea Mrema alikuwa akimiliki hoteli za kitalii zenye hadhi ya nyota tano zilizoko jijini hapa ambazo ni Impala, Naura Springs na Ngurdoto Mountain Lodge.

Wasimamizi hao wa mirathi walioenguliwa, walikuwa wanasimamia mali za Bilionea Mrema, zenye thamani ya Sh. bilioni 18.3.

Jana, mahakama hiyo chini ya Jaji Devota Kamuzora, aliyekuwa akisikiliza shauri dogo namba 170 la mwaka 2022, aliwapa haki ya kusimamia mirathi hiyo watoto wa marehemu ambao ni Randy Mrema na Lulu Mrema.

Watoto hao wawili ndio waliofungua shauri hilo la mirathi ya baba yao, wakiwapinga waliokuwa wasimamizi wa awali, Janeth Kimaro na Vivian Mrema, ambao nao ni watoto wa marehemu Mrema.

Akisoma uamuzi uliotenguliwa na wasimamizi wa mirathi hiyo, Jaji Kamuzora, alisema mahakama imezingatia sababu zilizotolewa na waleta maombi na waliokuwa wasimamizi wa mali kushindwa kukusanya mali na kulipa madeni, huku kukiwa na udanganyifu.

Kwa mujibu wa Jaji Kamuzora, sababu nyingine iliyozingatiwa ni wasimamizi wa awali wa mirathi kutokamilisha kazi ya kukusanya na kugawa mirathi ya marehemu kwa wakati.

Sababu nyingine, kwa mujibu wa Jaji Kamuzora ni ukubwa wa madeni na kesi zilizokuwa zikiendelea mahakamani kuhusiana na mali za marehemu.

Kutokana na sababu hizo, Jaji aliwapa wasimamizi hao wapya wa mali za marehemu miezi sita kukamilisha kukusanya, kulipa madeni na kugawa mali za marehemu kwa wanufaika.

Aidha, Jaji Kamuzora katika uamuzi wake, alisema iwapo kuna mali iliuzwa kizembe, familia inaweza kufungua mashtaka mahakamani.

Kabla ya uamuzi huo kutolewa, Wakili George Njooka, alidai mahakamani hapo kuwa athari zinazoweza kujitokeza iwapo mahakama itabatilisha uamuzi wa wasimamizi wa mirathi, ni kusababisha gharama kubwa pasipo msingi.

**NJE YA MAHAKAMA**

Akizungumzia alivyopokea uamuzi huo, msimamizi wa mirathi hiyo kwa sasa, Randy Mrema, alisema ameupokea kwa furaha, lakini anaona ana deni kubwa la kurekebisha yale yote yaliyotarajiwa kufanywa na wasimamizi waliopita.

Randy alisema amejipanga kukamilisha kulipa madeni, kufufua biashara zilizokuwa zimekufa ikiwa ni pamoja na hoteli lakini kwa kushirikiana bega kwa bega na wakurugenzi wengine kwenye kampuni ambazo Bilionea Mrema alikuwa mmiliki.

Mwaka 2021, baadhi ya mali za Bilionea Mrema ziliuzwa kwa amri ya mahakama ili kufidia madai ya wafanyakazi wa hoteli za Impala na Naura Spring yaliyotokana na malimbikizo ya mishahara zaidi ya Sh. bilioni 1.3.

Mali zilizouzwa ni pamoja na viwanja vitalu namba 16, 17, 18, 19, 20, 21, 22 na 23 vilivyopo eneo la Uzunguni jijini Arusha na kuwezesha kupatikana kwa Sh. bilioni 2.65.

**CNBMI TANZANIA LIMITED**

**Cheti cha Usajili Namba 127673 Sheria ya Makampuni, 2002 (KIFUNGU 334 (1))**

**MAAMUZI YA HIARI YA WANAHISA KUFUNGA KAMPUNI**

Umma unafahamishwa kuwa katika kikao cha CNBMI TANZANIA LIMITED (kampuni), yenye usajili namba 127673, kilichofanyika tarehe 20 September 2023 azimio maalumu lilipitishwa:

- Kufuatana na kifungu 331(1)(b) cha Sheria ya Makampuni ya 2002, kuwa kampuni ifutwe kwa hiari; na
- Wanahisa wamemteua LINDA ALLAN MWAMBETE wa Mikumi House, 368 Msasani Road, Oysterbay, S.L.P 9673, Dar es Salaam, Tanzania kuwa mfilisi wa kampuni.

Umma na wahusika wanafahamishwa kupeleka madai yao kwa usaili ndani ya siku thelathini (30). Maombi yote yatayopelekwa baada ya siku 30 kuisha hayataandikishwa.

**LINDA ALLAN MWAMBETE,**
**MFILISI wa CNBMI TANZANIA LIMITED**

# Mjane aangua kilio kizimbani

**Na Grace Gurisha**

MJANE Winnie Kiabulio (64) ameangua kilio akiwa ndani ya kizimba cha mahakama baada ya kumwona kijana aliyemkaba na kumwibia mali zake.

Amedai kuwa akimwona kijana huyo, anapata mshtuko kwa kuwa siku ya tukio, alinusurika kifo.

Shahidi huyo alimtambua mshtakiwa George Simeo kwa sura na kwa 'tattoo' ya mkono wake wa kushoto ambayo aliiona wakati anaokota vitu vyake chini ya miguu yake vilivyokuwa vimemwagika wakati wa purukushani za kumwibia.

Winnie alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Ramadhani Rugemalila wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kinondoni, Kivukoni, Dar es Salaam wakati anajibu maswali ya mshtakiwa Simeo ambaye anatuhumiwa kumtenda kitendo hicho.

Mjane huyo alifikia hatua hiyo ya kulia kutokana na maswali aliyokuwa anaulizwa na mshtakiwa kana kwamba aliyemfanyia kitendo hicho si yeye kwa kumtaka aeleze tattoo iliyopo katika mkono wake ni ya mchoro gani.

"Uwe na hofu ya Mungu wewe kijana, wewe ni mjukuu wangu, huna hata aibu. Una nguvu za kufanya kazi, kwanini unakuja kuwavamia wazee na kuwaibia? Mimi nina presha, nikimwona tu huyu kijana ninataka kuwa chizi," alidai.

Baada ya shahidi kudai hayo, Hakimu Rugemalira alimtaka mama huyo atulie na asiwe chizi kama alivyodai kwa kuwa hawataendelea mbele na kama akishindwa, basi angeahirisha kesi hiyo hadi siku nyingine.

Huku akiendelea kulia, shahidi huyo alidai: "Siku ya tukio hili niliumia sana mheshimiwa. Kwahiyo, siwezi kusahau aliyenifanyia kwa sababu ilikuwa ni asubuhi, mwanga wa kutosha kabisa!

"Tangu ninazaliwa sijawahi kufanyiwa tukio kama hili na pia sijawahi kufika mahakamani hata siku moja, ni leo hii. Ninaomba mheshimiwa umpe adhabu kali ili iwe fundisho kwa wengine," alidai shahidi.

Hapo Hakimu Rugemalira akaingilia, akamweleza shahidi kuwa muda wa kutoa ombi hilo la adhabu kali bado haujafika.

Wakili wa Serikali Rhoda Kamungu alipelekea maji ya kunywa, shahidi akanywa, akateta na wakili, akarudi kwenye hali yake ya kawaida na kesi ikaendelea.

Akiongozwa na Kamungu, shahidi alidai kuwa Juni 25 mwaka huu, saa 12:30 asubuhi, alikuwa ameahidiana na mtu waonane Bagamoyo, hivyo aliomba lifti kwa jirani yake kwa kuwa kila siku za mapumziko alikuwa anakwenda huko.

Alidai kuwa akiwa njiani kuelekea kwa jirani yake anayeishi nyumba ya tano kutoka kwake huko Kinondoni Morocco, Mtaa wa Kalembo, aliona bodaboda inakuja kwa kasi huku ikiwa imebeba abiria.

"Yule abiria alishuka. Nilishtuka sana, nikasema 'Yesu nisaidie!' Alikuwa ameshika kisu na nyundo, akaniambia nitoe vyote nilivyonavyo. Kwa harakaharaka nikataka kuiokoa simu yangu.

"Nikataka kuirusha ndani ya ukuta wa nyumba niliyokuwa nikienda, lakini iligonga geti ikarudi kwenye miguu yangu, vitu vya kwenye pochi vilimwagika.

"Mshtakiwa akiwa anafanya mambo ya 'komfuu' akainama, akaokota vitu vyangu," alidai.

Shahidi huyo alidai kuwa pochi hiyo ilikuwa na Sh. 830,000 na nyuma ya kava la simu kulikuwa na Dola za Marekani 250. Alidai kama wana hofu ya Mungu basi watakuja kulipia hilo.

Shahidi huyo pia aliitambua pikipiki namba MC 253 DTG ambayo inadaiwa kutumiwa na mshtakiwa huyo na mwenzake wakati wa uporaji huo.

Hakimu Rugemalira alimtaka mshtakiwa amwoneshe mkono wake wa kushoto shahidi, alivyovuta mkono wa shati, ni kweli alikuwa na tattoo.

Kesi imeahirishwa hadi Oktoba 16 mwaka huu kwa ajili kuendelea kusikilizwa.



Mwanafunzi Shamsa Juma wa kidato cha pili Shule ya Sekondari Mashujaa, Sinza Dar es Salaam, akichangia hoja katika mkutano wa kutoa elimu kuhusu madhara ya rushwa ya ngono na ukatili wa kingono, ulioandaliwa na Shirika la Usawa Kijinsia Tanzania (SUKITA) juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kumekucha mikopo ya wanafunzi wa diploma

## ●Masharti yatajwa, watengewa bilioni 48/-

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amezindua mwongozo wa utoaji wa mikopo kwa wanafunzi 8,000 yenye thamani ya Sh. bilioni 48 kwa ngazi ya stashahada (diploma) kwa mwaka wa masomo 2023/24.

Katika uzinduzi wa mwongozo huo jana jijini Dar es Salaam, Waziri Mkenda alisema kuanza utoaji wa mkopo kwa ngazi ya wanafunzi wa stashahada ni mageuzi yanayolenga kuboresha sekta ya elimu ya juu chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema uamuzi wa kuanza kutoa mikopo kwa wanafunzi wa stashahada unatokana na marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo yaliyofanywa mwaka 2017.

Kwa mujibu marekebisho hayo, hivi sasa bodi inaanza kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaosoma stashahada katika fani zenye uhitaji mkubwa wa wataalamu.

Alisema wanafunzi 8,000 watakaodahiliwa kusoma stashahada katika fani za kipaumbele watakaribishwa kuomba mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 48.

Waziri alizitaja fani hizo kuwa ni Afya na Sayansi Shirikishi, Ualimu kwa masomo ya Fizikia na Hisabati, Usafiri na Usafirishaji, Uhandisi na Nishati, Madini na Sayansi ya Ardhi pamoja na Kilimo na Mifugo.

Alisema serikali imefanya tathmini ya uhitaji wa wataalamu katika nchi na kubaini maeneo sita ambayo yameshatangazwa katika Gazeti la Serikali la Septemba 29 mwaka huu kuwa na uhitaji mkubwa wa wataalamu katika ngazi ya kati.

"Kwa mfano, serikali imejenga hospitali, zahanati na vituo vya afya nchini kote ambavyo vinahitaji wataalamu. Serikali imejenga na kukarabati shule ambazo zinahitaji walimu wa sayansi.

"Serikali pia inatekeleza mageuzi makubwa katika sekta za mafuta, gesi na madini na sekta ya kilimo kupitia mpango wa Building Better Tomorrow (BBT).

"Tunaosimamia sekta ya elimu, baada ya kufanya tathmini tumeona tuanze na maeneo haya sita ili kuwapa fursa vijana wetu ya kupata ujuzi na kuajirika baada ya kuhitimu masomo yao," alisema Prof. Mkenda.

Waziri huyo alisema mwongozo wa utoaji mikopo kwa wanafunzi wa stashahada ulianza kupatikana jana katika tovuti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, tovuti ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) na tovuti ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

Waziri huyo pia alishauri wanafunzi, wazazi na walezi wausome na kuuzingatia wakati wa kuomba mkopo huo.

Alisema dirisha la kupokea maombi kwa njia ya mtandao litakuwa wazi kwa muda wa siku 15 kuanzia Oktoba 7 hadi 22 mwaka huu.

"Ingawa mwongozo huo unapatikana kuanzia leo, wanafunzi, wazazi na walezi watumie siku nne kuusoma kabla ya kuanza kuomba," Waziri Mkenda alifafanua.

Alielekeza maombi yote ya mkopo yatafanyika kwa kwa njia ya mtandao kupitia www.olas.heslb.go.tz na waombaji wa mikopo hawatapaswa kutuma nakala ngumu kwenda HESLB badala yake watatuma nakala laini.

Alisema akunti ya SIPA ambayo mwanafunzi ataifungua ili kuomba mkopo ni sehemu ya kupata taarifa za mwenendo wa ombi na iwapo atatakiwa kufanya marekebisho.

"Mwombaji ahakikishe anatunza na kukumbuka nywila yake ili aweze kuingia katika akaunti na kupata taarifa mbalimbali kuhusu ombi lake," alisema.

Waziri Mkenda alisema baada ya kumaliza masomo, mnufaika atapaswa kurejesha mkopo kwa kiwango cha asilimia 15 kutoka kwenye mshahara wa mwezi kama ilivyo kwa wanufaika wengine wa HESLB.

Waziri pia alisisitiza waombaji mkopo kuusoma mwongozo wa uombaji mkopo kwa kuwa wasingependa kuona mwanafunzi ambaye ni mhitaji anakosa mkopo kwa sababu alikosea kuomba.

"Ninawasihi wazingatie muda uliotolewa wa kuwasilisha maombi. Vilevile, ninaomba wadau wote wanaohusika katika mchakato wa kuthibitisha taarifa na nyaraka zinazotakiwa katika maombi ya mikopo nao waendelee kutoa ushirikiano wa kutosha katika kipindi hicho cha maombi ya mikopo ya stashahada," alielekeza.

Prof. Mkenda alisema dhamira ya serikali ni kuona vijana wengi zaidi wa kitanzania wanapata elimu na ujuzi ili kushiriki katika ujenzi na maendeleo ya taifa lao.

Alisema uamuzi huo umesababisha ongezeko la bajeti ya fedha za mikopo hadi kufikia Sh. bilioni 731 mwaka huu na ongezeko la idadi ya wanufaika.

Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, alisema kuwa baada ya kuzinduliwa mwongozo huo, watajitahidi kutoa elimu kwa waombaji kupitia vyombo vya habari ili watimize lengo la kuomba na kunufaika na mkopo huo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya ya HESLB, Prof. Hamis Dihenga, alisema jambo hilo limekuwa linazungumzwa kwa muda mrefu na Rais Samia alishalizungumzia na imefika wakati limeanza kutekelezwa.

Alisema kazi kubwa inayotakiwa ni kutoa elimu kwa umma kujua vitu muhimu ambavyo vinatakiwa kwa waombaji ili wanufaike na mkopo huo wa stashahada.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Taila la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET), Dk. Adolf Rutayuga, aliunga mkono kutolewa mikopo hiyo. Walisubiri jambo hilo kwa muda mrefu.

Alisema wakipatiwa mikopo, itasaidia kuongeza namba ya wataalamu wanaohitajika katika kada za ajira kwa kuwa utendaji kazi unahitaji watu wenye taaluma mbalimbali.

Alisema waligundua programu hizo zinahitaji fedha nyingi katika kusoma na wengine kushindwa kusoma, hivyo serikali itasaidia kuongeza idadi ya wataalamu katika fani hizo zilizotajwa na waziri.

# Kardinali Rugambwa awataka Watanzania kudumisha amani

**Na Mwandishi Wetu,** ROME

MWADHAMA Protase Kardinali Rugambwa, amewataka Watanzania kukaa pamoja na kudumisha umoja, upendo na mshikamano ili kufanikisha maendeleo ya taifa.

Akizungumza katika mkutano wa kupongezwa baada ya kusimikwa kuwa Kardinali na Kanisa Katoliki, Rugambwa alisema matamanio yake ni kuona Watanzania wako tayari kujenga na kudumisha utamaduni wa upendo na mshikamano na watu wengine hata wale ambao si Watanzania.

"Huu ni mwito wa kuendelea kujifunza kujenga umoja na ushiriki na utume wa kanisa ili watu wote wafurahie maisha na kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa ufalme wa Mungu hapa duniani," alisema.

Kardinali Rugambwa ambaye pia ni Askofu Mkuu Mwandamizi Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Tabora, aliwashukuru waliotuma salamu za pongezi na upendo pamoja na kumtakia kheri katika maisha na utume wake tangu Baba Mtakatifu Francisco alipotangaza Makardinali wapya 21, akiwa miongoni mwao.

Rais Samia Suluhu Hassan ni miongoni mwa viongozi waliompongeza Mtanzania huyo wa tatu kutawazwa kushika nafasi hiyo. Katika salamu zake, Rais Samia alijikita kwenye kaulimbiu ya kiongozi huyo kama njia sahihi ya kuelezea namna ya utumishi wa kiroho wa kiongozi huyo wa dini

"Enendeni ulimwenguni mwote", ikiakisi mafundisho ya Yesu Kristo katika Injili ya Marko 16:15, juu ya utume unaojali watu wote, sehemu zote na wakati wote.

"Naungana na Watanzania wote kukuombea kheri, afya njema na mafanikio katika utumishi wako,"alisema Rais Samia Suluhu Hassan, akiungana na Watanzania wengi waliomtumia salamu za pongezi siku hiyo.

Balozi wa Tanzania nchini Italia, Mahmoud Thabit Kombo, aliwasilisha salamu za pongezi za Rais Samia kwa Kardinali Rugambwa na kuwataka viongozi wa kanisa kuliombea mema taifa na viongozi wake ikiwa ni njia ya kudumisha amani, umoja, mshikamano na upendo kwa wananchi wote.

"Rais Samia anaungana na Watanzania wote kumwombea Kardinali Rugambwa kheri, afya njema na mafanikio katika utumishi wake ambao unaongeza historia nzuri kimataifa kwa kuwa Mtanzania wa tatu kusimikwa katika ukardinali.

"Wakati ninamtakia kheri na baraka tele Kardinali Rugambwa katika maisha yake ya utume kama Askofu Mkuu Mwandamizi wa Jimbo Kuu la Tabora, niwaombe pia viongozi wa dini wote waliombee taifa letu ili kwa pamoja tushiriki kupiga hatua kubwa kimaendeleo," alisema Balozi Kombo.

Julai 9, mwaka huu, Baba Mtakatifu Francisko, alitangaza majina mapya ya Makardinali 21 huku watatu kati yao wakiwa ni wale waliojipambanua katika huduma kwa kanisa na watu wa Mungu kwa ujumla.



Watumishi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), wakitoa huduma ya uhakiki kwa Mstaafu Niwael Mbaga (wa pili kushoto), nyumbani kwake mjini Morogoro jana, katika kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja. PSSSF imetumia maadhimisho hayo kwa kuwafikia majumbani wastaafu wenye changamoto mbalimbali ikiwamo wale wanaokabiliwa na matatizo ya kiafya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jokate aahidi ushindi kwa Rais Samia

**Na Beatrice Shayo**

KATIBU Mkuu wa Jumuiya ya Umoja Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Jokate Mwegelo, amesema jukumu la jumuiya hiyo ni kuyasemea mafanikio aliyoyafanya Rais Dk. Samia Suluhu na kupata ushindi katika uchaguzi mkuu ujao.

Mwegelo aliyasema hayo jana wakati alipokwenda kuchukua barua yake ya kuteuliwa, ofisi za chama hicho Lumumba jijini Dar es Salaam.

Alisema wanawake ni jeshi kubwa litakalomsimamia Rais Samia abaki katika nafasi yake na kushinda kwa kishindo.

Aidha, alisisitiza wanawake kupendana kutoka moyoni kwa vitendo, kusaidiana, kusemeana kwa wema, kuinuana na kura wapigiane.

Alisema kuwa na rais mwanamke ni jambo la kujivunia na wanawake, mabinti na vijana wawe mstari wa mbele kulinda mafanikio yake.

"Rais Samia anasimama kama kielelezo cha wanawake kujikomboa, sasa kama amefika katika hicho kilele hatuna budi kumsaidia, kumsemea na kuhakikisha hiyo nafasi haiponyoki na sisi ndiyo jeshi la mama," alisema.

Alisema jeshi la wanawake litakuwa na nguvu na kasi ya kuhakikisha kwenye uchaguzi unaokuja kumwezesha Samia kushinda.

"Nawashukuru kwa kuniona ninafaa kutumikia nafasi hii nimesimama hapa kwa niaba ya wanawake wote hii nafasi ni yenu nipo hapa kwa ajili yenu sipo kama Jokate nipo kwa ajili yenu kwa hii nafasi ya Katibu Mkuu wa UWT," alisema Mwegelo.

Alisema yeye ni zao la Chama cha Mapinduzi na amesomeshwa na Jamhuri ya Muungano uwezo wake wa kusoma imetokana na sera nzuri ambazo zimemuwezesha kupata elimu.

Alisema elimu aliyoipata anakwenda kuwatumikia wananchi na yupo tayari kutoa ushirikiano kwa kila ngazi na kupokea ushauri ambao utasaidia kusogeza mbele maendeleo ya chama.

Aidha, alisema kikubwa anachokiomba ni ushirikiano. "Unaweza ukawa na nia nzuri na maono mazuri, lakini ukikosa ushirikiano ni kazi kubwa ila kwa ninyi sina mashaka, wote ni mashahidi tunao viongozi wetu wana uzoefu mzuri wanachanja mbuga kweli kweli," alisema.

Kadhalika, alisema ana imani kazi yake itakuwa ni nyepesi kwa sababu anaingia kwenye jumuiya ambayo imejipanga, imejizatiti na kujipambanua.

"Leo nimefika hapa kuchukua fomu ya uteuzi niridhie kuwa nimepokea jukumu hili ambalo nimepewa, lakini kama ilivyoelezwa kutakuwa na mapokezi rasmi ambayo yatafanyika Oktoba 12 Dodoma, nikiwa kule nitaongea kwa kirefu na nitaongea zaidi nitakapokuwa nimekabidhiwa ofisi rasmi," alisema na kuongeza;

"Nami nitakuwa na uwezo wa kuja kwenu kueleza mwelekeo wa UWT utakuwa ni upi leo nilikuwa na jukumu la kuchukua barua yangu ya uteuzi nimeshaipokea niwashukuru sana ofisi ndogo ya UWT na viongozi wangu kwa maandalizi haya mliyonifanyia inaonyesha jinsi gani mna imani kubwa na mimi.

Niwahakikishie katika watu ambao wanamfurahia Rais Samia mimi naongoza, hivyo niahidi nitawapa ushirikiano wa kila aina kuhakikisha tunasonga mbele kikubwa tuombeane kwa Mungu," alisema.

# Madereva wanaotumia majani barabarani sasa kukamatwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KIKOSI cha Usalama Barabarani cha Jeshi la Polisi kimetangaza kuanza kuwakamata na kuwachukulia hatua madereva wanaoweka majani barabarani kama alama ya tahadhari pindi gari linapoharibika badala ya kutumia alama ya pembetatu.

Kamanda wa kikosi hicho, Ramadhan Ng'anzi aliiambia Nipashe jijini hapa jana kuwa hatua hiyo inalenga kudhibiti ajali baada ya serikali kuruhusu mabasi kutembea usiku.

"Tunataka kuondoa hii tabia ya madereva wanaotumia majani barabarani kama ishara ya alama ya tahadhari badala ya triangle (alama ya pembe tatu) tutawakamata na kuwafungulia mashtaka," alionya Kamanda Ng'anzi.

Alisema uwekaji majani barabarani unachafua mazingira kwa kuwa wengi wao wanapoondoa gari barabarani wanayaacha.

"Madereva wa aina hii wamekuwa wakichangia kusababisha ajali barabarani kwa sababu gari lingine likiwa linakuja, dereva huenda asione majani yaliyowekwa kama alama ya tahadhari," alifafanua.

Alisema tayari kikosi hicho kimeshaongea na maofisa wake kuanza kuwakamata madereva wenye tabia hiyo.

Pia alionya kuwa magari yanayoharibika hayapaswi kuachwa zaidi ya saa 24 barabarani na kuanzia sasa kikosi hicho kitayatoa kwa nguvu, lakini kwa gharama za mmiliki wa chombo hicho cha moto.

"Kikosi cha Usalama Barabarani hakitavumilia hili, hivyo magari yatatolewa kwa nguvu, faini na gharama lazima wamiliki wa vyombo hivyo watalipa," alisema.

Alifafanua kuwa serikali imeruhusu magari kufanya safari za usiku, lakini ni lazima usalama wa barabarani uzingatiwe kama sheria inavyoelekeza na si kujiamulia kiholela.

Alisisitiza madereva na wamiliki wa vyombo vya moto kuzingatia maagizo hayo kwa sababu gari linapoharika linatakiwa kutolewa haraka ili kuhakikisha usalama wa magari mengine yanayotumia njia hiyo yanapita yakiwa salama.

Alitoa wito kwa madereva na wamiliki wa vyombo vya usafiri barabarani kuhakikisha wana vifaa ambavyo wanastahili kuwa navyo kama tahadhari wanapokuwa barabarani.

**"Kikosi cha Usalama Barabarani hakitavumilia hili, hivyo magari yatatolewa kwa nguvu, faini na gharama lazima wamiliki wa vyombo hivyo watalipa," alisema.**

# UN Women yawapa mafunzo maalum wanawake, wasichana

**Na Romana Mallya**

UN Women kwa kushirikiana na serikali wametoa mafunzo ya awamu ya pili ya 'Binti Digitali' kuwawezesha wanawake na wasichana kupata ujuzi wa Habari, Mawasilino na Teknolojia (ICT).

Mafunzo hayo yametolewa kwa wasichana wenye umri wa miaka 17 hadi 25 kwa lengo la kuwafanya kuwa wabunifu na watengenezaji programu za kompyuta na kuwa na taaluma katika sekta ya ICT, elimu na sekta ya usimbaji na kujiajiri na kutatua changamoto mbalimbali ndani ya jamii.

Kambi ya kwanza ya mafunzo ya ujuzi kidijitali ilifanyika visiwani Zanzibar na kuhusisha wanawake na wasichana 63 na ya pili ya jijini Dar es Salaam imewanufaisha washiriki wengine 50 na kufanya jumla ya wanufaika kufikia 113.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omari Kipanga, akizungumza hivi karibuni wakati akifunga kambi hiyo, alieleza hatua zilizopigwa katika kuendeleza usawa wa kijinsia na kuimarisha juhudi za nchi katika kufikia lengo la tano la Maendeleo Endelevu, ambalo linalenga kufikia usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake na wasichana wote.

Binti Dijitali inatekelezwa chini ya mradi ujulikanao 'African Girls Can Code Initiative (AGCCI)', ili kuwanufaisha wasichana wadogo wachangie katika teknolojia na ubunifu nchini na barani Afrika.

Mradi huo unatekelezwa na UN Women kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum pamoja na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Kipanga alisema Tanzania imeanzisha mfumo imara wa sheria unaohakikisha usawa wa kijinsia na mabinti kutobaguliwa katika upatikanaji ubunifu na teknolojia za kidijitali.

Alisema jitihada hizo zimesababisha kuwapo ongezeko kubwa la uandikishaji wa wasichana shuleni katika miaka ya hivi karibuni, jambo ambalo ni muhimu katika kufikia usawa wa kijinsia na kuwawezesha kufikia lengo.

Alisema katika mwaka wa masomo wa 2021/22, uandikishaji wa wasichana uliongezeka hadi asilimia 44, na kati ya wanafunzi 510 waliohitimu masomo ya uhandisi mwaka huo, asilimia 57 lilikuwa ni kundi hilo.

Kuhusu kambi ya pili ya Binti Digitali, kiongozi huyo alisema itahamasisha na kuwawezesha wasichana wadogo kufuata taaluma katika teknolojia na sayansi ya kompyuta, hasa katika muktadha wa mapinduzi ya nne ya viwanda.

Alikumbusha kuwa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025 inatarajiwa kujenga uchumi imara na wenye ushindani unaolenga kukuza sayansi na teknolojia kupitia elimu bora, ikiwa ni pamoja na sayansi ya msingi na Hisabati.

Alisema Tanzania imeanzisha mfumo imara wa sheria unaohakikisha usawa wa kijinsia na kutobagua upatikanaji wa ubunifu, teknolojia na teknolojia za kidijitali.

"Wanafunzi wa elimu ya juu wanaosoma sayansi na teknolojia wanafanya mambo makubwa katika jamii zao kama vile msichana kutoka Zanzibar ambaye alikuwa mwanafunzi wa kwanza Afrika Mashariki kurusha ndege zisizo na rubani," alisema.

Alibainisha kuwa mfano huo ni ushahidi wa mafanikio ambayo wanawake wanaweza kufikia wakati kuna mazingira ya kuunga mkono katika nyanja za STEM, kama vile kukuza usawa wa kijinsia katika elimu na mahali pa kazi, kutoa ushauri na mifano ya kuigwa na kuongeza upatikanaji teknolojia na rasilimali.

Mwakilishi wa UN Women, Mitra Sadanada, alisema kwa kutumia programu kama hiyo, wanaweza kushirikiana kuhakikisha wasichana wanakuwa na zana na ujasiri wa kuleta mabadiliko katika nchi.

Balozi wa Ubelgiji nchini, Petra Heylen, alisema Ubelgiji inajivunia kuunga mkono mpango huo wa kikanda unaotekelezwa kwa pamoja na UN Women, Tume ya Umoja wa Afrika na Umoja wa Kimataifa wa Mawasiliano.

"Usawa wa kijinsia na haki za binadamu za wanawake na wasichana ni vipaumbele vya muda mrefu vya Ubelgiji.

Mhitimu Annagrace Malamsha kutoka Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili (MUHAS) alisema kupitia kambi hiyo wametengeneza blogu inayoitwa 'Binti Kazi' ambayo inakwenda kutatua matatizo likiwamo la ajira kwa kuwapa ujuzi wahitimu ili nafasi zinapotoka waweze kuzipata.

Binti Dijitali inafadhiliwa na nchi ya Ubelgiji kuhakikisha wasichana wa Kiafrika wanafaidika na kuchangia mapinduzi ya kiteknolojia barani Afrika.

## Serikali yatoa mwongozo uuzaji wa parachichi

**Na Mwandishi Wetu**

ILI kulinda ubora wa soko la parachichi ndani na nje ya nchi, Wizara ya Kilimo imeandaa Mwongozo wa Uendelezaji wa Tasnia ya zao hilo ambao pamoja na mambo mengine, unaelekeza utaratibu wa ununuzi na uuzaji wake.

"Kwa mujibu wa taarifa ya Kitengo cha Mawasiliano Serikalini cha wizara hiyo iliyotolewa jana, mnunuzi wa parachichi anapaswa kuomba kibali cha kununua zao hilo wizarani kwa kuainisha eneo la uzalishaji atakalonunua.

"Atapaswa kuambatanisha nyaraka zote muhimu zikiwamo usajili wa kampuni au cheti cha kuandikishwa kwa mfanyabiashara binafsi, utambulisho wa namba ya mlipaKodi na leseni ya biashara," ilibainishwa katika taarifa hiyo.

Taarifa hiyo pia ilibainisha kuwa wizara itatoa vibali kwa wanunuzi wa parachichi na kuwatambulisha wanunuzi hao katika ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa ajili ya kupata leseni zinazohusika na ununuzi wa parachichi.

Pia ilibainisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika eneo husika la uzalishaji wa zao hilo, zitatoa kibali cha kuvuna na kusafirisha kwa mnunuzi mwenye kibali cha ununuzi kilichotolewa na wizara.

Taarifa hiyo ilisema wizara kupitia Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) itatangaza kufungua au kufunga msimu wa ununuzi kwa kuzingatia viwango vya ukomavu wa tunda.

"Mamlaka za Serikali za Mitaa zitasimamia malipo ya wakulima kulingana na makubaliano yaliyofikiwa baina ya wakulima na wanunuzi wa parachichi walioidhinishwa," ilisema.

Kadhalika, wasafirishaji wa parachichi kwenda nje ya nchi wanapaswa kuzingatia viwango vya ubora vinavyohitajika katika soko husika ikiwa ni pamoja na aina ya vifungashio na nyaraka za afya ya mimea.

Taarifa hiyo ilisisitiza kuwa mawasiliano kwa ajili ya ufafanuzi wowote unaoweza kuhitajika ufanyike kupitia Kituo cha Huduma kwa Wateja kwa namba ya simu 0733 800 200.


## Canara Bank (Tanzania) Ltd.

(Together we can build a better life)

### PUBLICATION OF INTEREST RATES, FEES AND CHARGES (REVISED W.E.F 01.11.2023)

**PURSUANT TO REGULATION 11 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS DISCLOSURE REGULATION, 2014 AND REGULATION 40(3)(a) OF THE FINANCIAL CONSUMER**

| S/N | DESCRIPTION | | EXISTING CHARGES TZS | EXISTING CHARGES USD | PROPOSED CHARGES TZS | PROPOSED CHARGES USD |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | **Monthly Maintanance** | SA | Free | Free | 2,000.00 | 2 |
| | | CA | Free | Free | 6,000.00 | 4 |
| 2 | **Non Maintanance of Minimum Balance** | SA | Free | Free | 1,500.00 | 2 |
| | | CA | Free | Free | 4,000.00 | 4 |
| 3 | **Account Statement Charges** | SA-Monthly | Free | Free | - | 0 |
| | | SA-Interim | 4,300.00 Plus TZS 500 per page | 5 Plus $1 per page | 1,500.00 per page | 1.5 per page |
| | | CA-Monthly | Free | Free | Free | Free |
| | | CA-Interim | 4,300.00 Plus TZS 500 per page | 5 Plus $1 per page | 1,500.00 per page | 1.5 per page |
| 4 | **Cash withdrawal** | SA-Up 25M | Free | | Free | |
| | | SA-Over 25M | Free | | 0.26% | |
| | | SA-Up to $2K | | Free | | Free |
| | | SA-$2K-$5K | | Free | | 0.60% |
| | | SA-Over $5k | | 0.26% | | 0.60% |
| | | CA-Up to 25 M | Free | | Free | |
| | | CA-Above 25M | 0.11% | | 0.26% | |
| | | CA-Up to USD 5K | | Free | | Free |
| | | CA-$ 5K-$10K | | 0.26% | | 0.60% |
| | | CA-Above $ 10K | | 0.43% | | 0.60% |
| 5 | **Cash Deposit Charges** | SA-Up to 25M | Free | | Free | |
| | | SA-Over 25M | Free | | 0.22% | |
| | | SA-Up $5K | | Free | | Free |
| | | SA-Over $5K | | Free | | 0.50% |
| | | SA-small currency ($1 to $20) | | Free | | 10.00% Minimum charge $1 |
| | | CA-Up to 50M | Free | | Free | |
| | | CA-Over 50M | 0.11% | | 0.22% | |
| | | CA-Up to $10K | | Free | | Free |
| | | CA-Over $10K | | 0.26% | | 0.50% |
| | | CA-small currency ($1 to $20) | | Free | | 10.00% Minimum charge $1 |
| 6 | **Balance Confirmation Certificate** | SA | 12,800.00 | 6 | 12,800.00 | 10 |
| | | CA | 21,200.00 | 13 | 21,200.00 | 13 |
| 7 | **Account Closure Charges** | SA | 12,800.00 | 13 | 20,000.00 | 20 |
| | | CA | 21,200.00 | 17 | 50,000.00 | 50 |
| 8 | **Activation of Dormant Account** | SA | 5,100.00 | 6 | Free | Free |
| | | CA | 5,100.00 | 6 | Free | Free |
| 9 | **Stop Payment Charges** | SA | N/A | N/A | Free | Free |
| | | CA | 25,500.00 | 13 | 35,000.00 | 28 |
| 10 | **Cheque Return Charges/Dishonoured Cheque** | CA-Inward | 25,500.00 | 13 | 50,000.00 | 50 |
| | | CA-Outward | 25,500.00 | 13 | 50,000.00 | 50 |
| 11 | **Cheque Clearing Charges** | CA-Inward | 1,300.00 | 1 | 1,300.00 | 1 |
| | | CA-Outward | Free | Free | Free | Free |
| 12 | **Ledger folio charges per folio (40lines per** | SA | N/A | N/A | Free | Free |
| | | CA | N/A | N/A | 6,000.00 | 4.00 |
| 13 | **Cheque book Charges** | CA-50 Leaves | N/A | N/A | 42,000.00 | 27 |
| 14 | **Mobile Banking** | | | | | |
| i | Withdrawal Charge | Upto 100,000 | 1,700.00 | N/A | 1,700.00 | N/A |
| | | 101,000 to 200,000 | 2,600.00 | N/A | 2,600.00 | N/A |
| | | 201,000 to 400,000 | 4,300.00 | N/A | 4,300.00 | N/A |
| | | 401,000 to 600,000 | 5,100.00 | N/A | 5,100.00 | N/A |
| | | 601,000 to 999,000 | 6,800.00 | N/A | 6,800.00 | N/A |
| ii | Funds Transfer/Mobile Wallet | Upto 100,000 | 500.00 | N/A | 500.00 | N/A |
| | | 101,000 to 250,000 | 900.00 | N/A | 900.00 | N/A |
| | | 251,000 to 500,000 | 1,700.00 | N/A | 1,700.00 | N/A |
| | | 501,000 to 1,000,000 | 4,300.00 | N/A | 4,300.00 | N/A |
| | | 1,001,000 TO 10 Mn | 8,500.00 | N/A | 8,500.00 | N/A |
| 15 | **Locker Rent-Yearly** | Small | 296,700.00 | N/A | 296,700.00 | N/A |
| | | Medium | 508,500.00 | N/A | 508,500.00 | N/A |
| | | Big | 635,600.00 | N/A | 635,600.00 | N/A |
| 16 | **Remittances** | | | | | |
| i | TISS | Any amount per 1 | TZS 8,450.00 | TZS 8,450.00 Equivallent | TZS 8,450.00 | TZS 8,450.00 Equivallent |
| ii | E Remittances | Upto USD 1000 or Eq. TZS | 17,000.00 | $ 9.00 | 17,000.00 | $ 9.00 |
| | | 1001 to 5000 | 20,400.00 | $ 11.00 | 20,400.00 | $ 11.00 |
| | | 5001 to 10000 | 40,700.00 | $ 22.00 | 40,700.00 | $ 22.00 |
| | | 10,001 and above | 84,800.00 | $ 43.00 | 84,800.00 | $ 43.00 |
| iii | Swift Outward | Upto 5,000 | NA | $ 39.00 | NA | $ 39.00 |
| | | 5,001 to 10,000 | NA | $ 51.00 | NA | $ 51.00 |
| | | above 10,000 | NA | $ 77.00 | NA | $ 77.00 |
| iv | Swift Inward | Upto 5,000 | NA | $ 11.00 | NA | $ 11.00 |
| | | 5,001 to 10,000 | NA | $ 16.00 | NA | $ 16.00 |
| | | above 10,000 | NA | $ 26.00 | NA | $ 26.00 |

| | | |
|---|---|---|
| HEAD TREASURY AND TRADE | SIGNED | 03-Dey-23 |
| GM-CREDIT | SIGNED | 03-Dey-23 |
| DEPUTY CEO | SIGNED | 03-Dey-23 |

| S/N | DESCRIPTION | | EXISTING CHARGES TZS | EXISTING CHARGES USD | PROPOSED CHARGES TZS | PROPOSED CHARGES USD |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 17 | **Loan/Advances Related Charges** | | | | | |
| i | Processing Charges | Upto 5 Mio - | 21,200.00 | | 21,200.00 | |
| | | 5Mio to 10 Mio - | 169,500.00 | | 169,500.00 | |
| | | 10 Mio to 25mio - | 339,000.00 | | 339,000.00 | |
| | | 25 mn to 500 mio - | 1.28% | | 1.28% | |
| | | >500mio--* (*minimum 7.5mio) | 1.06% | | 1.06% | |
| | | Upto 5,000 - | | $85.00 | | $85.00 |
| | | 5000 to 10,000 - | | $170.00 | | $170.00 |
| | | Upto 20,000 - | | $255.00 | | $255.00 |
| | | 20,000 to 500,000 - | | 1.28% | | 1.28% |
| | | >500,000--* | | 1.06% | | 1.06% |
| ii | Documentation Charges | Upto 100 MILLION | FREE | | FREE | |
| | | >100 Mio (-Min 300,000) | 0.26% | | 0.26% | |
| | | Upto 50,000 | | FREE | | FREE |
| | | >50,000 - (Min 150) | | 0.26% | | 0.26% |
| iii | Upfront fee on Term Loan | Upto 5Mio - | 21,200.00 | | 21,200.00 | |
| | | 5 Mio to 10 Mio - | 169,500.00 | | 169,500.00 | |
| | | 10Mio 25mio - | 381,400.00 | | 381,400.00 | |
| | | 25 mn to 500 mio - | 1.53% | | 1.53% | |
| | | >500mio--* (*minimum 9mio) | 1.28% | | 1.28% | |
| | | Upto 20,000 - | | $255.00 | | $255.00 |
| | | 20,000 to 500,000 - | | 1.53% | | 1.53% |
| | | >500,000--* (*minimum 9000) | | 1.28% | | 1.28% |
| iv | Inspection Charges | Upto 100 Mio - | 21,200.00 | | 21,200.00 | |
| | | >100 mio - | 42,400.00 | | 42,400.00 | |
| | | Upto 50,000 | | $22.00 | | $22.00 |
| | | >50,000 | | $43.00 | | $43.00 |
| v | Credit Reference Report Charges | | 101,700.00 | $43.00 | 101,700.00 | $43.00 |
| vi | Pre-payment penalty | Calculated as %ge pre-paid amount in the case of takeover of liability by other bank/lenders | 2.00% | 2.00% | 2.00% | 2.00% |
| 18 | **Guarantees (Local & International)** | | | | | |
| i | Bonds & Guarantees | per quarter (Min TZS 75,000) | 1.02% | 1.02% | 1.02% | 1.02% |
| ii | Bonds & Guarantees with 100 % Cash Margin | per quarter (Min TZS 75,000) | 0.43% | 0.43% | 0.43% | 0.43% |
| 19 | **Letter of Credit** | | | | | |
| 19.1 | **Import Letter of Credit (per qrtr of Part thereof)** | | | | | |
| i | Opening commission | commission Min $ 200 | NA | | NA | |
| ii | LC amendment Commission | Commision Min $50 max 350 | NA | 1.02% | NA | 1.02% |
| iii | Swift charge for LC opening | | NA | 0.34% | NA | 0.34% |
| iv | Swift charge for other message/amendments | | NA | $34.00 | NA | $34.00 |
| v | Extensions - Commissions | commission Min $ 200 | NA | $34.00 | NA | $34.00 |
| vi | LC cancellation charges | commission Min $ 200 | NA | 1.02% | NA | 1.02% |
| vii | Non payment of Bills on due date | Till Payment | NA | 1.02% | NA | 1.02% |
| 19.2 | **Export Letters of Credit (per quarter or part thereof)** | | | | | |
| i | Advising commission | | NA | $119.00 | NA | $119.00 |
| ii | Confirmation Commission | Commision Min $150 | NA | 0.43% | NA | 0.43% |
| iii | Negotiating bills under LC | Commision Min $75+cuourier+interest | NA | 0.43% | NA | 0.43% |
| iv | Reimbursement claim paid | Commision Min $75 | NA | 0.43% | NA | 0.43% |
| v | Extensions - | Commision Min $200 | NA | 1.02% | NA | 1.02% |
| vi | Collection of Export LC | Commision Min $75+cuourier+interest | NA | 0.43% | NA | 0.43% |
| vii | Amendments | | NA | $64.00 | NA | $64.00 |
| 20 | **Other disclosures** | | | | | |
| i | Base or Prime Lending Rate | | 16% | 7% | 16% | 10% |
| ii | Maximum spread | | 5% | 5% | 5% | 5% |
| iii | Penal Interest | | | | | |
| | a.For non compliance on Terms of Saction | Rate per year over regular rate of interest | 3% | 3% | 3% | 3% |
| | b.For Overdrawing/Excess drawing due to non payment of interest/installment/charges | Rate per year over regular rate of interest | 5% | 5% | 5% | 5% |
| vi | Deposit Rates | | | | | |
| | a. Current account | | Nill | Nill | Nill | Nill |
| | b. Savings bank deposit | | 3.00% | 1.00% | 3.00% | 1.00% |
| | C. Fixed Deposits Rates | **Up to TZS 50 M(up to USD 50,000)** | | | | |
| | | 30 -90days | 3.50% | 1.50% | 3.50% | 1.50% |
| | | 91-180days | 4.50% | 2.25% | 4.50% | 2.25% |
| | | 181-364 days | 5.50% | 3.00% | 5.50% | 3.00% |
| | | 1 year and above | 8.00% | 3.75% | 8.00% | 3.75% |
| | | 2 Years and Above | 8.00% | 4.00% | 8.00% | 4.00% |
| | | **TZS 50 M-100M (USD 50,000 -USD 100,000)** | | | | |
| | | 30 -90days | 4.50% | 2.25% | 4.50% | 2.25% |
| | | 91-180days | 5.50% | 2.50% | 5.50% | 2.50% |
| | | 181-364 days | 7.00% | 3.50% | 7.00% | 3.50% |
| | | 1 year and above | 8.25% | 4.25% | 8.25% | 4.25% |
| | | 2 Years and Above | 9.00% | 4.75% | 9.00% | 4.75% |
| | | **Above 100 M(Above USD 100,000)** | | | | |
| | | 30 -90days | 5.50% | 2.50% | 5.50% | 2.50% |
| | | 91-180days | 6.50% | 3.25% | 6.50% | 3.25% |
| | | 181-364 days | 7.50% | 4.00% | 7.50% | 4.00% |
| | | 1 year and above | 8.50% | 4.75% | 8.50% | 4.75% |
| | | 2 Years and Above | 9.50% | 5.00% | 9.50% | 5.00% |

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maagizo ya Makamu wa Rais yawe dira ya utendaji ATCL

**SHIRIKA** la Ndege la Tanzania (ATCL) juzi lilipokea ndege mpya aina ya Boeing 737- Max 9 hivyo kufanya kuwa na ndege 13 hadi sasa. Ujio wa ndege hiyo ni mpango mahususi wa serikali katika kuimarisha usafiri wa ndani na kuwa na shirika linalotambulisha nchi katika tasnia ya usafiri wa anga.

Kuwasili kwa ndege hiyo kunaongeza uwezo wa shirika katika kuboresha huduma zake pamoja na kuwafanya Watanzania na watu wa mataifa mengine kuwa na uhakika wa usafiri wawapo ndani ya nchi kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Pia kuwapo kwa ndege nyingi kunalifanya shirika kuwa na uwezo wa kujiendesha kwa maana kutoa huduma za viwango na za uhakika.

Kwenye hafla ya upokeaji wa ndege hiyo, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alikuwa mgeni rasmi na katika hotuba yake, alitoa maagizo kwa Wizara ya Uchukuzi ambayo ndiyo yenye dhamana ya kuisimamia taasisi hiyo pamoja na shirika lenyewe.

Moja ya maagizo hayo na pengine kubwa kuliko yote, ni kumaliza malalamiko ya abiria yanayotokana na kuahirishwa kwa safari au kusogezwa kwa muda wa safari huku akibainisha wazi kwamba tatizo hilo limekuwa sugu katika Uwanja wa Ndege wa Mwanza. Agizo lingine ni wizara na ATCL, kuangalia upya gharama za usafirishaji mizigo ambazo zimelalamikiwa kuwa ni kubwa na hatimaye kupeleka mapendekezo serikalini.

Sambamba na hayo, Dk. Mpango alisema serikali imedhamiria kuwekeza katika sekta ya uchukuzi na kuongeza biashara, hivyo imeazimia kwamba itaingiza ndege zingine mbili ifikapo Machi, mwakani. Kutokana na hali hiyo, aliagiza wizara na ATCL kuwa na utaratibu na usimamizi mzuri wa huduma za usafiri wa anga ikiwamo kuimarisha huduma ili kuwa na ushindani wa kikanda na kimataifa hatimaye shirika hilo kutoa mchango chanya katika pato la taifa.

Maagizo yaliyotolewa na Makamu wa Rais, yawe kama mwito wa kuiamsha ATCL katika kutekeleza majukumu yake kwa viwango vya juu ikiwamo kutoa huduma zenye sura ya kimataifa ilhali kwa kiasi kikubwa wateja wake wakiwa Watanzania kwa usafiri wa ndani.

Kama alivyosema Dk. Mpango, kumekuwa na kero kubwa ambazo zimefanya utendaji wa ATCL kuwa na walakini hasa katika usafirishaji wa abiria na mizigo. Kero kubwa ni ya uchelewaji wa safari unaotokana na kuahirishwa au kusogezwa mbele, ambayo imesababisha malalamiko na kuibua maswali mengi yasiyo na majibu. Moja ya maswali hayo ni wasiwasi kama uongozi wa shirika una uwezo wa kusimamia taasisi na kutekeleza majukumu yake kwa viwango vya kimataifa kama inavyotakiwa.


Kauli ya Dk. Mpango inadhihirisha kwamba kuna kasoro katika utendaji kazi ndani ya shirika ambao unatia doa nia thabiti ya serikali katika kuimarisha usafiri wa anga. Inakuwaje ndege 12 ziwapo, tena zenye uwezo mkubwa, zishindwe kukidhi kiu ya wadau wa usafiri wa anga na kuleta tija ndani ya shirika?

Kwa jumla, suala la kuahirishwa kwa safari au kusogezwa mbele kwa muda fulani ni jambo la kawaida ndani ya ATCL. Mtu anaweza kufika uwanja wa ndege na kufanya taratibu zote zinazotakiwa kwa ajili ya safari ikiwamo kuingia kwenye eneo maalum la kusubiri kupandia ndege, lakini muda ukikaribia linatolewa tangazo kwamba safari imesogezwa kwa muda fulani.

Jambo hili ni kero kubwa kwa abiria ambao wengi wao ni wafanyabiashara na wakati wanapanga safari zao na kuamua kutumia usafiri wa anga, wanakuwa na imani kwamba watafika kwa wakati na kufanya mambo yao kwa mujbu wa ratiba. Lakini inapofikia hatua ya kuahirishwa au kusogezwa mbele, inasababisha usumbufu mkubwa hata mipangilio ya shughuli zao kuharibika.

Ni vyema sasa bodi na menejimenti ya ATCL pamoja na wizara zikayachukulia maagizo ya serikali kupitia kwa Makamu wa Rais kama dira ya kufanya mabadiliko na kuboresha usafiri wa anga.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Zuwena Khatib

# Kilimo cha kiikolojia kwa wakulima wadogo, kina majibu yao ya uhakika

**INAJULIKANA** kilimo cha kiikolojia cha wakulima wadogo, kina manufaa ya kufanikisha haki za mazingira ya wakulima kwa sehemu nyingi duniani.

Mahali hapo wanapambana na mabadiliko ya tabianchi na mfumo wa uzalishaji unaosababisha janga hilo, ambao unatakiwa kuthibitiwa na ule wa uzalishaji chakula.

Vuguvugu la kilimo cha kiikolojia cha wakulima wadogo na lile la uhuru wa chakula, vyote vinalenga kukabiliana na nguvu za ushawishi za kampuni kubwa, zinazohodhi rasilimali za kilimo kama vile mbegu, mbolea, ardhi na maji.

Hapo inapaswa, msingi wa uzalishaji wa chakula kuwa wa watu na sio mashirika makubwa ya kimataifa.

Kwa kuwa watu, ndio wanaojua thamani ya ardhi yao, wanaitumiaje, ubunifu na kupeana maarifa hayo wenyewe.

Hao ni wakulima wadogo wenye uwezo wa kuilisha dunia nzima, kutuliza mabadiliko ya tabianchi ni walaji wanaostahili kupata chakula chenye lishe bora na chenye afya na kinachoendana na utamaduni wao.

Kwa kujali masuala yanayohusu utamaduni wa chakula unaothamini watu wote dunia nzima, kilimo cha kiikolojia cha wakulima wadogo ni jambo la kwanza na ni hatua muhimu kabisa ya kupigania haki za mazingira.

Kilimo hicho cha kiikolojia kinawaweka huru wazalishaji na walaji dhidi ya mfumo wa uzalishaji, unaohatarisha tabianchi na kumnyima nyenzo zao za kukabiliana na tatizo hilo. Njia za kilimo cha mapinduzi ya kijani, huwalazimisha wakulima kuchukua mikopo mikubwa na kuzalisha chakula kwa ajili ya kuuza nje na uzalishaji huo hauwi rafiki kwa mazingira.

Kwa ajili ya kupambana na hali hiyo, wanachama wa ngazi za chini wastahili kupigania haki za mazingira.

Kampuni zinazofanya biashara ya kilimo, nazo zinahimiza matumizi ya kiwango kikubwa cha nishati, kwa ajili ya kupata mazao mengi ya kukidhi mahitaji ya soko la kimataifa bila ya kujali madhara yanayotokea kwenye udongo na madhara kwa dunia.

Huwa wanahimiza kutumia suluhisho potofu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kwa kufanya hivyo, wanapuuza, kukandamiza na hata kupoteza maarifa ya asili ambayo ni muhimu sana katika mapambano dhidi ya haki za mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwenye maeneo husika na yanaendelea kujitokeza.

Ni maarifa hayo ya asili na sio kusisitiza matumizi ya maarifa ya kutoka mbali yanayopatikana kwenye mikutano pekee.

Maarifa hayo ya asili yanapaswa yapewe nafasi na kuhimizwa kutumika kupambana na hali ya tabianchi, kadri athari za mabadiliko ya tabianchi zinavyoongezeka na kuwa na madhara makubwa zaidi.

Biashara na kilimo zinasisitiza ubinafsishaji na kilimo cha mashamba makubwa ya mazao ya biashara.

Kilimo cha kiikolojia cha wakulima wadogo, chenyewe hupambana na haya yote, yaani kupanda mazao mbalimbali yanayoendana na mazingira husika na kusimamia kwa nguvu zote za haki za kijadi na matumizi ya umiliki wa ardhi.

Kwa njia ya sheria za haki miliki, ambazo zinakubaliwa na serikali kwenye majadiliano ya kibiashara, mashirika yanayojihusisha na biashara ya kilimo yanajaribu kuangamiza kabisa mfumo wa kupeana mbegu na mifumo ya wakulima wadogo na badala yake wanaweka mifumo ambapo wakulima watakuwa tegemezi kwenye bidhaa zinazouzwa na makampuni haya.

Kilimo cha kiikolojia cha wakulima wadogo kinahimiza matumizi ya njia hizo za asili, kama vile kubadilishana mbegu, matumizi ya nishati kwa kiwango kidogo na uhifadhi wa rutuba kwenye mashamba wakati wa kilimo, mambo yanayowasaidia wakulima kujaribisha mazao yanayohimili ukame na kuimarisha udongo.

Kilimo cha kiikolojia cha wakulima wadogo kinahitaji sera za serikali zisizozuia njia za asili za uzalishaji na ili kufanikiwa katika hilo kunahitajika mapambano.

Mapambano haya ni kwa ajili ya haki za mazingira. Maamuzi kuhusu namna serikali za mitaa zinasimamiwa na nani azisimamie, lazima yafanyike ili kupambana na mabadiliko ya tabianchi na kuulisha ulimwengu.

Nahimiza kwa kurudia kuwa kilimo cha kiilolojia cha wakulima wadogo si siasa, na ni maisha yanayotakiwa kupiganiwa.

HABARI KITAIFA

## Madaraja ya mawe yawa neema Kigoma

**Na Neema Emmanuel,** KIGOMA

WANANCHI Kigoma wamenufaika na ujenzi wa madaraja kwa kutumia teknolojia ya mawe iliyoonesha ufanisi katika ubora na urahisi wa kufungua barabara vijijini kutokana na gharama za ujenzi wake kuwa nafuu.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Barabara, Octavian Mshiu, alisema jana mjini hapa kuwa bodi hiyo imeamua kutembelea madaraja hayo yanayojengwa kwa teknolojia mbadala ya kutumia mawe ili kuona namna ya kusaidia kuisambaza teknolojia hiyo itumike kwa wingi zaidi nchini na hivyo kuipunguzia serikali gharama za ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya madaraja.

Alisema Mkoa wa Kigoma kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), umejenga jumla ya madaraja 110 kwa gharama ya Sh. bilioni 2.4, kiasi alichokitaja ni nafuu zaidi kwa kuwa yangejengwa kwa nondo na saruji, gharama ingekuwa zaidi ya Sh. bilioni 11, hivyo madaraja hayo 110 yameokoa zaidi ya asilimia 80 ya gharama ambazo zingetumika.

Alisema madaraja haya pia yametoa ajira kwa wakazi wa Mkoa wa Kigoma, zaidi ya ajira 500 zilitolewa kwa wazawa ili kutekeleza ujenzi huo.

Alifafanua ujenzi wa madaraja ya mawe unatoa ajira kwa mtu yeyote bila kujali kiwango cha elimu alichonacho.

Akizungumza kwa niaba ya wakazi wa Kwitanga, Zuwena Kwilelula aliiomba serikali kukamilisha haraka ujenzi wa Daraja la Nyamihanga ili wanufaike na huduma za kijamii upande wa Muzeze ambako kuna zahanati na mashamba ya maharage. Pia wasafirishe mazao yao kutoka Muzeze kwenda Kwitanga.

Mhandisi Felician Kavishe kutoka TARURA Mkoa wa Kigoma alisema wakala huo umejenga jumla ya madaraja 110 katika mkoa huo ambapo madaraja 35 yako Wilaya ya Kigoma, 20 Kasulu, sita Buhigwe, 15 Uvinza, 19 Kibondo na 15 Kakonko.

Wajumbe wa Bodi ya Mfuko wa Barabara wako mkoani Kigoma kujionea teknolojia mbadala kwenye ujenzi wa miundombinu ya barabara na madaraja inavyoweza kuipunguzia serikali gharama za ujenzi na matengenezo ya barabara nchini.

# Jela miaka 10 kwa kuua mtalaka

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita, imemhukumu mkazi wa Nyarugusu, Petro Mhoja (31) kutumikia kifungo cha miaka 10 gerezani kwa kosa la kumuua bila kukusudia mtalaka wake Asha Karujinda (22) kwa kumpiga mateke kifuani na tumboni.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Ntemi Kilekamajenga, baada ya mshtakiwa huyo kukiri kosa la kumuua bila kukusudia mtalaka wake huyo.

Jaji Mfawidhi Kilekamajenga baada ya mshtakiwa amekiri kosa mwenyewe bila ya kulazimishwa, alimtaka Wakili wa Serikali Theresia Mtao amsomee mshtakiwa huyo maelezo ya awali.

Akisoma maelezo ya awali, Wakili wa Serikali Theresia alidai kuwa Asha Karujinda alikuwa mke wa mshtakiwa Petro Mhoja, lakini walikuwa wametengana. Asha alikuwa anaishi kwa dada yake katika Kijiji cha Ilaluka wilayani Geita.

Wakili huyo alidai kuwa Julai 7, 2022, saa 12 jioni, Asha akiwa nyumbani kwa dada yake, mshtakiwa alikwenda huko akiwa amelewa na kuomba kuongea na mtalaka wake.

Alisema mtalaka wake alitoka nje akiwa amebeba mtoto ndipo mshtakiwa akamwambia wapange chumba ili waishi pamoja, mtalaka alikataa na kumwambia 'sitaki kurudiana na wewe'.

Alidai kuwa mshtakiwa akamwambia 'kama hautaki tuishi wote, basi nipe mtoto wangu'. Mtalaka alikataa kumpa mtoto mshtakiwa, ndipo wakaanza kunyang'anyana mtoto.

"Baada ya mshtakiwa kushindwa kumchukua mtoto, alimpiga mtalaka wake mateke kifuani na tumboni na kuanguka chini na wasamalia wema walimchukua na kumpeleka Kituo cha Polisi Nyarugusu na kupewa PF3 (Fomu Na. 3 ya Polisi) kisha wakampeleka Hospitali ya Waja na walipofika huko alifariki dunia," alidai.

Wakili huyo alidai kuwa mwili wa Asha Karujinda ulifanyiwa uchunguzi na daktari alibaini chanzo cha kifo cha marehemu ni kupasuka tumbo la chakula na damu kuvilia ndani.

Wakili huyo alidai mshtakiwa alikamatwa na alipohojiwa alikiri kosa lake la kumuua bila kukusudia mtalaka wake huyo na upelelezi ulipokamilika alifikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

Baada ya Wakili wa Serikali Mtao kumaliza kumsomea mshtakiwa maelezo ya awali, Jaji Mfawidhi Kilekamajenga alisema mshtakiwa anatiwa hatiani na mahakama hiyo kwa kosa la kuua bila kukusudia na akampatia nafasi ya kujitetee ili kupunguziwa adhabu.

Wakili wa Kujitegemea, Doreen Narzis ambaye alikuwa anamtetea mshtakiwa huyo, alidai mahakamani huko kuwa hilo ni kosa la kwanza kwa mteja wake, pia amejutia kosa lake, alikuwa anampenda mke wake ndiyo maana alikwenda kumwomba waishi wote.

Alidai kuwa mshtakiwa ana watoto wawili pamoja na mtoto wa marehemu mwenye umri wa miaka sita, wote wanamtegemea. Akaomba mahakama ipunguze adhabu kwa mteja wake.

Upande wa Mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali Theresia, ulidai hauna kumbukumbu ya makosa ya nyuma ya mshtakiwa. Ukaomba mahakama itowe adhabu kwa mjibu wa sheria.

Jaji Mfawidhi Kilekamajenga alisema mshtakiwa ulikuwa umeashaachana na mkewe na alikuwa anaishi kwa dada yake.

"Wewe unakwenda kumuua. Sasa hii kesi itakugharimu. Kama ulikuwa haumtaki ungemwacha kuliko kumuua. Marehemu hakuwa na hatia yoyote. Wewe ulikuwa umelewa ukaenda kumuua.

"Pia matukio ya wanawake kuuliwa yamekuwa mengi sana. Ili iwe fundisho kwako na watu wengine, mshtakiwa utakwenda jela kutumikia kifungo cha miaka 10," Jaji alitoa adhabu.

Baada ya Jaji Mfawidhi Kilekamajenga kumaliza kusoma hukumu na kutoka mahakamani, mshtakiwa aliangua kilio, akilalama "sikujua kama nitafungwa na kuwaacha watoto wangu watatu".




Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na Binafsi wa Benki ya NBC, Elibariki Masuke (kushoto), akizungumza na wafanyakazi, mawakala wakubwa na wadogo, wakati viongozi na wafanyakazi wa benki hiyo, walipotembelea wakala mkuu wa benki hiyo eneo la Goba, Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya mwezi wa huduma kwa wateja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kiongozi wa Mbio za Mwenge aridhishwa utunzaji mazingira

**Na Robert Hokororo**

KIONGOZI wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka huu, Abdallah Shaibu Kaim, amesema ameridhishwa na utunzaji wa uhifadhi wa mazingira unaotekelezwa na wananchi katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema hayo jana wakati akipandaji mti na kukagua miradi ya maendeleo katika Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP) ambako jumla ya miti 146 imepandwa. Kati yake, aina ya miashoki ni 129 na 15 aina ya jakalanda.

"Mwenge wa Uhuru mwaka huu una lengo la kuelimisha na kuhamasisha Watanzania juu ya athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi ambazo kimsingi asilimia 95 zinasababishwa na shughuli na matendo ya kibinadamu katika maisha yetu ya kila siku.

"Moja ya shughuli hizo ni ukataji miti kiholela, hivyo tuepuke kufanya hivyo, bali tushirikiane katika upandaji miti. Mambo mengine yasiyofaa ni uchomaji moto misitu, kilimo na ufugaji karibu na vyanzo vya maji. Ninaomba tufanye shughuli zetu umbali wa mita 60 kutoka vyanzo vya maji," aliagiza Kaim.

Kiongozi huyo aliongeza kuwa utupaji taka kiholela, uchimbaji madini usiozingatia uhifadhi wa mazingira ikiwa ni pamoja na ufugaji wa kuhamahama nao uchangia kwa kiasi kikubwa katika uharibifu wa mazingira.

Alibainisha kuwa athari mojawapo ya mabadiliko ya tabianchi zinazotokana na uharibifu wa mazingira ni ukame, mafuriko, ardhi kupoteza rutuba, kukosa mvua na kuongezeka joto sambamba na mabadiliko ya msimu wa mvua na mwisho kukosa chakula na kuathiri uchumi wa nchi.

Kaim alisema upandaji miti unakwenda kutekeleza agizo la serikali la kuhakikisha kila Mtanzania anashiriki katika uhifadhi wa mazingira ikiwa hatua ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Waziri wa Madini ambaye ni Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, alisema wataendelea kuenzi na kusimamia kaulimbiu ya serikali ya kuhakikisha wanatunza mazingira ili yalete manufaa.

Mavunde alisema ili kufikia lengo hilo wataendelea na kampeni mbalimbali za kuhakikisha mazingira yanatunzwa ili kuifanya Dodoma kuwa ya kijani.

"Kwa kutambua kuna changamoto ya ukataji miti, tumeandaa programu maalum ambayo tutawezesha wananchi wetu kuacha kukata miti kwa ajili ya kutengeneza mkaa na badala yake tutawahimiza kuanza kutengeneza mkaa kwa kutumia karatasi na uchafu ambayo itasaidia kutunza mazingira," alisisitiza.

Ujumbe wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka huu unahusu mabadiliko ya tabianchi na uhifadhi mazingira sambamba na utunzaji wa vyanzo vya maji "Tunza Mazingira, Okoa Vyanzo vya Maji kwa Ustawi wa Viumbe Hai kwa Uchumi wa Taifa."

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# PM aagiza ma-RC kuunda vituo vya uwezeshaji wananchi kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa miezi mitatu kwa wakuu wa mikoa nchini ambao hawajaanzisha vituo vya uwezeshaji wananchi kiuchumi kama ilivyoelekezwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020/2025, kufanya hivyo kabla ya mwakani.

Aidha, amewataka viongozi na watendaji wakuu wa taasisi za umma na sekta binafsi kuimarisha huduma za uwezeshaji ili kufikia malengo yaliyowekwa na kutimiza dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan, kukuza uwezeshaji na kupunguza umaskini nchini.

Akifungua kongamano la saba la uwezeshaji kiuchumi jijini Dodoma jana, alisema uanzishaji wa vituo hivyo uko kikatiba na mikoa ambayo haijafanya hivyo ni muhimu ikakamilisha ili kuwezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi zitakazowaongezea kipato.

"Katika hili ninawapongeza Mkoa wa Dodoma kwa kuwezesha Jukwaa la Mkoa kuanzisha SACCOs 76 za wanawake zenye wanachama 322 pamoja na Halmashauri ya Ushetu ambayo imeanzisha jukwaa linaloendesha mradi wa kampuni ya usafi wa mazingira na usindikaji wa mboga za majani maarufu kwa jina la Nsansa," alisema.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'i Issa, alisema kongamano hilo linalenga kuongeza ufahamu wa wadau mbalimbali kuhusu dhana ya uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuwakumbusha majukumu waliyonayo katika kuwawezesha Watanzania.

Alisema malengo mengine ni pamoja na wadau kupeana uzoefu katika kutekeleza shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi, kuzindua taarifa ya mwaka 2022/2023 ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 ambayo pia imejumuisha masuala ya ushiriki wa Watanzania katika miradi ya kimkakati na uwekezaji unaofanyika nchini.

Katibu Mtendaji huyo alitaja kaulimbiu ya kongamano hilo kuwa ni "Uwezeshaji kwa Uchumi Endelevu". "Kaulimbiu hii inaendana na azma ya serikali ya kuhakikisha Watanzania wanawezeshwa kushiriki kikamilifu katika uchumi wa nchi ili kutimiza malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025."

Pia katika kipindi cha mwaka 2022/ 2023, mifuko na programu za uwezeshaji ilifanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 743.7 kwa wanufaika 6,064,957 na miongoni mwao wanaume ni asilimia 46 na wanawake asilimia 54.



Mganga Mkuu wa Hospitali ya CCBRT, Dk. Cyprian Ntomoka (kushoto), akikabidhi kifurushi cha vitabu vyenye mwongozo wa matibabu ya ugonjwa wa fistula kwa Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Utengamao Tiba Shufaa na Wazee kutoka Wizara ya Afya, Christopher Mariba, jijini Dodoma juzi, kama ishara ya usambazaji rasmi wa mwongozo huo kwa wizara hiyo na waganga wakuu wa mikoa nchini. Katikati ni Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Kinga Wizara ya Afya, Dk. Mwinyikondo Ameir. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tatizo upatikanaji maji shuleni laathiri kiwango cha elimu

**Na Jumbe Ismailly,**
MANYONI

SHULE ya Msingi ya Mtakatifu Vincent, Tarafa ya Itigi, wilayani Manyoni, mkoani Singida inakabiliwa na tatizo la huduma ya majisafi na salama, michango ya chakula na upungufu wa vitabu hali inayokwamisha kupanda kwa kiwango cha elimu shuleni hapo.

Mkuu wa shule, Sista Mariela Ntandu, alisema hayo kwenye taarifa aliyosoma Jubilee ya miaka 25 ya shule hiyo.

Aidha Sista Mariela alisema uhaba wa maji ni tatizo kubwa ambalo kwa kiasi kikubwa linaathiri mazingira yao hususani maji ya kunywa, kupikia, kumwagilia bustani na kufanyia usafi.

Kuhusu michango ya chakula, alisema baadhi ya wazazi na walezi wa wanafunzi wa shule hiyo hawakusanyi michango kwa wakati na kusababisha mwalimu kupoteza muda mwingi kufuatilia.

Kwa mujibu wa Sista Meriela, kuchelewa kwa michango hiyo ya chakula kwa wakati mwingine husababisha mwalimu kupoteza kipindi chake na kuwaathiri wanafunzi kwenye masomo hasa kwa kukosa chakula.

Kuhusu vitabu, alisema shule ina upungufu wa vitabu vya kiada hasa mtaala mpya, na kwamba tatizo hilo linatokana na mabadiliko ya mara kwa mara ya mitaala.

Meneja wa shule hiyo, Sista Verediana Hermani, alisema walimu wazuri walioweka msingi imara wakati wa kuanzishwa kwa shule hiyo, imeendelea kufanya vizuri mpaka sasa.

Kwa mujibu wa Sista Veridiana ambaye ni Mkuu wa Province, kuanzishwa kwa shule hiyo ni msukumo wa viongozi na wanakijiji wa Mitundu, baada ya kuona matokeo mazuri ya wanafunzi wa chekechea iliyoanzishwa na masista waasisi chini ya uongozi wa Sista Carmen Saxl.

Katibu wa Askofu wa Jimbo la Singida, Faza Gilbert Mwiru aliyemwakilisha Askofu wa Jimbo Katoliki Singida, alishukuru serikali kwa kuibeba shule hiyo tangu ilipokuwa kwenye mchakato wa kuanzishwa, licha ya kuwapo kwa changamoto ambazo walizikabili.

Sista Gilber ambaye ni Katibu wa elimu wa jimbo hilo, aliwaomba watendaji wa Serikali ya Wilaya ya Manyoni kuendelea kuwasaidia viongozi wa shule hiyo ili iweze kuendelea kufanya vizuri zaidi mwaka hadi mwaka.

Akimwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Kemirembe Lwota, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Itigi, Husseni Simba, aliwakumbusha viongozi wa madhehebu ya dini katika wilaya hiyo kuwalea vijana katika misingi ya kiroho ili waweze kuwa na mioyo ya hofu kwa Mungu kwenye majukumu yao ya utendaji.

Shule ya Msingi ya Mtakatifu Vincent iliyoanzishwa miaka 25 iliyopita ilitoa zaidi ya wahitimu 1,500 ambao wengi wao ni wafanyakazi serikalini, wajasiriamali pamoja na wanazuoni.

# TCRA yaja na mfumo wateja kutoa maoni

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), inatarajia kuanzisha mfumo wa kisasa utakaojulikana Tanzanite Portal, utakaotoa fursa kwa wateja kutoa maoni.

Mkurugenzi wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, alisema hayo juzi alipotembelea dawati la wateja na kushirikiana na wafanyakazi wengine wa mamlaka hiyo, kutoa huduma kwa wateja, ikiwa ni wiki ya huduma kwa wateja.

Alisema kuanzishwa kwa mfumo huo kutasaidia kuimarisha mazingira bora ya huduma kwa wateja na walaji na kuleta mapinduzi katika utoaji wa huduma ya mawasiliano nchini.

Pia alisema kuanzishwa kwa mfumo huo kutasaidia kupunguza urasimu katika utoaji wa leseni za mawasiliano.

"Mawasiliano ni uhai wa taifa letu na tuna wajibu wa kuhakikisha yanafanyika bila vikwazo kwa manufaa ya Watanzania wote na kwa hili tumejipanga ili itusaidie kutoa huduma ya kipekee kwa wadau wetu hususani watumiaji na wateja wa huduma za mawasiliano," alisema Dk. Bakari.

"Tunataka kuhakikisha mtoa huduma anatimiza wajibu wake kwa ufanisi. Tanzanite Portal ambayo inapatikana kupitia tovuti ya mdhibiti wa mawasiliano, imeundwa ili kurahisisha mawasiliano kati ya TCRA na watoa huduma wote wa sekta ya hii, siyo tu kusikiliza kero zao bali pia kuchukua hatua madhubuti na kuzishughulikia."

Dk. Bakari alisisitiza kuzingatia umuhimu wa kurekodi na kuchambua maoni yanayopokelewa kutoka kwa watumiaji na kwamba hiyo ni moja ya mbinu ya kusaidia katika uboreshaji wa sera pamoja na mipango ya kuimarisha zaidi sekta ya mawasiliano nchini.

"Takwimu tunazokusanya kutoka kwa wadau wetu zitaleta mabadiliko chanya na kwa kuwa dhamira yetu ni thabiti, kwa kushirikiana na wateja wetu, Tanzania itaendelea kufurahia huduma za kisasa za mawasiliano," alisema Dk. Jabiri.

Miongoni mwa wateja waliohudumiwa na Mkurugenzi huyo wa TCRA ni Mkurugenzi wa Mawasiliano na Uhusiano wa Airtel, Beatrice Singano, ambaye pamoja na mambo mengine, alipongeza maboresho yanayofanywa na mamlaka hiyo hadi sasa katika kuhudumia wadau wake.

"Nimefurahishwa na jinsi mdhibiti wetu anavyofanya kazi zake kwa sasa hususani kwenye dawati la wateja ni nzuri sana, rafiki, ninaamini ujio wa Tanzanite Portal ni mwanzo mwingine mzuri zaidi katika utoaji wa huduma za mawasiliano nchini," alisema Singano.

Eugenia Chanda, mdau wa mawasiliano mkoani Dar es Salaam, alisema kuanzishwa kwa mfumo wa kisasa wa wateja kutoa maoni ni hatua nyingine ya maendeleo inayofanywa na TCRA na anaamini yatasaidia kuongeza ufanisi na uwazi katika utoaji wa huduma hiyo nchini.

# Wanafunzi kutoka familia maskini Manyara kupewa viatu

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

SERIKALI mkoani Manyara inatarajia kugawa viatu pea 2,500 kwa wanafunzi wa shule za msingi 24 ambao wanatoka katika familia ambazo hazina uwezo ili kuwapa molari ya kusoma vizuri.

Hayo yalibainishwa jana na Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Alisema shule ambazo wanafunzi watapewa viatu ni ambazo ziko barabarani.

Sendiga alisema serikali itagawa viatu hivyo kupitia Taasisi ya Mama ongea na mwanao ambayo ndiyo inaratibu kuhakikisha kila mtoto anayetoka familia isiyokuwa na uwezo anapata mahitaji ili aweze kuhudhuria masomo.

"Kuanzia Oktoba 6 tutawavisha viatu watoto wetu wa Kiteto ili wakipokea Mwenge wa Uhuru wawe wanakumbuka tukio hilo na baada ya hapo tutaenda kuwavisha watoto wa Simanjiro," alisema Sendiga.

Aidha, alisema kampeni hiyo haijaanza leo bali ilianza muda mrefu na katika mikoa mingine ilishawapa manufaa.

Mkuu huyo alisema kampeni hiyo inaratibiwa na msanii Stevin Nyerere na itakuwa endelevu siyo kwamba itaishia hapo.

Kuhusu maandalizi ya kilele cha mbio za Mwenge wa Uhuru alisema yamefikia asilimia 98 na ujenzi wa Uwanja wa Kwaraa umeishakamilika kwa asilimia 100.

Alitumia fursa hiyo kuvishukru vyombo vya habari kwa kulitangaza tukio hilo la kitaifa ambalo litahitimishwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Kadhalika, aliwaomba wananchi wote mkoani hapa kujitokeza Oktoba 14 kwenye kilele cha mbio za Mwenge wa Uhuru, Wiki ya Vijana na kushiriki ibada ya kumbukizi ya Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Nyerere itakayofanyika katika Kanisa la Romani Katoliki Babati.

# GGML yaibuka mshindi wa jumla Maonesho ya Madini Geita

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

KAMPUNI ya Geita Gold Mining Limited imenyakua tuzo nne ikiwamo ya mshindi wa jumla katika Maonesho ya Teknolojia ya Madini yaliyofanyika kwa siku 10 mjini Geita na kushirikisha washiriki zaidi ya 400.

Katika maonesho hayo ambayo yalianza Septemba 20 hadi 30 mwaka huu, Hospitali ya Rufani ya Mkoa Geita kwa kushirikiana na GGML walitoa huduma za upimaji saratani kwa wananchi zaidi ya 1,000.

Akifunga maonesho hayo kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman aliipongeza GGML kwa kuibuka na tuzo ya Mwoneshaji Bora kwa Mwaka 2023.

Kampuni hiyo pia ilipewa hati maalum ya shukrani kwa kuwa mdau muhimu tangu kuanzishwa kwa maonesho hayo mwaka 2018 pamoja na hati ya shukrani ya kuwa mdhamini mkuu ambapo kwa mwaka huu ilitoa zaidi ya Sh. milioni 150.

Akisoma hotuba hiyo kwa niaba ya Rais Samia katika maonesho hayo, Suleiman alisema Dira ya Sekta ya Madini (Vision 2030) inalenga kumaliza changamoto za muda mrefu kwa wachimbaji wadogo za kukosekana taarifa za kuaminika za maeneo yenye rasilimali hiyo.

Dira ya 'Madini ni Maisha na Utajiri' imelenga kuhakikisha hadi kufikia 2030 utafiti wa madini kwa njia za jiofizikia uwe umefanyika nchini kwa zaidi ya asilimia 50.

"Serikali inaendelea kuhakikisha wachimbaji wa madini wanapata masoko ya uhakika na itaendelea kuwawezesha wawekezaji wadogo wa sekta hii kwa kuwaunganisha na taasisi za fedha," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa GGML, Terry Strong, alisema katika siku 10 za maonesho hayo anaamini washiriki wakiwamo wachimbaji wadogo wamejionea na kujifunza teknolojia mbalimbali ambazo GGML inazitumia kuhakikisha uchimbaji madini unafanyika kwa usalama na tija.

"Dhamira yetu ni kuongeza thamani kwa wadau wetu wote kuanzia shughuli za utafiti, uchimbaji na uchakataji dhahabu kwa kuongezea thamani na mambo mengine.

"Ni kwa sababu hiyohiyo tumefanya juhudi zote kuwezesha uhamishaji ujuzi na teknolojia kama inavyoonekana katika maendeleo ya miradi yetu mitatu ya uchimbaji na ushiriki wa wasambazaji wa bidhaa na watoa huduma wazawa," alisema.

Alibainisha kuwa GGML imekuwa inatoa kipaumbele kwa wazawa kupata mafunzo na zabuni za utoaji huduma ndani ya migodi ya kampuni hiyo kwa mujibu wa matakwa ya sheria 'local content' ambapo kwa mwaka 2015 kampuni hiyo ilitumia Dola za Marekani milioni 202 na kiwango kimeongezeka hadi kufikia dolaza Marekani milioni 526 mwaka 2022.

Meneja Mwandamizi anayeshughulikia Uhusiano wa Jamii, Gilbert Mworia, mbali na kuishukuru serikali kwa kutambua jitihada za kampuni hiyo, alisema GGML itaendelea kutoa mafunzo kwa Watanzania na wachimbaji wadogo ili wapate fursa mbalimbali ndani ya mgodi huo.

Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, alisema wanaamini ifikapo mwaka 2025, mchango wa sekta ya madini katika Pato la Taifa utafikia asilimia 10.



Askofu wa Jimbo Katoliki Moshi, Mhashamu Ludovick Minde (kulia), akizindua moja ya majengo ya Shule ya Sekondari Marry Goreti, Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya jubilee ya miaka 25 ya shule hiyo hivi karibuni. **PICHA: JAMES LANKA**

# Mradi utatuzi migogoro nje ya Mahakama wafanikiwa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MRADI wa majaribio wa utatuzi wa migogoro ya kifamilia kwa kutumia njia mbadala za utatuzi nje ya vyombo vya Mahakama na Polisi (ADR), umepata matokeo Chanya.

Matoe hayo ni baada ya viongozi wa mila wa kimasai kuja na mageuzi makubwa katika masuala ya elimu kwa watoto wa jamii za kifugaji, mirathi na haki ya kumiliki ardhi kwa watoto wa kike.

Matokeo hayo yameanza kuonekana kuchipua katika Kata ya Karansi, Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, ambako mradi huo unatekelezwa.

Akizungumza jana katika Manispaa ya Moshi, wakati wa kikao kazi cha tathimini ya maendeleo ya mradi wa ADR, mshili wa ukoo wa Laizer, Saitabahu Laizer, alisema katika kata hiyo jamii ya kifugaji ya kimasai imeanza kustaarabika, imehamasika na inapeleka watoto wao shule na hazirazimishi watoto wa kiume kwenda kuchunga mifugo.

"Kule kwetu (Karansi) tumehamasika sana, sasa hivi Wamasai wanasomesha, Wameru wanasomesha na Waarusha wanasomesha, yaani kabila zote hizo zimeamka na wanashindana na Wachaga kusomesha watoto.

"Ukikuta haendi shule, hawasomeshwi, labda mmoja maana hawakosekani watu au familia za aina hiyo.

...Wamasai sasa hivi wanalipa mtu wa kuchunga ng'ombe, kama ni mshahara anampa mtu mbuzi kila baada ya miezi mitatu. Lakini watoto wao wote wa kike na wa kiume wanaenda shule."

Kuhusu ardhi, mshili huyo alisema jamii ya kifugaji ya kimasai katika kata hiyo watoto wa kike walioolewa hawaruhisiwi kunufaika na mgawo wa ardhi ya familia, ila taratibu za kimila zimeruhusu ambaye hajapata mume au kuolewa kurithi ardhi ya makazi na kilimo.

"Kwenye mirathi, kama mke amefiwa na mume, sasa hivi kule kwetu umasaini hakuna kumnyang'anya mali, iwe ardhi au nyumba na mali nyingine alizoachiwa na mumewe.

"Sisi Washili na maleigwanani, tunasimamia na ni utaratibu uliokokwenye mila."

Mradi huo wa mwaka mmoja unaendeshwa na Shirika la KWIECO, kwa ufadhili wa Legal Service Facility Tanzania (LSF).


Mratibu wa mradi huo, Lilian Mandari, alisema mradi unalenga zaidi kurahisisha upatikanaji wa haki kwa haraka zaidi.

Mradi huo unahusisha pia makundi mbalimbali ikiwamo wasaidizi wa kisheria walioko wilaya za Mkoa wa Kilimanjaro, maofisa maendeleo ya jamii, maofisa ustawi wa jamii, dawati la jinsia, wanasheria wa halmashauri na wadau wengine.

Mmoja wa wasaidizi wa kisheria, Immaculate Mwigani, alisema mradi huo umeongeza uelewa wa jamii kuhusu sheria na kuimarisha mfumo wa kifamilia katika utatuzi wa migogoro kwa kuzingatiwa viwango vya sheria nchini.

Mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Lucas Mnyula, alisema faida za mradi huo wa KWIECO/ADR, ni walengwa wa shauri husika watakaopita katika jopo la watoa huduma, baada ya usuluhishi kufanyika nje ya Mahakama kuishi kwa amani na upendo, kwa sababu hakupatikana mshindi katika kesi yao.

Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Mrakibu Asia Matauka, akizungumzia mradi huo alisema mradi wa utatuzi migogoro nje ya mahakama ni mzuri na unaweza kuleta tija katika jamii.



# Wilaya ya Ukerewe ya kwanza kutekeleza agizo la RC Makalla

**Vitus Audax,** UKEREWE

AGIZO la Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, la kila wilaya kutenga siku maalum ya kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua limeanza kutekelezwa wilayani Ukerewe.

Akizungumza na Nipashe jana kabla ya kufanyika kwa mkutano, Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe, Hassan Bomboko alieleza kuwa mkutano huo na wananchi wa Ukerewe wanatarajia kwenda kusikiliza na kutatua kero zote zinazowezekana kutatuliwa papo kwa papo.

Alisema mkutano huo utawakutanisha wananchi wa visiwa vyote pamoja na maeneo yote wilayani humo katika viwanja vya Gertrude Mongella ambako watakuwapo pia viongozi wa idara zote kusaidia utatuzi huo wa kero.

"Wilaya yetu ina wananchi wenye shughuli mbalimbali wakiwamo wavuvi, wakulima, wafugaji pamoja na wafanyabiashara, hivyo tutasikiliza kero, changamoto pamoja na migogoro wanayokabiliana nayo na kutatua," alisema Bomboko.

Aliongeza kuwa baada ya uzinduzi huo shughuli zitakuwa endelevu katika maeneo mbalimbali ya wananchi ambao hawatapata nafasi ya kuwasilisha kero zao, huku waliowasilisha kero bila kupata ufumbuzi zikiendelea kufanyiwa kazi.

"Rais Samia Suluhu Hassan ana nia ya kuhakikisha kila mwananchi anapatiwa haki na stahiki zake kwa wakati, hivyo sisi kama wawakilishi wake jukumu letu ni kuwafikia na kutatua changamoto za wananchi katika maeneo yetu," alieleza Bomboko.

Septemba 17 mwaka huu Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, alianzisha operesheni hiyo kwa kuwaita wananchi wote wenye kero, migogoro na changamoto mbalimbali katika mkutano wa pamoja.

Lengo la kufanya hivyo ni kutatua kero ambako idadi kubwa ya migogoro iliyoibuka katika mkutano

**"Wilaya yetu ina wananchi wenye shughuli mbalimbali wakiwamo wavuvi, wakulima, wafugaji pamoja na wafanyabiashara,**



huo ni ya ardhi pamoja na wananchi kunyimwa haki katika kuhudumiwa.

Kupitia mkutano huo Makalla aliwaagiza wakuu wote wa wilaya mkoani hapa kufanya mikutano ya namna hiyo ili kuhakikisha wanawafikia wananchi na kutatua kero zao.



Mkurugenzi wa Uzalishaji wa Kampuni ya Tumbaku ya Alliance One Tobacco Tanzania, David Mayunga (wa pili kulia), akifafanua jambo wakati akizungumza na viongozi wa vyama vya wakulima wa tumbaku kutoka mikoa ya Tabora, Kigoma na Shinyanga, waliotembelea kiwanda hicho, mkoani Morogoro juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Diwani 'kula sahani moja' na wazazi wanaowaozesha wanafunzi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

DIWANI wa Kata ya Nyamilangano Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, Robert Mihayo, amewatangazia kiama wazazi wenye tabia ya kuwaozesha wanafunzi wanaohitimu elimu ya msingi.

Alitoa kauli hiyo juzi katika Shule ya Msingi Nyamilangano na kueleza kuwa kwa mzazi yeyote ambaye ataendekeza tamaa za kupata mali yuko tayari kuwaburuza mahakamani.

Alisema serikali imekuwa ikiboresha mazingira ya kujifunzia kuhakikisha wanafunzi hususani wa kike wanasoma vema na kutimiza ndoto zao, hivyo kuwataka wazazi kutumia kikamilifu fursa hiyo kupeleka watoto wao shule bila kujali jinsia zao.

Akitoa taarifa ya shule, Mwaliku Mkuu wa shule hiyo, Mussa Yombo, alisema kuwa shuleni hapo kumekuwa na vitendo vya kuhama wanafunzi bila taarifa, huku wengine wakiachishwa shule na kwenda kuozeshwa kwa siri ili kujipatia mahari.

Altolea mfano wa darasa la saba waliohitimu mwaka huu kuwa walianza darasa la kwanza wakiwa 330 na wanaohitimu elimu ya msingi ni 190, kati ya hao wanafunzi wa kike 118 na wanafunzi wa kiume ni 72.

Kadhalika alieleza kuwa miongoni mwa wanafunzi wa kike waliohitimu elimu ya msingi mwaka huu mmoja wao alitoroshwa na kwenda kusikojulikana, wazazi wake walitoa taarifa katika vyombo vya sheria akatafutwa na kupatikana na baada ya vipimo alibainika kuwa ni mjazito.

Mmoja wa wazazi wa wanafunzi shuleni hapo, Maziku Mayala alisema kitendo cha kumwozesha mtoto wa kike angali bado ni mwanafunzi ni uvunjifu wa sheria na kuiomba serikali kuwachukulia hatua kali za kisheria wanaobainika kujihusisha na vitendo hivyo.

Hata hivyo, aliwataka wazazi wenzake pindi wanapoona kitendo hicho kinatokea wasisite kushirikiana na vyombo vya usalama katika kutoa ushahidi mahakamani ili mhusika awajibishwe kisheria.

# Kortini wakituhumiwa kuuza petroli, dizeli kiholela

**Na Remmy Moka,** SAUT

WATU wawili wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza wakituhumiwa kutenda makosa mbalimbali ikiwamo la kuuza mafuta ya petroli na dizeli bila kuwa na leseni pamoja na vibali maalumu.

Watuhumiwa hao ni Saidi Hussein (38) mkazi wa Kilimahewa wilayani Ilemela mkoani Mwanza na Leonard Stephano (37), mkazi wa Ibungilo wilayani Ilemela ambao walifikishwa mahakamani hapo na kusomewa makosa sita katika shtaka moja la jinai namba 146/2023.

Akisoma mashtaka hayo mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Ilemela, Fortunatus Kabaja, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Mwanahawa Changale alisema washtakiwa walitenda makosa hayo Septemba 23, 2023, eneo la Bwilu Wilaya Ilemela mkoani Mwanza.

Alitaja kosa hilo kuwa ni kinyume cha Kifungu Namba 131 (1), (4) cha Sheria ya Petroli Toleo Namba 21 ya Mwaka 2015 pamoja na kutunza petroli kinyume na Sheria Kifungu Namba 178 (1), (3) cha Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015, Toleo Namba 21.

Makosa mengine katika shtaka hilo alisema ni kuuza mafuta ya petroli bila kuwa na vifaa vya kiusalama kinyume na Kifungu Namba 179 (1), (2) (b) ya Sheria ya Petroli Toleo Namba 21 ya Mwaka 2015, kuuza vifaa vya petroli kinyume na Sheria Namba 179 (1), (2) (c) ya Sheria ya Petroli Toleo Namba 21 ya Mwaka 2015.

Vilevile washtakiwa hao walisomewa kosa la kukutwa na mali zinazosadikika kuwa ni za wizi kinyume na Kifungu Namba 312 (1) (b) cha Sheria ya Petroli Toleo Namba 21 ya Mwaka 2015.

"Washtakiwa walikamatwa na maofisa wa polisi wakiwa na lita tano za mafuta ya petroli, lita 235 za mafuta ya petroli na mipira 23 ya plastiki vyote vikiwa na thamani zaidi ya Sh.milioni 1.9 kinyume na sheria," alisema Changale.

**Alitaja kosa hilo kuwa ni kinyume cha Kifungu Namba 131 (1), (4) cha Sheria ya Petroli Toleo Namba 21 ya Mwaka 2015**

Aidha, baada ya kusomewa shtaka hilo watuhumiwa hao walirejeshwa mahabusu baada ya kushindwa kumudu masharti ya dhamana, huku hakimu akiahirisha kesi hiyo mpaka itakapoitwa kwa ajili ya kupokea maelezo ya awali.

ALHAMISI OKTOBA 5, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Magereza nayo yapokea kijiti na mbiu hadi sasa imepanda 850,000**



Ukurasa 13

Amesafiri umbali kilomita 800 kufuata matibabu ya moyo



Ukurasa 14

**Ukatili wa jinsia shida, wavulana kwa wasichana kote 'hakufai'**

MAZINGIRA

KAMPENI UPANDAJI MITI...

# Alichozindua Dk. Samia 2017, kinazidi kupamba moto kwa hamasa mikoani

- Makazi mapya 'Dodoma ya kijani' yatia fora

**Na Mwandishi Wetu**

AKIWA Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, ambaye jina lake la leo lina utangulizi wa kishangilio daktari, mnamo Desemba 2017, akaagiza kampeni mahsusi ya kustawisha miti jijini Dodoma ikiendeshwa na majeshi ya ulinzi na usalama, akielekeza ienee wilaya zote kitaifa.

Ilikuwa siku chache akiwa amehamia kwenye mji huo, wakati huo ofisi yake ina dhamana ya moja kwa moja kutetea mazingira nchini, akitamka jukumu hilo haliishii katika kuhifadhi mazingira, pia ni fursa kwao kiuchumi.

Hapo Samia akatoa elimu namna jukumu la kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, lina manufaa kiuchumi, akitumia mfano mti uliokomaa, unaweza kunyonya hadi kiasi cha kilo 150 za gesi ya hewa ya ukaa kwa mwaka, hata ukauzwa.

Hadi sasa mkoa wa Katavi, umeshaanzisha miradi ya namna hiyo kwa mafanikio kibiashara, inayobadili uchumi wa nchi na mtu mmoja mmoja, huku akisifu ubunifu ulioasisiwa na ofisi yake yenye Waziri anayeshughulikia Mazingira, wakati huo alikuwa Januari Makamba.

Samia akasisitiza suala hilo la kupanda miti liwe endelevu, akizitaka halmashauri zote nchini zitunge sheria ndogo zitakazoelekeza shule, vyuo, taasisi na familia, kuanzisha bustani ndogo za miti zitakazomudu mazingira husika.



Dk. Samia Suluhu Hassan, alipoweka udongo katika mti alioupanda, eneo la JKT Mgulani Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam, wakati wa uzinduzi kampeni ya upandaji miti mkoa huo. Sasa ni dhana ya kitaifa. **PICHA: MTANDAO**

Makamu wa Rais akaelekeza kwamba ni vyema kupunguza ukataji miti kiholela, akitaka sheria, kanuni na taratibu zizingatiwe, miti ipandwe mingine, kabla ya kukatwa.

Kwenye uzinduzi huo, walikuwapo wadau kufanikisha kama kampuni ya Tatu Mzuka, Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Makutopora, Dodoma, Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dodoma (DUWASA), Magereza na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

Hilo likaendana na rai yake Mama Samia, akiwataka kinamama Dodoma, kuanzisha vikundi vya upandaji miti. Daima Dk. Samia, hajautupa msimamo huo, sasa mwaka wa tatu katika urais nchini.

Si hatua ngeni kwake, kwani mnamo Oktoba Mosi, 2016. Samia akaongoza mamia ya wakazi wa Dar es Salaam, kuzindua kampeni ya upandaji miti inayojulikana 'Mti wangu jijini Dar es Salaam."

Wakati huo, Makamu Mkuu wa Nchi, akauambia umma uliojitokeza katika uzinduzi kwenye Barabara ya Kilwa -Kurasini, wilayani Temeke, kwamba serikali imeviagiza vyombo vya dola mkoani Dar es Salaam, jukumu la kutunza miti iliyopandwa isiharibiwe na vihakikishe inakuwa vizuri, kuifanya Dar es Salaam bora katika utunzaji mazingira.

Samia akasema, ni hatua ya kurejesha uoto wa asili na utunzaji wa vyanzo vya maji kote kitaifa

**KINACHOENDELEA SASA**

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Dk. Selemani Jafo, amezindua Wiki ya Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, Juni Mosi mwaka huu jijini Dodoma, akisema Tanzania inaendelea na mikakati, pia sera endelevu za uhifadhi na usimamizi endelevu wa mazingira.

Katika hilo, anataja suala la upandaji miti, ili kukabili athari za uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi, kukiwapo ajenda ya mazingira ya miaka mitatu.

**INAENDELEA UK.13**

**KAMPENI UPANDAJI MITI...**

MAZINGIRA

# Magereza nayo yapokea kijiti na mbiu hadi sasa imepanda 850,000

**Na Mwandishi Wetu**

NI kampeni aliyoanzisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, mwaka 2016 mkoani Dar es Salaam na kuipa mkazo mwaka unaofuata, Desemba 2017, jijini Dodoma.

Hiyo kampeni, sasa inaungwa mkono na serikali na vyombo vyake, pia taasisi na wadau binafsi, ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za serikali kwenye ushiriki wa kutunza mazingira nchini.

Kunatajwa shule, pia hospitalini panastahili kupandwa miti, hali kadhalika penye ushirikiano wa wadau kitaasisi, kama vile za dini na zingine binafsi, serikali zikihimiza kupandwa miti zaidi.

Zao lake linatajwa kuwa katika maeneo yao yote; wengi wanashuhudiwa kutii, wakipokea matunda ya ustawi wa miti.

Ni juhudi zinazoshikiliwa na mamlaka za kidola, zikihimiza kusimamia ustawi wake, huku uzinduzi jijini Dodoma ukifanywa na Makamu wa Rais wakati huo mwaka 2017, ambaye sasa ni Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, baadhi ya vyombo vya dola, vilikuwa na mchango mkubwa.

Jeshi la Magereza nchini, sasa limepanda jumla ya miti 850,000 katika maeneo ya Magereza na mengine ndani ya mwaka mmoja, ambao Kamishna Jenerali Jeshi Ramadhani Nyamka, amekuwa akihimiza upandaji miti katika maeneo yao, kuhakikisha wanakabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Miti iliyopandwa ni aina tofauti, ikijumuisha ya matunda, hata ikazifanya zilete kivuli, kugeuza maeneo hayo kuwa ya kijani, katika dhana ya kampeni inayosisitizwa na Rais Dk. Samia.

Sasa inatajwa ni hali inayochangia kukabili ukame, kwenye ardhi yake inayobadilika kuwa na asili ya unyevu.

**MKUU WA MAGEREZA**

Kamishna Jenerali Nyamka, anasema Jeshi la Magereza linathamini utunzaji na uboreshaji wa mazingira, ndio maana wamepanda miti katika maeneo yao na mengineyo, pia ikiwa na lengo la kuunga mkono jitihada za serikali kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Kamishna Jenerali, anasema pamoja na Magereza kufahamika kwa jukumu lao kubwa ni kulinda haki za raia husussani wafungwa, pia utunzaji mazingira nao unawahusu, kwa sababu pia wao ni sehemu ya jamii.

"Na sisi ni sehemu ya jamii, ndio maana tunashiriki shughuli za kijamii za kupanda miti, kama wanavyofanya jamii nyingine katika maeneo mbalimbali nchini," anasema Kamishna Jenerali Nyamka.

Anafafanua kuwa idadi waliyofikia sio mwisho wa upandaji miti, harakati zinaendelea kuhakikisha kunafikiwa tamko la serikali kutunza mazingira katika maeneo jamii inakoishi, ili kuhimili mabadiliko ya tabianchi ya kila mara.

Kamishna Nyamka anafafanua kuwa, miti hiyo wamepanda ikiwa ni ya matunda na bado inatoa faida kwa wahusika, hususani kwenye kuvuna matunda ambayo ni muhimu kwa jamii.

Pia, anataja inawezesha biashara ya kuvusha matunda kwingineko, ikirejesha kipato kwa muuzaji, huku akiahidi Magereza itaendeleza upandaji miti kutimiza azma hiyo ya kimazingira, kuunga mkono jitihada za kiserikali.

**MKUU KILIMO MAGEREZA**

Mawazo Makenzi, ni Kamishna Msaidizi wa Magereza anayehusika na kilimo, anasema utaratibu wa kupanda miti ndani ya Magereza utaendelezwa katika mikoa mbalimbali, lengo kuona mazingira yanaboreshwa kwa kupanda miti.

Makenzi anasema, kuna mikoa ambayo haijafikiwa, ila iko katika malengo yao kitaifa, akifafanua: "Jeshi la Magereza linathamini sana kuhusu suala la utunzaji mazingira.

Pia, anasema wanafaidika kuwa na udongo wenye rutuba nzuri, inayomuwezesha mkulima kufanya kilimo chenye tija kiuchumi.

Kamishna Msaidizi Makene, anasema miti husaidia kuondoa ukame, hivyo wito wake kwa jamii ni kuunga mkono jitihada za serikali za kuboresha mazingira, kwa kupanda miti katika maeneo mbalimbali, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

**WAZIRI JAFO**

Seleiman Jafo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Muungano na Mazingira), anatahadharisha umuhimu wa jamii kutunza mazingira, kwani kinyume chake uchumi wa umma unayumba, hususani kwenye kilimo, kutokana na ukame ambao utakuwepo, hali inayoathiri pia uzalishaji viwandani.

Jafo anarejea ni hali inayoangusha nchi, kupata mazao kidogo, ndio sababu yeye binafsi anazihimiza halmashauri zote nchini kuhakikisha wanapanda miti katika maeneo yao, ili kuboresha na kutunza mazingira na nchi kuwa ya kijani.

Hiyo anajijengea rai kwamba, halmashauri zote zinapaswa kutimiza lengo la serikali iliyojiwekea katika upandaji miti, ili kuhakikisha kunakuwapo mazingira bora katika maeneo mbalimbali nchini. Pia, anasisitiza halmashauri na taasisi kuanzisha kampeni za kuhimiza upandaji miti, ili kuihakikishia jamii ione suala hilo ni kazi kama zilivyo nyinginezo.

**HOJA ZA WANANCHI**

Hapo wananchi wadau katika hilo, wanaipongeza serikali upandaji miti kitaifa, kwa sababu limechangia kumaliza ukame, katika baadhi ya maeneo hapa nchini.

Mkazi wa Dodoma, Lucia Kasano, anasema awali Dodoma ilionekana kama ni eneo kame, lakini tangu serikali ianze kuhimiza suala zima la utunzaji mazingira, hivi sasa miji imeonekana ni eneo la kijani katika baadhi ya maeneo, ambayo miti imepandwa.

"Tunaishukuru sana serikali kutokana na kuhimiza suala la upandaji miti, tunaomba liwe zoezi endelevu kwa jamii ili kuhakikisha nchi yetu inakuwa na mazingira bora ambayo yataiwezesha kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi pale yatakapotokea," anasema.

Anasema miti ina faida kwa jamii, hivyo wananchi wanapaswa kupewa elimu ya upandaji ili kila moja ahakikishe anapanda miti ya kutosha kama moja ya kuunga mkono jitihada za serikali za upandaji miti.



Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza Ramadhan Nyamka, akimwagilia mti katika eneo la jeshi baada ya kupanda kwa ajili ya uboreshaji mazingira. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

## Alichozindua Dk. Samia 2017, kinazidi kupamba moto kwa hamasa mikoani

**INATOKA UK.11**

Anasema ni hatua inayopewa msukumo na serikali, katika kampeni za usafi wa mazingira na upandaji miti, kukabili athari za tabianchi, akitoa mfano katika visiwa Unguja na Pemba, maji yanaongezeka maji ya bahari kwenye makazi ya wananchi, kunakotokana na kuyeyuka barafu, hata kuongeza kiwango cha maji baharini.

Kwa mujibu wa Waziri Jafo, serikali pia imezielekeza mamlaka za serikali za mitaa, kuhakikisha vibali vya ujenzi wa makazi vinavyotolewa kwa wananchi, viendane na wajibu kwao kupanda miti katika eneo husika, ili kulinda mazingira.

Katika kuendeleza alichozindua Rais Dk. Samia, mwaka 2017, wakati huo akiwa makamu wa rais, Dk. Jafo ana ufafanuzi: "Takribani miti Milioni 276 itapandwa kila mwaka na hili ni lengo la kila Halmashauri kupanda miti Milioni 1.5 kila mwaka.

"Kwa hapa Dodoma, lengo ni kupanda miti milioni 40 ambalo ni lengo la kipekee, ukilinganisha na mikoa na wilaya nyingine nchini. Tunazishukuru Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kusimamia vyema kampeni hizi."

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule anaishukuru Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kuendelea kuipatia ushirikiano ofisi yake kwa kuendelea kutoa msukumo na hamasa ya uhifadhi wa utunzaji wa mazingira.

Anasema, huo ni mpango mkakati wa mazingira ambapo mkoa wa Dodoma umetajwa kupiga hatua nzuri katika kutimiza hilo kwenye uhifadhi wa mazingira.

'Tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuanzisha mchakato maalum wa kampeni ya 'Dodoma ya kijani'. Miti yote mikubwa iliyopo sasa ilitokana na juhudi zake wakati akiwa Makamu wa Rais. Tutahakikisha maelekezo yote yatakayotolewa tupo tayari kuyatekeleza" anatamka mkuu wa mkoa.

Anasema, ofisi yake pia imeweka mikakati kulinda vyanzo vya maji, ikiwamo Bonde la Mzakwe, Dodoma, eneo lililopandwa miti ya kutosha kutokana na hamasa kubwa ya umma.

AFYA

HALI YA TIBA

# Amesafiri umbali kilomita 800 kufuata matibabu ya moyo

• Miaka 40 katika dozi inayompa ahueni

**Na Christina Mwakangale**

"NIMEANZA kutumia dawa mwaka 1980 nilipojifungua mtoto wa pili, ndipo tatizo lilianza. Niliolewa mwaka 1978 nikiwa na miaka 21. Ninatumia dawa hadi sasa ingawa awali nilikuwa natumia pale ninapoumwa tu..."

Ni simulizi ya Magreth Mwaijala, mkazi wa kijiji cha Katumba, wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya. Mahali hapo ni umbali wa takribani kilomita 800 kutoka Dar es Salaam, kunakopatikana huduma muhimu za kijamii, ikiwamo matibabu ya kibingwa ya madaktari.

Magreth anasimulia anavyoishi na ugonjwa wa presha (shinikizo la juu la damu), anapokutana na gazeti la Nipashe kwenye kambi ya siku mbili ya kuchunguza Magonjwa Yasiyoambukiza (NCDs), ikiwamo presha, iliyoandaliwa na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) na kufanyika katika Hospitali ya Dar Group-JKCI.

Tanzania, ni miongoni mwa nchi zenye ongezeko 'NCDs'. Takwimu za mwaka 2021 zinaonyesha wagonjwa 3,440,708 walitibiwa na idara za wagonjwa wa nje (OPD) kwenye hospitali tofauti nchini, ikilinganishwa na 3,852,973 waliotibiwa mwaka 2022 ikiwa ni ongezeko 412,265 sawa asilimia 12.

Takwimu hizo ni kwa mujibu wa Meneja Mpango wa Taifa wa Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza kutoka Wizara ya Afya, Valeria Millinga, akizungumzia hali ya magonjwa hayo nchini na mikakati ya kukabiliana nayo.

"Magonjwa ambayo yanaongoza ni pamoja na shinikizo la juu la damu (presha) na kisukari. Katika magonjwa 10 yanayoongoza kusababisha vifo nchini, yapo manne yaliyo kwenye kundi la NCDs; magonjwa ya moyo kwa asilimia 4.5 na shinikizo la damu asilimia 3.8 nafasi ya tatu," anasema Valeria.

**MAISHA YALIVYO**

Magreth (66), ni mama wa makamo, lakini bado ana nguvu unapomuona. Ameketi kwenye kiti akiwa miongoni mwa watu takribani 100 waliofika siku ya kwanza ya kambi hiyo katika Hospitali ya Dar Group-JKCI, mkabala na makutano ya barabara kuu Dar es Salaam, Mandela na Nyerere.

Nipashe, inasogea jirani naye na anaitikia wito wa mahojiano. Magreth anafafanua: "Nimekuja Dar es Salaam kwa ajili ya matibabu, nipo kwa watoto wangu Kimara. Nilipotazama taarifa ya habari katika televisheni nikaona nije kufanya uchunguzi. Nimetumia dawa kwa zaidi ya miaka 40 sasa.

"Naweza kusema mbali na kudra za mwenyezi Mungu, kuwapo hai hadi leo, kuanza tiba mapema ya presha ni miongoni mwa msaada mkubwa kwa umri wa maisha yangu," anasema na kuongeza:

"Mwaka 1980, nilipitia changamoto za kifamilia, mara napata msukosuko huu, nikaanza kusikia mapigo ya moyo kwenda mbio. Nikalazwa Hospitali ya Morogoro, kabla haijapandishwa hadhi na kuwa ya mkoa, miaka hiyo tuliishi Morogoro mume wangu aliajiriwa huko.

"Nilikwenda kwenye vipimo kwa mara ya kwanza wakabaini nina tatizo la presha. Kwa hiyo, sikuanza kutumia dawa, wakasema nisubiri kwanza kwa kuwa ni mara ya kwanza. Ila nikarudi tena hospitali, tatizo likawa pale pale, wakaniandikia dawa, nikaanza kuzitumia hadi sasa," anaeleza Magreth.

Anasema, awali hakuzingatia umuhimu wa matumzi ya dawa alizoandikiwa na madaktari kila siku 30, badala yake alikunywa pale tu alipohisi mwili kuwa na mabadiliko.


"Nilitumia kila nilipojisikia kuwa ninaumwa...nikaambiwa tumia kila siku maadam umeapata tatizo hilo ni hatari linaweza kukuletea matatizo kila siku, sina bima ninanunua kwa pesa taslimu kila ninapokuwa na fedha, ila changamoto inakuja ninapokuwa sina fedha nashindwa kukamilisha dozi ya mwezi," anasimulia. Magreth.

Anasema matumizi ya fedha ya kila mwezi, hayapungui Shilingi 45,000 hadi Shilingi 50,000, ikiwa ni pamoja na nauli ya kwenda kurudi kuzifuata dawa, vilevile kliniki kwa ajili ya magonjwa hayo.

"Nanunua dawa ya Losartan Shilingi 25,000 na Amlodipine Shilingi 10,000 na pia Asprin junior kuanzia Shilingi 3,500 hadi Shilingi 4,500 ila kuna wakati siwezi kununua dozi yote ya mwezi, nanunua vidonge vichache vya siku mbili au tatu, ama wiki, ikiisha narudi tena kununua, sina ya bima ya afya."

Magreth, ametumia dawa za presha kwa miongo minne, akiwa na watoto saba na makundi ya wajukuu wapatao 20, anasema anaporudi nyumbani kwake Tukuyu, anapeleka ujumbe wa kuhamasisha jamii vijana kwa watu wazima, kufika hospitalini mapema kufanya vipimo na kubaini iwapo wanaugua ugonjwa huo na mwingine na kuanza tiba mapema.

> Naweza kusema mbali na kudra za mwenyezi Mungu, kuwapo hai hadi leo, kuanza tiba mapema ya presha ni miongoni mwa msaada mkubwa kwa umri wa maisha yangu.



Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Dk. Peter Kisenge akisikiliza mapigo ya moyo ya mgonjwa kutoka nchi jirani ya Malawi, Anna Kamwaza, aliyelazwa katika taasisi hiyo. **PICHA: JKCI**

Brigita Boaz, yeye ni mkazi wa River Side, Ubungo, mkoani Dar es Salaam, anasifu kambi hiyo, akisema ni muhimu kwa kuwa inasaidia kuwafikia wananchi wengi ambao hawana bima za afya na wenye wenye uchumi mdogo.

"Nimeona bora nije kufanya vipimo katika kambi hii ya bure, kwa siku za hivi karibuni mapigo ya moyo yako sawa. Nashauri watu wafike, ili kutibua iwapo wana matatizo ya kiafya," anasema Brigita.

**HALI ILIVYO NCHINI**

Valeria anasema, katika kila vifo vitatu, vinavyotokea nchini, kimoja kinasababishwa na magonjwa hayo yasiyoambukiza.

"Taarifa ya hali duniani zinaonyesha watu milioni 42 (sawa na asilimia 71 ya vifo vyote) walifariki duniani kwa magonjwa haya. Tanzania asilimia 33 ya vifo vyote vinachangiwa na NCD," anasema na kuongeza;

"NCDs huchangia kwa asilimia 75 ya vifo vyote vinavyohusu watu wenye miaka 30-70. Shinikizo la Juu la Damu na Kisukari huchangia kwenye matatizo ya kiharusi (stroke) na figo kwa zaidi ya asilimia 25 ya wagonjwa wote."

**WANAVYOUGUA PRESHA**

Dk Kisenge anasema, wakati taasisi hiyo ya JKCI imewafikia wananchi takribani 7,000 kwenye kambi kama hiyo kwa mikoa 11 nchini, kupitia mpango wa TIBAMKOBA, huku wengi wa waliochunguzwa afya zao wakibainika kuwa na tatizo la presha bila kujijua.

"Unakuja kutibiwa wakati moyo umekwishatanuka matibabu yake ni ghali, mfano kubadilisha valvu inaweza kufikia Shilingi milioni 10 hadi 12 kwa upasuaji mmoja. Hivyo ni vyema ukapima afya, ili kama kuna matibabu endelevu ni vyema yatapunguza athari.

"Programu ya TIBAMKOBA ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan imewafikia wananchi 7,000 ambao tulibaini wanaugua. Zipo sababu kadhaa ambazo zinafanya mtu asifike kwa wakati kupata huduma hospitalini kama za kiuchumi, hivyo mpango huu, unasaidia watu wa kundi hilo," anasema Dk. Kisenge.

Bingwa huyo anasema, nchini magonjwa ya moyo hasa kwa wagonjwa wanaolazwa hospitalini, yanashika nafasi ya tatu ya takwimu ya vifo ikilinganishwa na mengine, kama vile ya kuambukiza yakiwamo malaria na Ukimwi, huku duniani, magonjwa ya moyo yakigharimu maisha ya watu takribani milioni 17 kila mwaka.

AFYA

# Ukatili wa jinsia shida, wavulana kwa wasichana kote 'hakufai'

• Walioko vitani walia ishara ni mbaya

**Na Yasmine Protace**

MFUMO wa maisha mara zote unabaki kuwa kikwazo kwa watoto wa kike na kiume kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia, wakinajisiwa.

Pia mimba za utotoni, ndoa kuvunjika zikitajwa kuwa visababishi vya kuwapo matukio hayo ya ukatili wa kijinsia kwa jamii.

Inaelezwa kuwa baadhi ya wanaume wamezama katika tabia ya kuwalawiti wavulana, wakitarajiwa wamwechaa kubaka wasichana, kwa kuhofia mikasa ya mimba.

Mwenyekiti wa Kituo cha Taarifa na Maarifa, Mabibo jijini Dar es Salaam, Rehema Mwinyi, anasema ukatili wa kijinsia unatokana na sababu mbalimbali, ikiwamo mfumo wa maisha ulivyo.

Anafafanua kwamba, kutokana na kituo chao kuwasaidia watu wanaofanyiwa ukatili kiweze kupata haki sahihi, kuna wajibu wa wanaofanyiwa ukatili wazipeleke taarifa sahihi kuhusu wanavyofanyiwa ukatili.

Mwinyi anafafanua kwamba, hadi sasa uchunguzi wanaoufanya ni kwamba, kinachofanyika kwa yale wanaofanyiwa ukatili, wamebaini ni mfumo wa maisha unaotawala, unachangia kufanyika hayo, ikiwamo hatua za kuvunjika ndoa.

"Mfumo wa maisha, unakuta watoto wengi wanakosa malezi, wanakosa chakula na hivyo wanaamua kutafuta chakula kwa njia ambazo sio halali na hivyo kubakwa au kulawitiwa, ili waweze kupatiwa pesa," anasema.

Kwa mujibu wa Mwinyi, sababu nyingine inagusa hali ya wanandoa kuachana na kusababisha watoto kujilea, ikifungua mlango wa ukatili wa kijinsia, watoto wakiachwa wanajilea. Sababu nyingine zinatajwa za kuwapo mimba za utotoni, mtoto anapojifungua anaachwa akijilea au kulelewa na mtu baki au wazee vijijini, sasa mtoto anajilea mwenyewe na kuamua kujiingiza katika yasiyofaa, hata akafanyiwa ukatili.

Rai yake anataka elimu kwao iendelee kutolewa, ili kuwanusuru watoto wasifanyiwe matukio ya ukatili, kwani baadhi yake wanafanyiwa wavulana, sababu kuu ni wanapokosa pesa za kuingia katika mabanda ya sinema, hata wanaangukia mabaya kwa hitaji la Sh. 200 pekee.

"Watoto wa kiume wanaofanyiwa ukatili hasa wanapokuwa hawana pesa ya kuingia katika mabanda ya kuangalia sinema," anasema.

Anaongeza kuwa baada ya kubaini changamoto za masuala ya ukatili, sasa wanaelekeza nguvu kubwa shuleni kwa kuwapatia elimu ya kijinsia na namna watoto wanajikimu, akisema maisha ya nidhamu zikikubalika, ukatili unaweze ama kwisha au kupungua.

Mwinyi anaeleza kwamba, hata katika ofisi zao wanawapokea watu waliofanyiwa ukatili, pia wanapochunguza sababu ya kufanyiwa ukatili, huangukia jibu la 'mfumo wa maisha.'



Baadhi ya wakazi wa Dar es Salaam wakiwa katika viwanja vya Jakaya Kikwete (JKCI) kwenye Hospitali ya Dar Group, Barabara ya Nyerere, ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Moyo Duniani. **PICHA: YASMINE PROTUS**

> **"Elimu itolewe kwa mabinti mama, ambayo elimu hiyo ikitolewa, itawasaidia wao kuwaelimisha wenzao na wataacha kuzaa bila ya kufuata utaratibu.**

### HATUA ZA WADAU

Kaimu Mkurugenzi wa Shirika la Usawa wa Kijinsia Tanzania (SUKITA), Mwajuma Msafiri, akiwa pia Mkuu wa Dawati la Mafunzo na Uelimishaji, anasema huwa wanawapatia watoto elimu jinsi ya kupambana na halo na matukio ya kikatili.

Anafafanua kurejea mwaka 2014, akisema ukatili ulivyopamba, akifafanua hatua: "Serikali iliweka nguvu kubwa kwa ajili ya kuwalinda watoto wa kike katika ukatili na wakawasahau watoto wa kiume."

Mwajuma anafafanua kwamba, kutokana na nguvu kubwa inayotumika kuwalinda watoto wa kike, sasa imesukumu shari hilo kwa ulawiti kufanywa kwa wavulana. Anasimulia kuwa watoto wa kiume wanaofanyiwa ukatili, huwa hawasemi kwa wazazi na wanaamua kukaa kimya, kwa hofu wanayotishiwa kuuawa.

Pia katika inatajwa sababu za ulawiti na unajisi, ni kukosekana pesa za kwenda kuangalia ama video au kucheza 'gemu', hata wakalazimika kufanya tendo hilo na wanaume, wapate kiingilio hicho.

Anaongeza kwamba, kwa wavulana kila wanaposhiriki tendo hilo hushindwa kuwa wawazi wa mikasa inayowakuta, hali inayochangia matukio ya ulawiti na unajisi kuwa juu maradufu, takwimu zikionyesha uwiano asilimia 60 ya wavulana kunajisiwa, asilimia 40 ni kwa wasichana.

Kutokana na kuwapo matukio hayo ya ukatili, taasisi yao imekuwa ikitoa elimu kwa watoto jinsi ya kulinda na ukatili wa kijinsia, sasa taasisi yao iko katika hatua kupambana na ukatili wa ngono.

"Wanatoa elinu ili iwasaidia wanafunzi, ili wawe mabalozi shuleni na sasa wana mpango wa kwenda masokoni, misikitini na makanisani, kwa ajili ya kutoa elimu ya masuala ya ukatili," anafafanua.

Anaongeza kuwa changamoto anayoiona ni kwa baadhi ya watu kufanyiwa ukatili wa kijinsia na kushindwa kutoa taarifa au wengine kumaliza majumbani, ili kesi zisiendelee.

Mdau huyo anatoa uzoefu kwamba, kwa sasa matukio ya ukatili wa kijinsia yanatokea baada ya wazazi kutengana na kusababisha watoto kujilea wenyewe, ikifungulia milango ya ukatili wa kijinsia.

"Chanzo cha wanawake kutelekeza watoto na kusababisha kukaa na mama wa kambo, nayo inachangia kufanyika ukatili kwa jamii," anasema.

Anaeleza, hatua waliofikia ni kwamba kumeshatolewa elimu stahiki ianyohusu afya ya akili kwa umma, kwa kuwa hali hiyo nayo ina mchango kuangukia kwenye madhila la ubakaji, ulawiti na kunajisi watoto.

Kwa mujibu wa mwelimishaji huyo, tangu kuanzishwa taasisi yao, wameweza kushughulikia haki za watoto na wanawake, ikijumuisha zaidi ya kesi 50 na kati yake 30 zimeendana na hukumu ya watu kwenda jela, zingine zikipelekwa ustawi wa jamii, zikashughulikiwe.

Hadi sasa SUKITA inafanya kazi katika wilaya ya Temeke, Ubungo na Kigamboni, kukishuhudiwa kuwapo changamoto katika masuala ya ukatili wa kijinsia.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Macho kwa Jamii, ambaye ni Mwenyekiti wa Kituo cha Taarifa na Maarifa Manzese, Dar es Salaam, Theresia Lihanjala, anasema kuwa hali ya watu kukosa hofu ya Mungu, hata wakaanguki kwenye ukatili huo.

Pia anataja hali ya umaskini, nao unachangia ukatili huo wa kijinsia, kuwapo vijana wanaojifungua watoto bila ya kuwa na matarajio, kunawafanya watoto kukosa mahitaji muhimu na wanaamua kujiingiza katika uhusiano wa kimapenzi.

"Unakuta mtoto kazaa mtoto, kumtunza hawezi, anamwachia mtoto wake mtu amlelee! Na mtoto anapokosa huduma za kimsingi, anajiingiza katika uhusiano na kufanyiwa ukatili," anasema.

Anaongeza kuwa watoto wengi wanapoyakosa malezi, ni hali inayochangia kukosa hamu ya kusoma na wanajiingiza katika makundi yasiyofaa, hata wakafanyiwa ukatili huo, akitoa mfanikio na uzoefu anadai kuushuhudiwa eneo la Manzese.

"Elimu itolewe kwa mabinti mama, ambayo elimu hiyo ikitolewa, itawasaidia wao kuwaelimisha wenzao na wataacha kuzaa bila ya kufuata utaratibu," anasema.

Jamal Juma, anatamka sababu ya kuwapo tamaa zinazosababisha watoto kufanyiwa ukatili wa kijinsia, huku

Zuwena Juma akisema, kushamiri matukio ya ukatili kwa kijinsia zote, kukishuhudiwa kunashamiri kwa wanaume.

Zuwena anafafanua: "Wanaume nao hufanyiwa ukatili, unakuta mwanamke kulazimisha apewe taraka huku akitaka mgawanyo wa mali uwe sawa, lakini suala la watoto libaki kulelewa watoto na baba yao.





# Serikali kufikisha huduma ya utangamano vituo vya afya

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema imejipanga kuhakikisha huduma za utangamano kwa watu wenye mahitaji maalum kiafya zinapatikana maeneo yote, hususani katika vituo vya afya.

Hayo yalielezwa na Mratibu wa Huduma za Afya Wazee (Idara ya Tiba) Wizara ya Afya, Dk. Msafiri Kabulwa, wakati wa Kongamano la Afya Tanzania (THS), kwenye mkutano wa huduma za utangamano ulioandaliwa na Taasisi ya Rehab Health.

Dk. Kabulwa alisema bado kuna changamoto ya kufikisha huduma za utangamano kwa watu wenye mahitaji maalum kiafya katika ngazi ya vituo vya afya, lakini kwa sasa huduma hiyo inapatikana pekee katika Hospitali ya Taifa, mikoa na wilaya.

Alisema wataalamu wa tiba ya kuzungumza na sikizi, tiba ya viungo, tiba ya kazini, afya ya akili na madaktari wa mifupa wapo wachache na wanapatikana hatika hospitali za mikoa na kidogo wilaya.

Mwazilishi wa Taasisi ya Rehab Health, Remla Shirima, alisema lengo lao ni kuhakikisha huduma za utangamano kwa watu wenye mahitaji maalum kiafya zipatikane ngazi ya chini.

Alisema pia kuhakikisha mafunzo yanapatikana kwa wataalamu kwa sababu idadi ya madaktari katika sekta hiyo ni wachache.

Remla alisema pia wanahakikisha kunakuwapo na maeneo maalum ya kupata huduma hiyo katika hospitali pamoja na vifaa vya matibabu.

Remla alisema: "Bado kuna tatizo la upatikanaji wa huduma ya utangamano, pia wataalamu wa idara hiyo nao wapo wachache hawafiki 2,000. Hivyo ndiyo maana tunashirikiana na serikali na wadau wengine kuhakikisha huduma hii inawafikia Watanzania wengi".

Alisema lengo la Rehab Health ni kuhakikisha kunakuwapo na upatikanaji wa vifaa saidizi, upatikanaji wa mafunzo kwa wataalamu wa kutoa tiba hiyo pamoja na kushirikiana na wadau wengine wa sekta ya afya ili kukuza sekta hiyo.

**Alisema wataalamu wa tiba ya kuzungumza na sikizi, tiba ya viungo, tiba ya kazini, afya ya akili na madaktari wa mifupa wapo wachache na wanapatikana hatika hospitali za mikoa na kidogo wilaya.**

# NaCongo yaiangukia serikali malimbikizo madeni ya kodi

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

BARAZA la Asasi za Kiraia Tanzania (NaCONGO) limeiomba serikali kuwafutia malimbikizo ya madeni ya kodi na kufanyika kwa marekebisho ya sheria ya kodi iliyopo kwa sababu wanatoa huduma na sio wafanyabiashara.

Mratibu wa Mtandao wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Ole Ngurumo, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizindua ripoti ya hali ya ulipaji kodi kwa sekta isiyo na faida Tanzania.

Ole Ngurumo aliomba serikali kufanya marekebisho ya sheria hiyo na kusamehe madeni yao ili kutoa nafuu kwa asasi za kiraia zilizopo nchini kwa sababu wao wanatoa huduma kwa wananchi.

"Tunaona kwamba sisi kama sekta ambayo haijiendeshi kwa kupata faida tunaona ipo haja ya kukaa na serikali, ndio maana katika ripoti yetu tuliyoizindua leo tumezunguka nchi nzima na asasi zimetoa maoni yao," alisema.

Alisema wamezunguka nchi nzima kukusanya maoni kwa asasi za kiraia 1,500 na maoni yao ni hayo ya kuomba kufutwa kwa sheria pamoja na kupata msamaha wa madeni wanayodaiwa.

Alibainisha kuwa asasi za kiraia zinatakiwa kutambuliwa kama wakusanyakodi kwa niaba ya serikali na siyo walipakodi kama sheria iliyopo inavyowatambua watu kwa sasa.

Alieleza kuwa sekta hiyo inatafuta fedha za ndani na nje kutoka kwa walipa kodi kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania.

Kadhalika, alisema wamependekeza kuwa kwa wale watakaokuwa wanafanyabiashara kupitia asasi za kiraia watawekewa sheria maalumu zisije zikafanya kuonekana sekta nzima inafanya biashara.

Aidha alisema sekta hiyo wameingiza fedha zaidi ya Sh. trilioni mbili kutoka nje na wamekuwa wakitoa ajira kwa makundi mbalimbali ya wananchi hapa nchini na nje ya nchi.

Mwenyekiti wa Baraza la NACONGO, Dk. Lilian Badi, aliomba kuwapo kwa madawati ya majadiliano ya kikodi kuanzia ngazi ya wilaya na NGO'S ili wapate mjumbe kwa kila dawati.

Dk. Badi alisema lengo la madawati hayo itakuwa kupokea malalamiko mbalimbali ya kikodi kutoka kwa wananchi na makundi mengine.

Aliongeza kuwa asasi nyingi zinafanyakazi kwenye ngazi za huko chini, hivyo uwepo kwa dawati itakuwa na tija katika ukusanyaji wa kodi za serikali.

Kamishna wa Sera na Utafiti kutoka Wizara ya Fedha, William Mhoja ambaye alimwakilisha Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba alisema ameyachukua maoni hayo na watawaita ili kukaa nao ili kupata ufumbuzi.

Mhoja alisema serikali imeanzisha kikosi kazi ambacho kinasikiliza malalamiko ya kikodi na kimeanza kazi kwa baadhi ya mikoa nchini.



Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Mashirika yasiyo ya Kiserikali Tanzania (NaCoNGO), Dk. Lilian Badi, akiwasilisha maoni ya mashirika hayo, wakati wa uzinduzi wa ripoti ya hali ya ulipaji kodi kwa sekta isiyo ya faida Tanzania, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Jamii yatakiwa kutowaficha watoto wenye ulemavu

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

JAMII imetakiwa kuacha kuwaficha majumbani watoto wenye ulemavu ili wapate hadhi zao za msingi ikiwamo elimu.

Mhasibu wa Mradi wa Elimu Jumuishi, Anna Pusse, kutoka Shirika la Tanzania Chesire Foundation linalotekeleza mradi wa elimu Jumuishi katika Mkoa wa Dodoma na Shinyanga alitoa rai hiyo jana kwenye maonesho ya wiki ya asasi zisizo za serikali jijini hapa.

Pusse alisema bado kuna tatizo kwenye jamii ya uelewa kuhusu watoto wenye ulemavu kutakiwa kwenda shule, hivyo serikali kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali wanapaswa kuongeza jitihada katika utoaji elimu kwa wazazi na walezi.

"Bado kuna baadhi ya maeneo wanawaficha watoto wenye ulemavu, wazazi, walezi msifanye hivyo, mnachotakiwa toeni ushirikiano kwa mashirika yanayotoa msaada wa elimu kwa jamii hiyo wanapowatafuta watoto,"alisema Pusse.

Aliongeza: "Katika utekelezaji wa mradi huo wameshakutana na vikwazo vingi ikiwamo kufukuzwa kwingine wanakuta watoto wamefungiwa majumbani kwa muda mrefu, kwa hiyo akitolewa anakuwa anaogopa kuchangamana na watu."

Hata hivyo alisema katika mradi huo tayari wamewafikia watoto zaidi ya 2,800 katika mikoa ya Dodoma na Shinyanga ambao wanaendelea na masomo ya elimu jumuishi katika shule mbalimbali za msingi.

Mmoja wa wanufaika wa mradi huo, Isaya Peter, alisema jamii itoe ushirikiano kwa mashirika ambayo yanatekeleza mradi mbalimbali kwa ajili ya kuwainua watu wenye ulemavu.

Alisema wazazi na walezi wanapaswa kuacha dhana potofu ya kwamba kuwa na mtoto mlemavu kwenye familia ni mkosi jambo ambalo sio kweli.

# TRA yaanzisha kampeni wananchi kudai risiti

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Singida, imewataka wananchi kujenga utamaduni wa kudai risiti wanaponunua bidhaa ili kuepuka kutozwa faini ya asilimia 20 au Sh. 30,000 ya bidhaa alizozinunua.

Meneja wa Elimu kwa Mlipakodi TRA, Sadru Kamugisha, alitoa kauli hiyo juzi kwenye uzinduzi wa Kampeni ya Tuwajibike inayolenga kuwahamasisha walipakodi na wananchi kwa ujumla kuhusu wajibu wao wa kutoa na kudai risiti halali kwa kutumia mashine za EFD.

Alisema kampeni hiyo ina malengo ya kuwakumbusha na kuwasisitiza wauzaji wa bidhaa na watoa huduma nchi nzima kuwajibika kwa kutoa risiti halali ya EFD kila wanapouza bidhaa au kutoa huduma mbalimbali.

Kamugisha alisema kampeni hiyo pia inawakumbusha na kuwahamasisha wanunuzi wa bidhaa na huduma kote nchini kuwajibika kudai risiti halali ya EFD pamoja na kuzikagua ili kujiridhisha kuwa inakidhi vigezo vyote muhimu.

Naye Meneja wa TRA Mkoa wa Singida, Azaria Kasomi, aliwahimiza wafanyabiashara kuwa wazalendo kwa kutoa risiti kulingana na kila ambacho wamekiuza kwa wateja wao ili kuepuka usumbufu wanaoweza kupata wasipotoa risiti.

Akizindua kampeni hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Singida, Mhandisi Paskas Muragili, alisema wafanyabiashara wanatakiwa kuiunga mkono serikali kwa kulipa kodi halali ili kuleta maendeleo kwa wananchi.

Hivyo, aliiagiza TRA Mkoa wa Singida kuendelea kutoa elimu juu ya matumizi ya mashine za EFD na umuhimu wa kutoa risiti kupitia kampeni hiyo na baada ya wafanyabishara kuelimishwa kutafanyika operesheni kwa wasiozingatia hayo na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.



# Bashungwa: Nina shaka na kitengo ununuzi TANROADS

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAZIRI Ujenzi, Innocent Bashungwa, ameshtukia kitengo cha ununuzi cha Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS) akisema kuwa inawezekana 'kinacheza dili' kwa kuwapatia tenda makandarasi wasiokuwa na uwezo wa kufanya kazi, hali ambayo inasababisha miradi ya serikali kutekelezwa chini ya kiwango ama kutokamilika kwa wakati.

Akizungumza wakati akikagua mradi wa ujenzi wa barabara ya njia nne inayoanzia eneo la Nsaraga hadi Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA) mkoani Mbeya, Waziri Bashungwa alisema kuwa amebaini kuwa kitengo cha manunuzi cha wakala huo kinatoa tenda bila kuzingatia vigezo.

Alisema katika ziara yake mkoani Mbeya alibaini mkandarasi aliyepewa tenda ya kujenga Barabara ya Ibanda- Kanjunjumele (km. 22), Barabara ya Kanjunjumele-Kiwira Port (km 6) pamoja na Kanjunjumele- Itungi Port (km 4) akiwa hajaanza kazi na wala vifaa hana.

Alisema kutokana na hali hiyo huwenda kuna mchezo mchafu baina ya kitengo hicho cha manunuzi na makandarasi wanaopewa kazi hizo jambo ambalo alisema hawezi kulivumilia.

"Haiwezekani mkandarasi ambaye hana vifaa anapewa kazi ya ujenzi wa barabara, anasubiri tukisha mlipa fedha za advance (malipo ya awali) ndio anakwenda kununua vifaa Uturuki, hali hii inatukwamisha kwa sababu inasababisha miradi yetu isikamilike kwa wakati," alisema Bashungwa.

Kutokana na kubaini 'mchezo' huo Bashungwa alikionya kitengo hicho na kumwagiza Mtendaji Mkuu wa TANROADS kukiangalia kwa jicho la karibu kabla yeye mwenyewe hajachukua hatua.

Pia aliwaonya watendaji wa kitengo hicho cha manunuzi kuwa makini wakati wa kufanya tathmini ya manunuzi ili kuepuka kuwapatia tenda makandarasi ambao hawana uwezo.

Katika hatua nyingine, Bashungwa alitoa wiki mbili kwa mkandarasi anayejenga barabara hizo za wilayani Kyela kuhakikisha anafikisha vifaa kwenye mradi ili kazi ya ujenzi iendelee badala ya sasa ambapo vifaa vipo vichache.

Alisema mkandarasi wa barabara hiyo alisaini mkataba Aprili lakini mpaka sasa ni asilimia 15 pekee ya vifaa ndivyo vimefikishwa kwenye mradi hali ambayo haileti matumaini ya mradi huo kukamilika kwa wakati.

Kaimu Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Bonface Mkumbo, alisema ujenzi wa barabara ya njia nne katikati ya Jiji la Mbeya ulikuwa unachelewa kuanza kwa sababu miundombinu mbalimbali ilikuwa haijaondolewa kwenye eneo la kazi.

Alisema miundombinu ambayo ilikuwa haijaondolewa ni ya umeme, maji na mawasiliano ya simu na kwamba kwenye baadhi ya maeneo ambayo imeondolewa mkandarasi anaendelea na kazi.

Alisema barabara inajengwa kwa Sh. bilioni 138 na inatarajiwa kukamilika baada ya miaka miwili, huku akisisitiza kuwa utaanzia katika eneo la Nsalaga jijini Mbeya mpaka katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA).

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, alisema watahakikisha wanasimamia mradi huo ili kuhakikisha unakamilika kwa wakati na wananchi wanaanza kunufaika nao.



Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC), Ndele Mwaselela, akizungumza na vijana wa seneti ya vyuo na vyuo vikuu vya Mkoa wa Mbeya alipokuwa akifungua mafunzo ya ujasiriamali na ajira juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Polisi ajiua kwa risasi akiwa nyumbani kwa mpenzi wake

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ASKARI mwenye namba J.2596 Kontebo wa Polisi, Samwel Kaziyote (24) wa Kituo Kikuu cha Polisi mkoani Mbeya, amejiua kwa kujipiga risasi akiwa nyumbani kwa mpenzi wake baada ya kuibuka mzozo baina ya wawili hao.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi Benjamin Kuzaga, alisema tukio hilo lilitokea Oktoba 2, mwaka huu saa 2:15 usiku katika Mtaa wa Mzumbe Foresti ya Zamani jijini Mbeya.

Alisema askari huyo alitoroka kazini kwenye moja ya benki zilizopo jijini hapa na kwenda kwa mpenzi wake huyo akiwa na silaha ambayo alikuwa anaitumia kwenye lindo aina ya AK. 56 ikiwa na risasi.

Alisema uchunguzi wa awali walioufanya walibaini kuwa baada ya askari huyo kufika nyumbani kwa mpenzi wake huyo uliibuka mzozo baina yao ambao ndio ulikuwa chanzo cha kijana huyo kujipiga risasi.

Kamanda Kuzaga alisema baada ya mzozo huo kuwa mkubwa mpenzi wa askari huyo alikimbia na kutoka nje kisha akamfungia marehemu mlango kwa nje kama sehemu ya kujihami asipigwe na ndipo kijana huyo akachukua maamuzi magumu.

"Alijipiga risasi kwenye kidevu ambayo ndiyo iliyosababisha kifo chake papo hapo, lakini tunaendelea kufanya uchunguzi zaidi wa tukio hili ili hatua zingine zichukuliwe, lakini hili ni tukio baya sana," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema mpenzi wa marehemu ambaye jina limehifadhiwa, anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa ajili ya upelelezi zaidi wa tukio hilo ambalo alisema siyo la kawaida.

Aliwataka askari kuwa waadilifu na kuhakikisha wanafanya kazi kwa kuzingatia sheria za kazi hiyo ikiwa ni pamoja na kuepuka matumizi mabaya ya silaha wanazopewa kwa ajili ya kuzitumia wawapo kazini.

# Watakiwa kuepuka kupanda miti adui kwa vyanzo vya maji

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANANCHI mkoani Njombe wametakiwa kuepuka upandaji wa miti ambayo sio rafiki kwa vyanzo vya maji ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Hayo yalielezwa na Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, baada ya kutembelea chanzo cha mradi wa maji cha Lugenge kilichopo katika Halmashauri ya Mji Njombe utakaonufaisha wakazi zaidi ya 10,000.

Mtaka alisema unaweza ukawa nje ya mita 60 lakini miti iliyopandwa ikawa na madhara makubwa kwenye vyanzo vya maji.

Hata hivyo alisema pia wananchi wanatakiwa kuepuka ugomvi usio wa lazima kwa kulima kandokando ya vyanzo vya maji. "Wananchi waepuke ugomvi na serikali kwenye kulima pembeni mwa vyanzo vya maji, lakini kwa wale ambao wanalima nje ya vyanzo vya maji waepuke miti ambayo haitakuwa rafiki kwenye vyanzo vya maji ukaweka miti itaenda kuua chanzo chenyewe cha maji," alisema Mtaka.

Pia alishauri kwamba ni vizuri miradi ya maji ikaunganishwa na uzalishaji.

"Maana yake hivi vyote vinaenda wananchi wanapata unakika wa maji ni uhai, lakini wanaofanya shughuli za kilimo wanapata maji ni uchumi kwenye kilimo, mambo yamebadilika sana maana kuna mashirika yanadizaini matone maana yake ni kwamba hatutaathiri mradi na inapendeza unaposema mradi huu utahudumia watu 10,000 lakini unaweza ukahudumia mashamba madogo madogo ya mboga ya hekali 100 lakini na mashamba makubwa 300 aina ya miti," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Maji, Fedelis Lumato, alisema miaka miwili iliyopita upatikanaji wa maji ulikuwa asilimia 56 lakini hivi sasa yanapatikana kwa asilimia 72.

Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Judica Omari, alisema asilimia 40 ya mapato ya ndani ya halmashauri yanatokana na mazao ya misitu, hivyo wananchi wanapaswa pia kupanda miti ambayo ni rafiki ili kuepuka vyanzo vya maji kukauka ndani ya mkoa.

Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa, alisema anaamini mradi huo utasaidia kutatua changamoto ya maji, huku wakiwa wanasubiri mradi mkubwa wa miji 28.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Njombe (NJUWASA), John Mtyauli, alisema mradi huo utagharimu Sh.bilioni 8.7, unategemea kuhudumia Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Njombe pamoja na wakazi wanaozunguka eneo hilo wapatao 10,235.



## Serikali yatoa bilioni 21.5/- kudhibiti mfumuko wa bei wa bidhaa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum, amesema Serikali ya Zanzibar imetoa Sh.bilioni 21.5 ikiwa ni ruzuku kwa bidhaa ya mafuta yanayoingia nchini kwa ajili ya kudhibiti mfumuko wa bei wa bidhaa.

Aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akiwasilisha mapendekezo ya Ripoti ya Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2023-2024.

Alisema serikali itaendelea kutoa ruzuku kwa kadri ya hali ya mfumuko wa bei ya mafuta katika soko la dunia itakavyopanda, ili kuhakikisha maisha ya wananchi yanakuwa na utulivu mkubwa.

Alisema Zanzibar imekuwa na utulivu wa bei za bidhaa ikiwamo nishati ya mafuta katika nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, kwamba kwa sasa serikali imejipanga zaidi kuimarisha miundombinu ili kuharakisha mwenendo wa biashara na nchi jirani.

Pia alisema Serikali ya Zanzibar imeingia makubaliano na Kampuni ya AGL kutoka Ufaransa kwa ajili ya kuendesha Bandari ya Malindi na kuleta ufanisi wa shughuli za upakuaji na uingizaji wa mizigo.

Alisema katika kipindi kifupi mafanikio ya kasi ya utoaji na uingizaji wa mizigo imeonekana ikiwamo meli kukaa bandari kwa wastani wa siku tano kutoka siku 10 za awali.

Dk. Mkuya alisema awali Bandari ya Malindi ilizidiwa na msongamano wa mizigo, meli hukaa nje ya bandari kwa zaidi ya mwezi mmoja na kusababisha malalamiko mengi kutoka kwa wamiliki wa meli ikiwamo kuongezeka kwa ushuru wa meli.

Aidha, alisema pia serikali imekamilisha ukarabati mkubwa wa Bandari ya Mkoani Pemba katika eneo la sehemu ya ujenzi wa kuhifadhi makontena.

Alisema hatua hiyo sasa itawezesha baadhi ya meli kwenda Pemba kushusha bidhaa za mizigo ambapo itasambazwa moja kwa moja kwa wafanyabiashara, hivyo kupunguza gharama ikiwamo kupanda kwa bei za vyakula.

Mkuya alisema hizo ni sehemu ya juhudi za kwenda kukifungua Kisiwa cha Pemba na kuwa lango kuu la kiuchumi na uwekezaji katika Afrika ya Mashariki na Kati.

# Unyanyasaji, udhalilishaji watoto Zanzibar bado tatizo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera na Uratibu wa shughuli za Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma, amesema bado kuna hali ya unyanyasaji na udhalilishaji dhidi ya watoto visiwani hapa.

Aliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi wa matokeo ya utafiti wa awali wa kutathmini matokeo ya Mpango wa Pili wa Kunusuru Kaya Maskini Tanzania, utafiti huo pia umeonyesha hali ya unyanyasaji na udhalilishaji kwa kaya maskini.

Alisema takwimu zinaonesha kuwa ndani ya miaka minne hali ya matukio ya udhalilishaji ni mengi na hayapungui, hivyo ni vyema wananchi kujitathmini wanakosea wapi.

"Utamaduni wetu Wazanzibari ni watu wakarimu, rahimu, wakushirikiana na watu wa kusaidiana. Lakini utafiti unaonyesha ndani ya miaka minne hali ya udhalilishaji ipo lazima tujiulize tumekosea wapi kwa kweli," alisema.

Alisema kama unyanyasaji na udhalilishaji utaendelea hata vizazi vijavyo watarithi matendo hayo, hivyo ni lazima kujirekebisha na kuwa na jamii yenye maadili mema.

Akizungumzia kuhusu utafiti huo wa awali alisema, TASAF (PSSN II) ni mojawapo ya mipango mikubwa inayotekelezwa nchini kwa kuzishirikisha kaya za walengwa katika kupambana na umaskini na kuimarisha uchumi wao. Alisema malengo ya mpango huo ni kuimarisha hali za maisha ya walengwa kiuchumi na kijamii.

Kadhalika alisema katika utekelezaji wa mpango wa kuweka akiba na kuwekeza, kaya za walengwa wanapata mafunzo ya stadi za ujasiriamali na mbinu za kuunda vikundi endelevu vya kuweka akiba na kuwekeza.

Pia alisema miradi ya kuendeleza miundombinu ya afya, elimu, barabara, kilimo, mazingira na maji imetekelezwa kwa walengwa kupitia mpango huo.

Hata hivyo alisema matokeo ya utafiti huo yamelengwa kuonyesha ulinganifu wa hali za kaya zilizo katika mpango na unafuu wa gharama za kutekeleza shughuli za mpango katika vijiji vilivyochaguliwa na ambavyo kwa sasa vinaendelea kupatiwa fedha za ruzuku kwa walengwa.

Alisema matokeo yameonyesha kuwa wastani wa matumizi kwa siku ni Sh. 1,419 kwa kutumia kiwango cha ubadilishaji wakati wa kukusanya taarifa, kwamba kiwango hicho kipo chini ya mstari wa umaskini wa Tanzania wa Sh. 1,859.

Alisema matokeo yanaonyesha jumla ya matumizi ya kaya kwa mwezi ni wastani wa Sh. 152,621, matumizi ya chakula ni Sh. 113,256.

Naye Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Salum Kassim Ali, alisema katika kupunguza umaskini uliokithiri, serikali imeweka mpango wa kunusuru kaya maskini wenye lengo la kusaidia kaya maskini kwa kupewa ruzuku na fedha.

Alisema dhumuni kuu la mpango huo ni kuimarisha upatikanaji wa fursa za mapato na huduma za kiuchumi katika jamii na wanakaya ambazo zipo katika hali ya umaskini.

Mkurugenzi wa Mfumko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Shedrack Mziray, alisema kipindi cha kwanza cha kunusuru kaya maskini kilianza kuhudumia zaidi ya kaya milioni moja na utekelezaji wake unafanyika kwa halmashauri 184 kwa Tanzania Bara na Zanzibar.

Alisema madhumuni ya kipindi cha pili cha mpango ni kuziwezesha kaya za walengwa kutumia fursa ya kuongeza kipato, huduma za jamii na kuwekeza katika kuendeleza rasilimali watu.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Jenista Mhagama (kushoto), ajadiliana jambo na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi SMZ, Dk. Khalid Salum Muhammed (kulia) na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara za SMZ, Masoud Muhammed nje ya Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ZEC yaagizwa kufuata Katiba, sheria, miongozo katika kazi

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, ameutaka uongozi wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) kutekeleza majukumu yao kwa kufuata katiba, sheria na miongozo yote katika utendaji wao wa kazi.

Aliyasema hayo jana ofisini kwake Vuga alipokutana na uongozi wa ZEC na kusema kuwa tume hiyo ni chombo muhimu ndani ya nchi ambacho kinategemewa katika shughuli mbalimbali za uchaguzi.

Hemed aliwata viongozi hao kufanya kazi kwa kufuata maadili ya kazi zao na maamuzi yafanyike kwa mujibu wa sheria zinavyoelekeza pasipo na utashi binafsi.

Aidha, aliwataka kufanya kazi kwa umoja na ushirikiano na kutumia taaluma na uzoefu walionao kujenga maelewano kwa lengo moja la kuwatumikia Wazanzibari.

Alisema kuwa Wazanzibari wana imani kubwa na utendaji kazi wa tume hiyo hivyo, wanapaswa kufanya kazi kwa kukidhi mahitaji ya Wazanzibari.

Aidha, aliwataka viongozi hao kuendelea kuelimisha jamii kuhusu masuala ya uchaguzi ili kuweka usawa na umoja kwa Wazanzibari bila ya kujali tofauti zao za kisiasa.

Alisema imani waliopewa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa kuteuliwa kushika nyadhifa hizo ni kwa maslahi ya Wazanzibari hivyo ni vyema kutumia elimu na uzoefu wao katika kusimamia maslahi ya Wazanzibari.

Naye Mwenyekiti wa ZEC, Jaji George Joseph Kazi, alisema kuwa tume hiyo itafanya kazi kwa kufuata misingi ya ya sheria, kanuni na taratibu zilizopo na kutumia uwezo walionao kwa kufanya kazi kwaueledi ili kufikia malengo.

Aidha, alisema kuwa watahakikisha amani na utulivu inakuwapo kabla ya uchaguzi, wakati wa uchaguzi na baada ya uchaguzi na kuwaomba wananchi kuendelea kuiamini na kuipa ushirikiano.

TANGAZO


# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



SARAH MSAFIRI MBILU anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.1224-0010 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia USA RIVER ACADEMY mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: PHQ/DAR/KIN/20239/2023.

## KUPOTEA KWA CHETI



SHAFII IDRISA SHABANI anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S5134-0081 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia KIMANGE SECONDARY SCHOOL mwaka 2016. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: PWA/BAG/RB/183261/2023

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Moshi**
**Kituo cha Moshi Mjini Mkoa Kilimanjaro**
**Shauri la Ndoa 35, 2023**
**Jina la Mdai SUZAN MCHOMVU**
**Jina la Mdaiwa MICHAEL SHABANI NDIMGWANGO**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

Kwa: **MICHAEL SHABANI NDIMGWANGO**
Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta /Wameleta madai yao kwamba (eleza hapa habari za Madai )
Mdai ameleta madai ya talaka , mgawanyo wa mali na matunzo ya mtoto dhidi yako, .Fika Mahakamani kujibu madai hayo
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 23 mwezi 10 mwaka 2023 saa 03:00 asubuhi kwa mujibu wa maombi hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashaidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya w ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 29 mwezi 09 Mwaka 2023



.......................................
**HAKIMU**

## KUPOTEA KWA CHETI



MWANAIDI ABUBAKARI MANGULA anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0199.0017 kilichotolewa na baraza la mtihani la taifa kupitia MSAMALA MUSLIM SEMINARY mwaka 2020. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: MKO/RB/2445/2023


## KUPOTEA KWA CHETI



SOPHIA OBED MBINDO anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index No. S0951/0072/2018 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Tarifa kupitia MLOWA SECONDARY SCHOOL mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: PHQ/DOD/CHA/4246/2023.


**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTATION COUSE 121 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**BARAKA AMOS MWASOMBA**
**DECEASED OF KIKUYU STREET, DODOMA CITY COUNCIL**
**AND**
**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY HOGLA MWASOMBA CHILONGANI**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF THE PROBATE RULES GN NO.369 OF 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of the letters of administration is made to the above named petitioner
Objection to the grant should be filed on or before 25 day of 10, 2023
Dated at Dodoma this 04 day of 10, 2023




**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**LILILOKO DODOMA**
**MAOMBI NA. 03 YA MWAKA 2023**
**FARES ENOCK MAHUHA............MDAI**
**DHIDI YA**
**REONALD LYAJELA ...............MDAIWA 1**
**HAMISI CHISEMWA............MDAIWA 2**
**MIKECHI ONJA ONJA............MDAIWA 3**
**HAMISI HILBA MWINGEREZA.........MDAIWA 4**

KWA:
HAMISI HILBA MWINGEREZA
POPOTE ULIPO.
YAH: KUITWA SHAURINI
Kwa kuwa mwombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika baraza hili wewe binafsi, Wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 01. 11. 2023 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
ANGALIZO:- Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 04 ya mwezi wa OKTOBA, 2023.




## KUPOTEA KWA CHETI



ATHUMAN .O. SALIM anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index No.S1117-0007 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Tarifa kupitia DABALO SECONDARY SCHOOL mwaka 2006. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: SON/RB/685/2017.

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**ABUBAKAR AYOUB MOHAMMED** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye namba **TAE157712** iliyotolewa makao makuu Dar es salaam tarehe 14/08/2019. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/TEM/21455/2023**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 0677020701**

**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**

**WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## OUT yapata mbinu kuongeza mapato

**Na Miraji Msala**

UTAFITI machapisho yenye kukidhi ubora wa ushindani vitasaidia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) kupata ufadhili na miradi itakayoongeza mapato ya ndani ya chuo.

Naibu Makamu Mkuu wa OUT anayesimamia Mipango, Fedha na Utawala, Prof. George Oreku, alitoa kauli hiyo juzi alipofungua mafunzo ya siku tano ya uandishi wa mapendekezo ya utafiti yenye viwango vya juu vya ubora na shindani yanayofanyika Shule ya Uongozi ya Mwalimu Julius Nyerere Kibaha, mkoani Pwani.

"Kurugenzi yetu ya Utafiti, Machapisho na Ubunifu imeundwa kwa lengo kuitumikia taasisi yetu kuhakikisha utafiti, machapisho na ubunifu unaotoka unakuwa na ubora unaokidhi viwango vya hali ya juu. Hapa tunawajengea uwezo wahadhiri kuandika mapendekezo ya utafiti yenye viwango vya kiushindani ili maandiko yao yashinde na hili ni muhimu sana kwa kuongeza mapato ya chuo na kusaidia shughuli nyingine za kimaendeleo za chuo," alisema Prof. Oreku.

Alisema mapendekezo ya utafiti yakiandikwa vizuri kitaalamu na kibobezi yatashinda na kuwa sehemu ya kukitangaza chuo na kukaribisha wafadhili na wadau wa maendeleo ambao watawekeza kwa kuanzisha miradi mbalimbali kwa kushirikiana na chuo.

Mkurugenzi wa Utafiti, Machapisho na Ubunifu wa OUT, Dk. Harrieth Mtae, alisema mafunzo hayo yanalenga kuongeza ujuzi wa uandishi wa kiushindani kwa wanataaluma wa chuo hicho katika kuandika mapendekezo ya utafiti na miradi itakayoshinda kutokana na ubora wake.

Mratibu Mwandamizi wa Utafiti kutoka Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Bestina Daniel, alikumbusha watafiti kusajili utafiti wao na kupata kibali kabla ya kuanza kufanya utafiti ili kuhakikisha wanafuata sheria, maadili na taratibu za nchi.

"Wakati mwingine utafiti hasa wa kimataifa unaohusisha watafti kutoka nje ya nchi unaweza kuwa kwao ni sahihi lakini nchini kwetu ukawa hauendani na sheria, tamaduni au miiko yetu, hivyo usajili wa utafiti ili kupata kibali ni muhimu sana kwa watafiti wote," alitoa angalizo.

# Ugonjwa wasababisha shule kufungwa Kenya

**NAIROBI,** Kenya

WIZARA ya Elimu nchini Kenya imefunga shule ya upili ya wasichana ya St Theresa's Eregi baada ya wanafunzi 90 kulazwa hospitalini kutokana na ugonjwa wa ajabu.

Ilielezwa kuwa jana maofisa wa elimu katika Kaunti ya Kakamega walifikia hatua ya kufunga kwa muda shule hiyo baada ya wanafunzi kuibua ghasia.

**Hata hivyo, taarifa hiyo ilisema wanafunzi wa kidato cha 4 wanaotarajiwa kuanza mitihani yao watabakia shuleni.**

Pia ilibainishwa kuwa wanafunzi hao walikuwa wanataka kuruhusiwa kurudi nyumbani baada ya idadi hiyo ya wanafunzi kulazwa katika hospitali mbalimbali kutokana na mlipuko wa ugonjwa ambao jina lake halikubainishwa.

Taarifa ya Serikali ya Kaunti mlipuko huo ulipotokea, ilisema kuwa Bodi ya Usimamizi, Maofisa wa Wizara ya Elimu na Tume ya Utumishi wa Walimu walifanya mashauriano kabla ya uamuzi wa kufunga shule kutolewa.

Hata hivyo, taarifa hiyo ilisema wanafunzi wa kidato cha 4 wanaotarajiwa kuanza mitihani yao watabakia shuleni.

Vile vile, ilielezwa kuwa baada ya tukio hilo kujiri maofisa wakuu wa kaunti wakiongozwa na Mwanachama wa Kamati Tendaji ya Kaunti ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Bonface Okoth na mwenzake wa Huduma za Afya Benard Wesonga walitembelea shule hiyo ili kujionea hali halisi ilivyo.

Okoth alisema sampuli za damu kutoka kwa wanafunzi walioathiriwa zimetumwa katika Taasisi ya Utafiti wa Matibabu ya Kenya (KEMRI) jijini Nairobi na Kisumu kwa uchunguzi zaidi. **BBC**




Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Dar es Salaam, Dismas Prosper (wa pili kushoto), akikabidhi msaada wa viti, meza na madawati vyenye thamani ya Sh. milioni 20 kwa Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo katika Shule ya Sekondari Tambaza, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya shule tatu za Sekondari za Tambaza na Jangwani na Shule ya Msingi Kiwalani. Kulia ni Mbunge wa Ilala na Naibu Spika wa Bunge, Mussa Azzan 'Zungu' na (kushoto) ni Meneja wa benki hiyo Tawi la Muhimbili, Frank Makungu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Papa ataka kurekebisha mustakabali wa kanisa

**VATICAN,** Roma

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis amesema kuna haja ya kurekebisha mustakabali wa kanisa hilo ili liwe mahala pa kumkaribisha kila mmoja, na sio kikwazo kinachosababishwa na hofu na itikadi.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua Sinodi ya XVI ya Maaskofu Ulimwenguni iliyofanyika mjini Vatican. Ikielezwa kuwa miongoni mwa ajenda zitakazotawala katika Sinodi hiyo ni pamoja na jukumu la wanawake na mtazamo wa kanisa kuhusu watu wanaoshiriki mapenzi ya jinsia moja.

Pia ilielezwa kuwa waumini wa Katoliki wanaopenda maendeleo wana matumaini kuwa Sinodi hiyo itachangia wanawake zaidi katika nafasi za uongozi, huku wahafidhina wakionya kuwa inaweza kuligawa kanisa.

Katika mahubiri yake, Papa Francis alikiri kuhusu mgawanyiko wa kiitikadi uliopo, akiwasihi waumini kuuweka pembeni na badala yake wamsikilize roho mtakatifu.

Aliongeza kwa kuwataka waumini kufanya sawa na alichokifanya Mtakatifu Francisco wa Asizi, aliyemaliza mgawanyiko uliojitokeza katika uongozi wake kwa ibada na upendo.

Kumekuwepo na wito wa kuwainua wanawake zaidi na kuwajumuisha katika ngazi za kufanya maamuzi kwenye kanisa, ikiwamo kuwa mashemasi, na kwa waumini wa kawaida wa Kikatoliki kuwa na sauti zaidi ndani ya utawala wa kanisa.

Ilielezwa kuwa wakati Papa Francis anaufungua mkutano huo wa kilele wa maaskofu, kundi dogo la waandamanaji lilikusanyika katika viwanja vya Mtakatifu Peter, Vatican wakitetea hatua ya wanawake kuwekwa wakfu.

"Tumekusanyika hapa Roma kwenye ufunguzi wa Sinodi ya Maaskofu. Tuko hapa kuhakikisha kwamba sauti zote zinajumuishwa, miito yote inakaribishwa, na kura zote zinahesabiwa," alifafanua Kate McElwee, Mkurugenzi Mtendaji wa Kongamano la Kuwekwa Wakfu kwa Wanawake. **DW**

## Shule zapatiwa madawati, meza

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kusaidia maendeleo ya elimu nchini, Benki ya NMB imekabidhi meza na madawati yenye thamani ya Sh. milioni 20 kwa shule tatu za Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam.

Hizo ni Shule ya Msingi Kiwalani, Shule ya Sekondari Tambaza na Shule ya Sekondari Jangwani. Kutolewa samani hizo ni utekelezaji wa Mkakati wa Uwekezaji kwa Jamii (CSI) wa benki hiyo mwaka huu.

Akizungumza wakati wa hafla fupi ya kukabidhi vifaa hivyo iliyofanyika katika Shule ya Sekondari ya Tambaza jijini jana, Meneja wa benki hiyo Kanda ya Dar es Salaam, Dismas Prosper alisema msaada huo unalenga kurejesha kwa jamii ambamo benki inafanya kazi.

Alisema sekta ya elimu ni miongoni mwa vipaumbele muhimu katika mkakati wa Uwajibikaji kwa Jamii wa benki yake na ndiyo sababu benki imekuwa inawekeza kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa sekta hiyo.

# SINGIDA FOUNTAIN GATE YAOTA 'TOP THREE' BARA

**Na Saada Akida**

BAADA ya kushindwa kufikia malengo katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Rais wa Singida Fountain Gate FC, Japhet Makau amesema sasa mikakati ya klabu hiyo ni kupambana na hatimaye kumaliza katika nafasi tatu za juu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Pia timu hiyo iliyotolewa kwa kufungwa mabao 4-2 na Future FC ya Misri imesema inahitaji kutwaa ubingwa wa Kombe la FA msimu huu.

**Akizungumza na Nipashe jana, Makau alisema kuondolewa katika michuano hiyo hakuwakatishi tamaa na sasa wanajiimarisha ili wafanye vizuri katika kila mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ili kufikia malengo.**

"Tukiachana na ligi, lengo letu lingine ni kuhitaji kufanya vizuri katika Kombe la FA, hapa tunahitaji kutwaa taji la michuano hiyo ili kurejea kwa mara ya pili kushiriki katika michuano ya kimataifa. Ni kweli hapa kati tulikutana na sintofahamu za makocha wetu akiwamo Ernest Middendorp kuondoka, hiyo changamoto kutokea kwenye timu ni kawaida, sasa tuko kwenye hatua za mwisho kumalizana na kocha wetu mpya," alisema Makau.

Aliongeza anaamini watakamilisha mchakato wa kupata kocha mpya baada ya mechi ya leo dhidi ya Mtibwa Sugar kwa ajili ya kukiongoza kikosi kwenye mechi inayofuata ya Oktoba 8, mwaka huu watakapoikaribisha Simba.

Kuhusu uwapo wa Kocha, Didier Gomes Misri akishuhudia Singida Fountain Gate ikicheza dhidi ya Future, amewataka mashabiki wa timu hiyo kuwa watulivu kwa sababu wanaleta mwalimu ambaye anaifahamu vyema Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Gomes ni mwalimu mzuri, alikuwapo Simba na alifanya vizuri, ninaimani kwa uwezo wake hakuna klabu au timu ambayo haitahitaji huduma yake, ila sijasema ndio kocha ambaye tuko naye katika mazungumzo," alisema Makau.

Mindendorp aliamua kuondoka nchini na kuachana na Singida Fountain Gate akisema yale yale yaliyotamkwa na Hans van Pluijm, ya viongozi kuingia upangaji wa kikosi.



Mchezaji wa Mamlaka ya Bandari (TPA), Aji Omari (kulia), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa timu hiyo, Hamis Mohamed walipokuwa katika mazoezi Uwanja vya Jakaya Kikwete Youth Park, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Dream Maker yazinduliwa tena

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya michezo ya kubahatisha ya BetPawa Tanzania imezindua awamu ya pili ya programu yake ya kuwasaidia Watanzania wenye mawazo chanya kutimiza ndoto zao inayojulikana kama 'Dream Maker'.

Kupitia awamu ya pili ya programu hiyo, Watanzania 20 wenye mawazo ya miradi yenye uwezo wa kubadilisha maisha yao na jamii inayowazunguka 'watashikwa mkono' na BetPawa na hivyo kutimiza ndoto zao.

Akizungumza jijini jana, Meneja Masoko wa BetPawa Tanzania, Borah Ndanyungu, alisema programu hiyo itahusisha mikoa mitatu ambayo ni Lindi, Mtwara na Ruvuma.

"Watu watakaokutana na basi maalum la Dream Maker watakaribishwa kupanda na kujaza fomu pamoja na kurekodi video kuhusu ndoto zao. Wengine ambao hawatapata fursa ya kukutana na basi, wanaweza kufanya hivyo popote pale walipo na kutuma kwa njia ya mtandao kwa kutumia hashtag #betPawaDreamMaker," alisema Ndanyungu.

Aliongeza fursa ipo wazi kwa kila Mtanzania mwenye umri kuanzia miaka 18 kujitokeza na kuyawasilisha miradi kwa kampuni hiyo.

"Katika programu hii ya Dream Maker, huhitaji kubashiri kabisa. Tueleze ndoto yako bila kujali ukubwa wake na sisi tutakusaidia kuitimiza na kukufanya kuwa mmoja kati ya wanufaika 20 wa msimu wa pili," aliongeza meneja huyo.

Aliongeza BetPawa itatembelea mikoa hiyo mitatu kwa magari ya matangazo yatakuwa yakihamasisha watu kujitokeza na kuelezea ndoto zao.

Msimu wa kwanza wa Dream Maker uliofanyika Septemba, mwaka 2021 jumla ya ndoto za Watanzania 13 zilitimizwa ikiwamo ujenzi wa nyumba mpya, viwanja vya michezo na ufunguzi wa biashara mpya.

## KMKM, Ngome kibaruani Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MZUNGUKO wa tano wa Ligi Kuu Zanzibar unatarajia kuendelea leo kwa Ngome FC kuwaalika KMKM SC kwenye Uwanja wa Mau A, Unguja huku kwenye Uwanja wa Finya Kisiwani Pemba Chipukizi itavaana na Maendeleo.

Kocha Msaidizi wa Ngome, Suleiman Mohamed "Mo" alisema baada ya kutopata matokeo mazuri katika michezo minne iliyopita, kikosi chake kimejipanga kurekebisha makosa na matarajio yake leo ni kuvuna alama tatu.

Mohamed alisema anajua atakutana na timu ngumu na yenye uzoefu mkubwa katika ligi hiyo lakini hilo halitampoteza matumaini ya kupata matokeo mazuri lakini wakiingia dimbani kwa tahadhari.

"Tunaenda kucheza na timu kubwa, tena ni bingwa mtetezi na pia mchezo wake wa nne alipoteza kwa kufungwa ugenini Pemba sawa na sisi, hivyo lazima tucheze kwa akili kubwa huku wachezaji wakifanya maamuzi ya haraka pale wanapopata mpira ili kujihakikishia ushindi," alisema kocha huyo.

Ngome yenye pointi mbili iko katika nafasi ya 15 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar.

## Tanzania Prisons yaanzisha timu ya wanawake

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Prisons imeanzisha timu ya soka ya wanawake itakayojulikana kwa jina la Prisons Queens, imeelezwa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo Ajabu Kifukwe (pichani) amesema Prisons Queens itaweka maskani yake kwenye Chuo cha Ufundi cha Magereza Ruanda kilichoko jijini Mbeya.



"Tunapenda kuwajulisha umma na wanamichezo wote kwa ujumla rasmi tumeanzisha rasmi timu ya wanawake itakayofahamika kama Tanzania Prisons Queens.

Kwa kuzingatia umuhimu wa timu hii hivi karibuni uongozi utafungua mtandao rasmi wa kijamii ya timu hiyo ili kusaidia upatikanaji wa habari na watu wafahamu maendeleo ya timu yetu," alisema Kifukwe.

Prisons inakuwa timu ya saba inayoshiriki Ligi Kuu Bara na Tanzania ndio inashikilia ubingwa wa Afrika Mashariki kwa Wanawake baada ya JKT Queens kutwaa taji lililokuwa linashikiliwa na Simba Queens.

## ZISIKUPITE

### SANCHO KUREJEA DORTMUND

KUNA uwezekano mkubwa wa winga wa England, Jadon Sancho kuondoka Manchester United wakati wa uhamisho wa Januari, huku Borussia Dortmund wakipania kumrejesha mchezaji huyo kwenye Ligi Kuu Ujerumani maarufu Bundesliga. ***(Sky Germany)***

### BRANTWAITE ANUKIA UNITED

MLINZI wa Everton na England wa chini ya miaka 21, Jarrad Branthwaite yupo kwenye orodha ya wachezaji wanaonyatiwa na Manchester United katika dirisha lijalo la uhamisho. ***(Mail)***

### LAMPARD KUTUA RANGERS

FRANK Lampard yuko tayari kuzungumza na Rangers kuhusu nafasi iliyo wazi ya ukocha huku klabu hiyo ikianza mchakato wa kutafuta mbadala wa kudumu wa Michael Beale. ***(Telegraph)***

### MESSI KUREJEA OLD BOYS

GWIJI wa Argentina, Lionel Messi, 36, ameripotiwa kutaka kurejea katika klabu yake ya kwanza, Newell's Old Boys mara mkataba wake na Inter Miami utakapokamilika mwaka 2025. ***(Mirror)***

### 777 PARTNERES KUSHTAKIWA

LEEDS United, Leicester City na Burnley wameandika barua ya pamoja kwa wamiliki wapya watarajiwa wa Everton ambao ni 777 Partneres kwa kosa la klabu hiyo kulipa pauni milioni 30 iwapo watapatikana na hatia ya kukiuka sheria za matumizi ya Ligi Kuu England. ***(Mail)***

### OSIMHEN KUTUA CHELSEA

CHELSEA inapewa nafasi kubwa ya kumsajili mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen, 24, kutoka Napoli msimu ujao, huku Evan Ferguson wa Brighton (18), na Ivan Toney (27) wa Brentford pia akiwa miongoni mwa washambuliaji wanaolengwa. ***(Caught Offside)***

### BARCA KUJIPANGA UPYA

BARCELONA inatarajiwa kupokea ofa ya wachezaji wote wa kikosi cha kwanza kwani klabu hiyo bado inazidisha kikomo cha matumizi ya kila mwaka ya euro milioni 270 iliyowekwa na LaLiga. ***(Sport)***

### MODRRIC KUELEKEA MIAMI

KIUNGO wa kati wa Croatia, Luka Modric ambaye amekuwa akihusishwa na kuhamia Inter Miami anaweza kuondoka Real Madrid huku klabu hiyo ya Hispania ikihisi uchezaji wa nyota huyo mwenye umri wa miaka 38 umeshuka. ***(Football Espana)***

### FRIMPONG MAMBO SAFI

MLINZI wa Bayer Leverkusen, Jeremie Frimpong (22), anatazamiwa kusaini mkataba mpya na klabu hiyo ya Ujerumani, na hivyo kuongeza thamani ya uhamisho wa mchezaji anayeivutia Manchester United na Real Madrid. Hilo linaweza pia kufaidisha klabu yake ya zamani ya Celtic, ambayo ina kipengele cha kupata asilimia 30 ya mauzo. ***(Daily Record)***

### AWANIWA FC BARCELONA

BARCELONA inapania kumjumuisha mshambuliaji wa Athletico Paranaense na Brazil, Vitor Roque mwenye umri wa miaka 18, katika klabu hiyo Januari badala ya Julai huku Mkurugenzi wa Michezo, Deco akipanga kusafiri hadi Brazil wakati wa mapumziko yajayo ya kimataifa. ***(Goal)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA AHOFIA AFYA YA SAKA

**LENS,** Ufaransa

●●● Lakini kocha huyo asema hajutii uamuzi wake wa kumwanzisha...

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta alikiri majeraha ya hivi karibuni zaidi ya Bukayo Saka ni ya "wasiwasi" lakini akasisitiza hana majuto kwa kumwanzisha winga huyo katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya waliyochapwa mabao 2-1 na Lens hapo juzi.

**Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 alikuwa amekaa nje katika mechi mbili za awali za Washikabunduki hao za Ligi Kuu England, lakini alijumuishwa kwenye kikosi kilichocheza kwenye Uwanja wa Bollaert-Delelis, ambapo alimudu kwa dakika 34 pekee kabla ya kulazimika kutoka nje kutokana na jeraha la misuli.**

Saka alitengeneza bao la ufunguzi la Gabriel Jesus kabla ya Adrien Thomasson kusawazisha na Elye Wahi kufunga bao la ushindi dakika ya 69 na kuisababishia Arsenal kichapo cha kwanza msimu huu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England sasa huenda akafanyiwa uchunguzi ili kubaini ukubwa wa tatizo hilo na kuna shaka ya kuwapo kwenye mechi ya Jumapili ya Ligi Kuu England dhidi ya Mabingwa watetezi, Manchester City.

"Alijaribu kurudisha mpira nyuma katika kipindi cha kwanza na alihisi kitu," alisema Arteta. "Kulikuwa na kitu chenye misuli. Hakuwa na raha na ilibidi tumwondoe.

"Hatujui lolote zaidi ya hilo. Ni wazi, ilikuwa kubwa kiasi cha kutomruhusu kuendelea kucheza mchezo huo na ni wazi ni wasiwasi kwetu.

"Sijui, kuhusu wikendi, sijui."

Alipoulizwa kama alikuwa na majuto yoyote ya kumwanzisha Saka kutokana na matatizo yake ya hivi majuzi ya utimamu wa mwili, Arteta alijibu: "Hapana, ilikuwa ni goli ambalo alikuwa nalo.

"Alikuwa sawa kabisa. Ilikuwa ni hatua, kisigino, ambacho kinaweza kutoa aina hiyo ya kuumia, tutaona ukubwa wake ni kiasi gani.

"Michezo michache iliyopita ilikuwa ya kugonga kuliko kitu kingine chochote. Hajakosa mechi. Tulimpa mapumziko dhidi ya Brentford wiki iliyopita."

Arsenal wamesalia na pointi tatu katika Kundi B na Arteta aliongeza: "Nilichora picha na aina ya mazingira ambayo tungekabiliana nayo leo (juzi) na wote walijua kuhusu hilo. Lakini Ligi ya Mabingwa Ulaya ni ngumu."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,159,5

MECHI KALI

TANZANIA PRISONS VERSUS SIMBA SC

1 | 7.91
X | 4.45
2 | 1.35

tigo pesa SportPesa

WASHINDI WA MAOKOTO Deilee!

1. Ramadhani Mtumba - 0653 380 XXX
2. Salhina Kimbekete - 0656 004 XXX
3. Fabian Ramadhan - 0658 920 XXX
4. Hamisi Lauka - 0659 342 XXX
5. Juliana Mollel - 0673 970 XXX
6. Awena Rajab - 0676 969 XXX
7. Peter Nyato - 0677 904 XXX
8. Pendo Malang'wa - 0679 501 XXX
9. Eliza Davide - 0712 102 XXX
10. Yohana Mkwavi - 0714 130 XXX

20,000/= KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# BELLINGHAM: NAFURAHIA KUCHEZA NA VINICIUS JR

**NAPLES,** Italia

JUDE Bellingham alisifu ushirikiano wake na Vinícius Jr akimwita mshambuliaji huyo "bora zaidi duniani" -- baada ya wawili hao kuwa kwenye ukurasa wa mabao katika ushindi wa 3-2 wa Real Madrid kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Napoli iliyochezwa juzi usiku.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England alitoa pasi kwa Vinicius aliyefunga bao la kusawazisha baada ya Leo Ostigard kuwaweka wenyeji mbele kwenye Uwanja wa Diego Armando Maradona, na Bellingham akaiweka Madrid mbele kwa mabao 2-1 kabla ya muda wa mapumziko.

Piotr Zielinski alifanya mambo kuwa 2-2 kwa penalti kabla ya Federico Valverde kupiga shuti lililompita kipa, Alex Meret na kutinga wavuni na kuipa Madrid pointi zote tatu, na kuwaacha kileleni katika Kundi C.

"Pengine ndiye bora zaidi duniani kwa upande kwangu," alisema Bellingham akiiambia Movistar, alipoulizwa kuhusu ushirikiano wake na Vinicius.

"Yeye ni mmoja wa wachezaji wenye vipaji zaidi ambao nimewahi kucheza nao."

Bellingham sasa amefunga mabao nane katika mechi tisa za kwanza akiwa na Real Madrid katika mashindano yote.

"Ninajiamini, lakini sikujua itakuwa nzuri hivi," alisema. "Nina deni kwa wafanyakazi na wachezaji wenzangu."

Bao la Bellingham ambalo lilimwona kiungo huyo akiuchukua mpira ndani ya nusu ya wapinzani kabla ya kuanza kukimbia peke yake -- lililinganisha lile na nguli wa zamani wa Napoli na Argentina, Maradona.

# Ten Hag alalamikia kichapo



**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag amelaani "makosa ya kiakili" ambayo yalichangia kufungwa kwa Manchester United na Galatasaray katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya uliochezwa juzi.

Mashetani Wekundu walikuwa mbele mara mbili wakati wa mchezo huo uliochezwa kwenye Uwanja wa Old Trafford, lakini hatimaye walipoteza 3-2 baada ya makosa kadhaa ya safu ya ulinzi - ikiwa moja la Andre Onana na kumfanya Casemiro kuonyeshwa kadi nyekundu kwa kucheza rafu eneo la hatari.

Kipigo hicho kilikuwa cha sita kwa United katika msimu ambao umekuwa mbaya zaidi hadi sasa, na klabu hiyo iko mkiani katika kundi lake baada ya kufungwa mechi zao mbili walizocheza.

Akizungumzia kufungwa huko TNT Sports, Ten Hag alisema kulikuwa na makosa ambayo wachezaji wake walifanya usiku huo.

"Tulifanya makosa ya kiakili, huwezi kuyaruhusu katika kiwango hiki. Unaadhibiwa. Hii ni ngumu kudhibiti. Sote tuko pamoja katika hili. Tulikuwa juu mara mbili na kudhibiti mchezo. Tunatarajia zaidi pamoja."

Kosa moja kama hilo lilitoka kwa nyota Marcus Rashford. Huku timu yake ikiwa sare ya 1-1 katika kipindi cha pili, fowadi huyo alibaki yeye na beki, lakini badala ya kupiga shuti, akajaribu kutoa pasi kwa Bruno Fernandes, pasi ambayo haikutoka.

Ten Hag alitoa maoni yake juu ya tukio hilo, akisema: "Hiyo ni juu ya Marcus. Kwa wakati kama huo lazima afanye uamuzi."






574,731/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 07/10/23 | 19:30 | Mallorca vs Valencia | 2.45 | 3.05 | 2.90 |
| 02. 07/10/23 | 19:30 | Werder Bremen vs Hoffenheim | 2.70 | 3.65 | 2.29 |
| 03. 07/10/23 | 22:00 | Reims vs Monaco | 2.60 | 3.55 | 2.42 |
| 04. 08/10/23 | 15:15 | FC Lugano vs Servette Geneva | 2.12 | 3.45 | 2.80 |
| 05. 08/10/23 | 16:00 | Frosinone vs Verona | 2.26 | 3.30 | 3.00 |
| 06. 08/10/23 | 16:00 | Lazio vs Atalanta | 2.55 | 3.25 | 2.60 |
| 07. 08/10/23 | 16:00 | Tanzania Prisons vs Mtibwa Sugar | 2.25 | 2.80 | 3.40 |
| 08. 08/10/23 | 16:00 | GIF Sundsvall vs IK Brage | 2.48 | 3.20 | 2.48 |
| 09. 08/10/23 | 16:00 | Brighton vs Liverpool | 2.80 | 3.80 | 2.18 |
| 10. 08/10/23 | 16:00 | Wolverhampton vs Aston Villa | 3.30 | 3.40 | 2.07 |
| 11. 08/10/23 | 16:00 | West Ham vs Newcastle | 3.00 | 3.55 | 2.14 |
| 12. 08/10/23 | 17:30 | Lausanne-Sport vs FC Luzern | 2.44 | 3.35 | 2.42 |
| 13. 08/10/23 | 17:30 | Famalicao vs Vitoria Guimaraes | 2.55 | 3.15 | 2.70 |
| 14. 08/10/23 | 18:05 | Lens vs Lille | 2.15 | 3.45 | 3.05 |
| 15. 08/10/23 | 18:30 | Arsenal vs Manchester City | 2.70 | 3.35 | 2.43 |
| 16. 08/10/23 | 18:30 | Hammarby vs Hacken | 2.35 | 3.35 | 2.50 |
| 17. 08/10/23 | 19:30 | Alaves vs Betis | 2.75 | 3.10 | 2.55 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 05/10/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 5447 | Artsakh vs Bkma Yerevan | 1.40 | 4.37 | 6.30 |
| 15:00 | 1830 | Dhamk vs AL Hazm | 1.80 | 3.62 | 4.19 |
| 15:00 | 3054 | Phnom Penh vs Shan United FC | 1.92 | 3.61 | 3.30 |
| 15:00 | 3856 | Tainan City FC vs Cpk | 1.64 | 3.70 | 4.20 |
| 15:00 | 4594 | Hougang United vs Hai Phong | 4.69 | 3.87 | 1.59 |
| 15:00 | 4889 | Merw Mary vs FC Abdysh-Ata Kant | 2.95 | 3.35 | 2.05 |
| 15:00 | 5785 | PSM Makassar vs Sabah | 1.78 | 3.35 | 3.85 |
| 16:00 | 1398 | Mtibwa Sugar vs Singida BS FC | 2.59 | 2.84 | 2.84 |
| 16:00 | 2132 | Masr vs Baladiyyat AL Mehalla | 2.06 | 2.90 | 3.94 |
| 16:00 | 2670 | Tanzania Prisons vs Simba | 7.91 | 4.45 | 1.35 |
| 17:30 | 5784 | Astana vs Viktoria Plzen | 3.19 | 3.59 | 2.05 |
| 18:00 | 2126 | Al Taawon vs AL Tai | 1.60 | 3.98 | 5.13 |
| 18:00 | 4630 | AL Riyadh vs Al Shabab Riyadh | 5.65 | 4.29 | 1.52 |
| 19:00 | 3515 | Smouha Club vs Arab Contractors | 2.50 | 3.00 | 2.85 |
| 19:45 | 1068 | Marseille vs Brighton | 2.70 | 3.60 | 2.31 |
| 19:45 | 1360 | KAA Gent vs Maccabi Tel Aviv | 1.76 | 3.75 | 4.10 |
| 19:45 | 1640 | KF Ballkani vs Dinamo Zagreb | 4.30 | 3.75 | 1.72 |
| 19:45 | 2289 | KI Klaksvik vs Lille | 7.22 | 4.81 | 1.36 |
| 19:45 | 2658 | Sporting Lisbon vs Atalanta | 2.18 | 3.40 | 3.05 |
| 19:45 | 2806 | Betis vs Sparta Prague | 1.75 | 3.87 | 4.02 |
| 19:45 | 2836 | Olimpija Ljubljana vs Slovan Bratislava | 2.30 | 3.40 | 2.85 |
| 19:45 | 2945 | Breidablik vs Zorya Lugansk | 2.76 | 3.56 | 2.29 |
| 19:45 | 3018 | Besiktas vs FC Lugano | 1.37 | 4.79 | 7.18 |
| 19:45 | 3057 | Aris Limassol vs Rangers | 3.70 | 3.60 | 1.88 |
| 19:45 | 3139 | Bodo Glimt vs Brugge | 2.50 | 3.49 | 2.55 |
| 19:45 | 3450 | Rakow Czestochowa vs Sturm Graz | 2.33 | 3.26 | 2.91 |
| 19:45 | 4077 | AEK Athens vs Ajax | 2.13 | 3.61 | 3.01 |
| 19:45 | 4467 | Backa Topola vs Olympiakos | 5.19 | 4.09 | 1.56 |
| 19:45 | 4605 | SC Freiburg vs West Ham | 2.49 | 3.43 | 2.58 |
| 20:30 | 2988 | Sekhukhune United vs Golden Arrows | 2.62 | 2.82 | 2.82 |
| 21:00 | 1737 | Al-Ettifaq vs Al Fateh (KSA) | 1.96 | 3.71 | 3.45 |
| 22:00 | 1065 | BK Hacken vs Karabakh | 2.47 | 3.35 | 2.65 |
| 22:00 | 1150 | Roma vs Servette Geneva | 1.15 | 6.82 | 15.05 |
| 22:00 | 1178 | Toulouse vs LASK Linz | 1.79 | 3.66 | 4.01 |
| 22:00 | 1349 | Maghreb Tetouan vs FUS Rabat | 2.57 | 3.02 | 2.57 |
| 22:00 | 1771 | Fiorentina vs Ferencvaros TC | 1.45 | 4.49 | 5.99 |
| 22:00 | 2103 | Spartak Trnava vs Fenerbahce | 5.39 | 4.49 | 1.49 |
| 22:00 | 2598 | Molde vs Bayer Leverkusen | 6.39 | 4.80 | 1.40 |
| 22:00 | 2646 | Villarreal vs Rennes | 2.00 | 3.55 | 3.35 |
| 22:00 | 2684 | Slavia Prague vs Sheriff Tiraspol | 1.37 | 4.69 | 7.38 |
| 22:00 | 3789 | AZ Alkmaar vs Legia Warszawa | 1.66 | 3.85 | 4.60 |
| 22:00 | 3824 | Liverpool vs Union Saint Gilloise | 1.20 | 6.57 | 10.96 |
| 22:00 | 4140 | Aston Villa vs Zrinjski Mostar | 1.10 | 8.37 | 20.92 |
| 22:00 | 4553 | Maccabi Haifa vs Panathinaikos | 2.25 | 3.36 | 2.96 |
| 22:00 | 5312 | PAOK vs Eintracht Frankfurt | 2.70 | 3.36 | 2.55 |
| 22:00 | 5469 | Nordsjalland vs Ludogorets Razgrad | 1.72 | 3.85 | 4.20 |
| 22:00 | 5863 | Cukaricki St vs Racing Genk | 4.79 | 4.09 | 1.60 |
| 22:00 | 5937 | Aberdeen vs HJK Helsinki | 1.85 | 3.77 | 3.92 |
| 22:30 | 2005 | Racing Ferrol vs Amorebieta | 1.80 | 3.22 | 4.46 |
| 22:30 | 4088 | FC Cartagena vs Espanyol | 3.63 | 3.33 | 1.95 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# SPORTPESA YAIPONGEZA YANGA KUTINGA HATUA MAKUNDI CAF

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya burudani na michezo SportPesa imeipongeza Yanga kwa kufanikiwa kuingia hatua ya makundi katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Yanga ambao ni mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara wametinga hatua ya makundi baada ya kuwaondoa Al Merrikh ya Sudan kwa jumla ya mabao 3-0.

Akizungumza kutoka makao makuu ya ofisi za SportPesa jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya SportPesa, Abbas Tarimba amewapongeza wachezaji na viongozi wa Yanga kwa kufanikiwa kuingia hatua hiyo katika michuano ya msimu huu ambayo bado inaendelea.



"Sisi tukiwa wadhamini wakuu tunafarijika kuona mafanikio ya timu ya Yanga kwa jinsi inavyopiga hatua kubwa katika soka la Tanzania na kimataifa," alisema Tarimba.

Bosi huyo aliongeza wanaitakiwa mafanikio zaidi Yanga katika mechi zake zinazofuata na wanaamini wataendelea kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania.

"Tunawatakia kila la heri kwenye mechi zijazo za hatua ya makundi katika kuipeperusha bendera ya Tanzania. Tunawapongeza viongozi wakiongozwa na Rais Hersi Saidi na pia wachezaji wote," Tarimba alisema.

Aliongeza SportPesa itaendeleza juhudi zake katika kuunga mkono, kuipa thamani na kuinua sekta ya michezo Tanzania.

## Majaliwa afunguka

INATOKA UK. 24

fanyia kazi ombi la Rais wa Shirikisho, Wallace Karia, juu kuomba usafiri wa ndege kwa timu ya taifa, usafiri wa kuwapeleka Morocco kwenye mechi ya kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia 2026 dhidi ya Morocco ," alisema Majaliwa.

Alimtaka Waziri ya Fedha kutoa asilimia tano ya fedha za mchezo wa kubashiri ziende kwa wakati kwenye mfuko husika ili kuhakikisha utekelezaji wa maendeleo ya michezo.

"Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Michezo Ally Mayai na Katibu Mkuu wa BMT, Neema Msitha mhakikishe taifa linavuka hapa lilipo na kusonga mbele zaidi kimataifa.

Hivi karibuni tutampokea Rais wa Fifa, Gianni Infantino, atakuja hapa nchini kushuhudia mechi ya ufunguzi ya michuano ya Africa Football League, kati ya Simba dhidi ya Al Ahly, lakini pia ataenda kutembelea visiwani Zanzibar na Kigoma, matembezi hayo itakuwa ni moja ya kuinua uchumi wa nchi," alisema.

Kiongozi huyo pia amewataka makocha na wachezaji wazawa kujitathimini kwanini hawapati nafasi ya kwenda kucheza na kufundisha soka nje ya Tanzania.

Alizitaja nchi kama Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Burundi na Kenya wachezaji na mako-




Mshindi wa Jackpot bonus kutoka SportPesa, Kaitani Materu akiwa ameshikilia zawadi yake ya mfano wa hundi ya Sh. milioni 5.9 baada ya kubashiri kwa usahihi baadhi ya mechi za Jackpot. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Yanga yatepeta*

INATOKA UKURASA 24

Kuelekea mchezo huo, Robertinho alisema wamejiandaa vizuri na anawakumbuka vizuri wapinzani wao kutokana na ushindani waliowapa msimu uliopita.

"Mara zote tunapokutana na Prisons mchezo unakuwa mgumu, lakini tupo tayari kupambana nao lengo likiwa kuhakikisha tunaondoka na alama tatu," alisema kipa wa Simba, Hussein Abel.

Minziro alisema maandalizi ya timu yake yamekamilika na ataingia kwenye mchezo huo akiiheshimu Simba ingawa lengo lake ni kutafuta pointi tatu na kujiweka katika mazingira mazuri zaidi kwenye msimamo.

"Simba ni timu kubwa ambayo mwaka huu imekuwa katika kiwango kizuri katika mashindano mbalimbali wanayoshiriki, tumeyafanyia kazi mapungufu machache ambayo tumekuwa nayo katika baadhi ya maeneo na sasa tuko tayari kwa ajili ya mchezo," alisema Minziro.


# Michezo

Alhamisi Oktoba 5, 2023

Nipashe




Arteta ahofia afya ya Saka UKURASA 21




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kushoto), akimkabidhi Rais wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF), Wallace Karia (kulia), hundi ya mfano ya Sh. milioni 500 kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), ambayo imefuzu kucheza fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2024). Katikati ni Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro. **PICHA: SAADA AKIDA**

# Yanga yatepeta Mbarali

## Yakubali kichapo tena, Simba, Prisons hapatoshi Sokoine...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

KWA mara nyingine tena, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wamepoteza mechi kwenye Uwanja wa Highland Estates ulioko Mbarali, Mbeya dhidi ya wenyeji Ihefu kama ilivyokuwa katika mchezo wa msimu uliopita wa ligi hiyo.

**Idadi ya mabao ni ile ile ya 2-1 na mmoja wa wafungaji akiwa ni yule yule, Lenny Kissu, lakini safari hii akifunga bao la kwanza badala ya la pili kama alivyofanya Novemba 29, mwaka jana.**

Kipigo hicho cha Yanga dhidi ya Ihefu, kinakumbushia machungu ya msimu uliopita ilipopoteza mechi kwa mara ya kwanza baada ya kucheza mechi 49 bila kufungwa.

Ni mechi ya kwanza Yanga kupoteza msimu huu, ikiwa ni mechi ya kwanza pia ugenini ikibakiwa na pointi zake tisa kwenye mechi nne ilizocheza.

Yanga ilianza kuishtua Ihefu dakika ya tatu tu ilipopachika bao la kwanza lililowekwa wavuni na Pacome Zouzoua, lakini goli lake la pili msimu huu baada ya kazi kubwa iliyofanywa na Clement Mzize.

Never Tegere angeweza kusababisha wenzake kupata bao dakika ya 14, baada ya kuambaa na mpira winga ya kushoto lakini alipiga krosi kwa ya juu iliyotoka nje huku wenzake wakiwa wanaisubiri langoni.

Dakika moja baadaye aliwatoka tena walinzi na Yanga na kuachia shuti lililopanguliwa kwa ustadi na kipa wa Yanga, Djigui Diarra na kuzaa kona ambayo nayo pia ilileta kizaazaa.

Baada ya jitihada nyingi, Ihefu ilifanikiwa kusawazisha bao dakika ya 40 likifungwa na Kissu.

Msimu uliopita alifunga bao dakika ya 62 lililotokana na kona ya Tegere, jana alifunga dakika ya 40 kutokana na mpira wa faulo ya Tegere pia.

Mzimbabwe huyo alipiga faulo iliyotokana na Bakari Mwamnyeto kumchezea madhambi Saadun, kipa Diarra alifanya kazi kubwa kuuokoa mpira uliokuwa unatinga wavuni, lakini ulikwenda juu na kurejea kwenye usawa wa lango, mfungaji akaruka juu na kuujaza wavuni.

Kipindi cha pili, timu zote zilifanya mabadiliko, Yanga ikiamua sasa kuwaingiza wachezaji wake tegemeo kama Yao Kouassi, Stephane Aziz Ki, Khalid Aucho, Mudhathir Yahaya lakini ukuta wa Ihefu, ukiwa na Kissu, Kenneth Kunambi, Victo Akpan na nahodha Juma Nyosso walikaa imara kulinda lango lao.

Yanga ikionekana kabisa haikuwa kwenye kiwango chao kilichozoeleka, ilijikuta ikipachikwa bao la pili lililofunga na Charles Ilamfya dakika ya 66.

Lilikuwa ni shambulizi la kushtukiza, baada ya Yanga kufanya shambulizi, lilirudishwa na Ihefu, mpira ukapigwa krosi wingi ya kulia, Akpan akauruka na kuwapoteza maboya mabeki wa Yanga na kipa wao, Diarra, mfungaji akaunganisha kwa mguu wa kulia, mpira ukajaa kwenye nyavu za juu.

Dakika za lala salama kulitokea tafrani baada ya baadhi ya mashabiki wanaodhaniwa ni wa Yanga kurusha chupa za maji kwenye lango la Ihefu na kusababisha kipa, Fikirini kuondoka kwa muda na mpira ulisimama hadi hali ilipotulia.

Wakati huo huo Simba inatarajia kuwavaa wenyeji Tanzania Prisons katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini Mbeya huku Wekundu wa Msimbazi wakionekana wanahitaji kulipa kisasi.

Kikosi cha Simba kinachonolewa na Mbrazil Roberto Oliviera 'Robertinho' itamkosa nyota wake, Luis Miquissone ambaye aliumia katika mazoezi ya kuivaa Power Dynamos pamoja na Aishi Manula, Hennock Inonga na Aubin Kramo ambao ndio wameanza mazoezi mepesi.

INAENDELEA UKURASA 23

# Majaliwa afunguka uraia pacha AFCON 2024

**Na Saada Akida**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ameitaka Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani kuangalia namna itakavyoweka mwongozo wa kusaidia wachezaji wenye asili ya Tanzania wanaocheza nje wenye viwango vya juu kuongeza nguvu kwa kujiunga na Timu za Taifa.

Majaliwa amesema hayo jana wakati anakabidhi kiasi cha Sh. milioni 500 kwa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), ambacho kilikuwa ni ahadi iliyotolewa na Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kukata tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2024).

Fainali za AFCON zitafanyika kuanzia Januari 13, mwakani huko nchini Ivory Coast.

Alisema anaimani kuna wachezaji wazuri walioko nje wenye asili ya Tanzania ambao wanaweza kusaidia nchi katika mashindano mbalimbali yanayozikabili timu za Taifa ikiwamo soka.

Waziri huyo alisema zinatakiwa wizaea hizo mbili kukaa pamoja ili kuangalia uwezekano wa kupata wachezaji nyota watakaozitumikia timu za taifa kwa kufuata sheria na taratibu za nchi.

Alisema pia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo inatakiwa kushirikiana kwa karibu na wadau ili kupatiana fedha kwa haraka ili kuhakikisha maandalizi ya mashindano ya AFCON yanakamilika kwa wakati ikiwamo ujenzi wa viwanja vya mazoezi kukamilika mapema.

"Ninataka kuona fedha zinapatikana kwa uharaka na kutumika kwa wakati sahihi pamoja na Baraza la Michezo la Taifa (BMT) kuandaa mikakati inayowezesha timu za taifa kushinda michuano ya kimataifa.

Pia washirikiane na TFF kwa ajili ya kuandaa mipango thabiti wa kuhakikisha Timu ya Taifa inashinda mechi zake zote, nali-

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >